# Tembe Kajimezea

***Tembe Kajimezea*** *ni hadithi ya kusisimua inayojenga taswira kamili kwenye akili ya msomaji na kumwacha mwenye shauku ya kujua linalotendeka katika sentensi inayofuatia. Inamhusisha 'Sheha', kijana wa makamo ambaye yuko kwenye safari ya kutafuta kiini hasa cha kukosa kazi baada ya kusoma na kuhitimu chuo kikuu. Je, ni kutokana na mambo ya tamaduni au ni sadfa tu ya maisha? Aidha, ni hadithi inayokuza maadili kwenye jamii na kuimarisha ushirikiano na umoja.*

**Jared K. Mwanduka**

**Tembe Kajimezea** © Jared K. Mwanduka

**Imechapishwa kwa mara ya kwanza 2022**

Haki zote zimehifadhiwa. Ni marufuku na hatia kwa wenye silika za kugushi, kuiga, kubadili, kuchapisha, kutafsiri, kuigiza au kutumia mbinu zozote bila idhini ya mwandishi na/au wachapishaji.

Mtu yeyote atakayefanya kitendo chochote kinyume cha sheria ataweza kushtakiwa.

**ISBN 9798805937973**

# Tabaruku

Kwa **Annah Mukethe** na **Kister Mukiti**, kwa kunisaidia katika uhariri wa nakala hii, hivyo kunipa fursa ya kuwasilisha kazi isiyo na dosari kwa msomaji.

**-Mwenyezi Mungu awabariki.**

# YALIYOMO


Tabaruku ........ iii

SURA YA KWANZA ........ 5

SURA YA PILI ........ 18

SURA YA TATU ........ 32

SURA YA NNE ........ 43

SURA YA TANO ........ 55

SURA YA SITA ........ 66

SURA YA SABA ........ 74

SURA YA NANE ........ 84

SURA YA TISA ........ 92

SURA YA KUMI ........ 100

# SURA YA KWANZA

Safari yetu iling'oa nanga asubuhi na mapema siku ya Jumamosi. Hii ilikuwa siku iliyobeba umuhimu wa kiasi cha haja kwa wafanyakazi wa kampuni ya Ujadi Mills. Kila mtu alionekana kuwa tayari kwa safari. Wanawake walikuwa wamebeba mifuko iliyofutuka kama hamri lililotiwa hamira. Kama kawaida ya jinsia hii, kwao ni lazima kama ibada kusadikisha kuwa vitu kadha wa kadha vimo katika mabegi yao. Vifaa vya kujipodoa, kurembesha makucha, kope, midomo na nywele vikiwemo kati yao. Kwa fikra zangu, pengine hata vichana na vioo vya kujitazama havingekosekana kwenye mabegi yale kama yangefunguliwa. Kwa upande mwingine, wanaume wakionekana kubeba mifuko saghiri na hata wengine bila kuwepo na kitu chochote mikononi mwao. Kinyume na kawaida ya kufika kazini, siku hii mambo yalikuwa tofauti kabisa.

Kila mmoja wetu alifika saa kumi za mapambazuko, kusudi asije akaachwa na basi la kuwabeba watu. Kiini hasa cha kuweza kufika bila kuchelewa ni kutokana na kuwika kwa jogoo ambao wengi wa wakazi wa eneo letu walikuwa wakifuga. Jogoo alitumika sana katika kuwaamsha wanakijiji. Wakaweza kufahamu nyakati na saa tofauti zilizoashiriwa na kuwika kwa jogoo hao, hivyo basi, kawaida ikawa kama sheria. Uraibu wa kuwaweka kuku kwenye chumba cha malazi haukuwa jambo jipya katika eneo letu. Hata ingawa tuliishi karibu na mji mkuu, kulikuwa na jogoo wa shamba walioweza kuwika mjini. Wanakijiji waliamini kuwa ndege hao wakijengewa chumba chao kando na chumba cha watu ni sawa na kukaribisha ufakiri katika familia. Kwa kweli, aliyekuwa keshafika lazima alirauka na jogoo la pili.

Naam, kila nafsi ilikuwa na lengo tofauti la kuweza kufika mapema zaidi ya mwenzake. Malengo hayo yote yalikuwa katika fikra zao walipopiga hatua moja hadi nyingine kuelekea kwenye basi lile. Kuna

wale waliofika kwa shabaha ya kuketi karibu na madirisha ya basi lile kubwa ili waweze kuyatazama mandhari ya safari kwa utaratibu, walikuwepo waliokusudia kuketi karibu na dereva kwa minajili ya kuona namna gari linavyoendeshwa na wengine walikuwa na lengo la kutaka kujua nani alikuwa kabeba nini au pengine nani kaketi sako kwa bako na nani? Malengo niliyoyataja hapa ni machache mno ikilinganishwa na wingi wa malengo waliokuwa wameyasitiri akilini mwao.

Nilipofika nilikuwa katika wakati mwafaka. Nilipata takriban watu watano hivi ndio waliokuwa tayari wamewasili. Isitoshe, basi nalo lilionekana kuwa tayari. Basi hili lilikuwa likiwaka kwa umaridadi mkubwa kwenye taa zake za mbele na nyuma. Taa kubwa kubwa za umeme nazo ziliweza kuangaza langoni mwa kampuni hii kubwa lililojulikana ndani na nje ya jiji kuu. Sifa zake ziliweza kufurika kote kijijini na kupita zaidi ya kingo za mji mkuu. Ikajitwalia sifa tele kutokana na kazi yake iliyowasaidia wengi wa kiwango cha chini kiuchumi na kujipatia kipato cha kila siku. Kweli, aisifuye mvua imenyea!

Basi namna kila mtu pale alivyokuwa na lake kichwani, mimi pia nilikuwa na lengo langu. Langu kuu lilikuwa kwenda kumwona binamu yangu aliyeishi mjini kwa madhumuni ya kupanga jambo fulani ambalo nililipa kipaumbele. Hatua hii ingenisaidia kubadilisha hadithi ya maisha yangu ya usoni kama sio yale ya kale. Kwa wakati huo, msururo wa mawazo ulikuwa umenisonga kichwani hadi nikakosa la kufanya. Mawazo hayo yaliyokuwa maswali bila majibu, yalikivamia kichwa changu na kushika mateka hisia zangu zote. Kwa muda nilihisi kana kwamba nilikuwa nikiogelea katika bahari lililojaa na mawimbi ya kutisha. Mawimbi ambayo yaliyokomesha juhudi za mikambi yangu kwenye maji. Namna mawimbi hayo yalivyokuwa yakivuruga bahari, ndivyo wanyama wakali wa majini walivyokuwa wakininyemelea kwenye ile vurugu. Nguvu zakaniishia, nikatoweka

kwenye hali ya kawaida. Hapo ndipo sauti ya binamu yangu iliponijia akilini. “Kazamoyo, wewe ni mwerevu na mwenye akili za juu sana kimasomo. Zaidi ya hayo, tabia zako hapa kijijini na mjini zimewakinaisha watu wote, wazee kwa vijana, maskini kwa matajiri. Maisha yako lazima yafane sana utakapohitimu masomo yako,” akasema. “Huwezi kuwa kama sisi tuliokosa misingi thabiti ya kuzingatia kwenye masomo yetu. Hatujui tutokako wala tuendako. Tufani inayokuja haitatubakisha. Itatuacha kwenye jangwa ama katikati ya bahari. Kwetu sisi tusiojua kuogelea wala kutembea kwa siku nyingi bila chakula na maji, tutasahaulika.” Akamalizia. “Kati yangu na binamu, nani mwenye maisha yenye mwanga? Nani mwenye masomo kuliko mwingine?” Nikajiuliza. “Basi mbona tembe yangu ya maisha ikawa chungu na zaidi kuniletea madhila badala ya tiba?” Nikaendelea kuwaza. Macho yangu yalijaa machozi yaliyokosa mfariji. Kwa muda, nikasahau kilichokuwa kimenileta hapo. Nikabubujikwa na machozi kwa njia nnenne. Machozi hayo yakalowesha ndevu zangu isitoshe upande mmoja wa shati la manjano nililokuwa nimevalia. Kwa kulitazama shati langu, umri wake ungelinganishwa na muda wa kutosha mtoto kuzaliwa, kutembea, kuongea na kujiunga na shule ya msingi hadi kuhitimu. Lilikuwa limezeeka kutokana na kuvaliwa takriban kila siku.

Mengi yalikuwa yamenikumba baada ya kuhitimu shahada ya uzamili na uzamifu kutoka mojawapo ya vyuo vikuu maarufu nchini. Nikavutiwa na kazi ya uwanasheria. Ndoto yangu ya kuwa mwanasheria tajika kijijini ikatimilika. Ikabakia ndoto ya kuwa mwanasheria tajika ulimwengu mzima. Sheria ya uraia ikawa ndio wimbo wangu wa kila siku. Nikawa suluhisho kwa wanyonge na waliodhulumiwa katika jamii. Waliokosa mwanasheria wa kuwakilisha kesi zao mahakamani wakanikimbilia kama guzo madhubuti kwa shida zao. Nikawa wakala kwa jamii nzima kwa maana kesi yoyote niliyoanza lazima ingetoka na ushindi wa kipekee. Jamii ikanipenda na kunienzi. Ikanisifu kwa utenda kazi wangu

mzuri. Wakanibandika jina la utani 'Sheha' kwa maana ya kiongozi. Kata ya Hesabika ikawa katika mstari wa kwanza kwani ilitoa mwanasheria mahiri. Hesabika ikaweza kuhesabika na kujulikana.

Hata hivyo, bali na sifa nilizopokea ndani na nje ya kata yetu ya Hesabika, kuna jambo moja lililokuwa kero kubwa sana katika maisha yangu. Nilikuwa nimezaliwa katika eneo ambalo wakazi wake waliamini sana tamaduni na itikadi kwa mapana na marefu. Hakuna aliyeamini kuwa elimu ingesaidia yeyote bila kutia kidole kingine ili kuongeza ufanisi kwa njia nyingine. Basi swali kuu likawa, mbona wazazi wangu wakajitolea kunisomesha ilhali hawakuamini mafanikio kutokana na elimu? Ni kweli, ukweli usiofichika kama mchana kwamba walikuwa tayari wameona watu wengi sana waliosoma na kupata kazi za kifahari kutokana na masomo yao. Hata hivyo, walibaki kwenye fikra potovu za upigaji ramli. Kama kawaida yao, kila walipotaka yeyote kupata kitu chochote, lazima wangeenda kwa mganga mashuhuri ili kushauriwa.

Dini ya kwetu ikawa ni uganga tu. Wala sio uganga unaofanyika kama taaluma ila kwenye sihiri. Mila na desturi ikawa upigaji ramli, uchawi na ushirikina. Eneo letu likapata sifa tele kwa kutoa mahiri wa uganga na uchawi. Inasemekana kuwa waganga walioweza kutibu magonjwa ya kila aina walitoka katika kata ya Hesabika mji wa Weusisi. Weusisi ni jina ambalo lilibeba maana mbili. Kwanza, lilikuwa na maana ya kuwa walio weusi ni sisi wala sio wengine. Huu ni weusi uliotokana na rangi ya ngozi ya watu walioishi humo. Pili, lilikuwa na maana ya weusi wa nafsi. Ulozi ulikuwa umetawala kwenye fikra, mawazo na mioyo yao. Matambiko nayo yalikuwa kama kawaida na hakuna mtu yeyote angekuwa kuheshimika katika jamii pasi na kupitia kwenye mila, asili, jadi na imani yao kama vile ukeketaji. Kung'olewa jino moja au meno mawili kama ishara ya kuhitimu utu uzima, ndoa za mapema na lazima na mambo mengine mengi yaliyovunja nyoyo. Weusi wa rangi ya ngozi na ule wa nafsi

ukatiana nguvu na kuhimiza juhudi za kutii na kuiga mila na desturi. Mila ikakua na kukomaa kila uchao.

Bali na weusi huo wote wa nafsi, kulikuwa na mwanga wa matunda yake. Mgala muue na haki yake umpe. Mwanga huu ulitokana na misingi thabiti iliyotawalia malezi ya watoto katika jamii. Tofauti na kata zingine, watoto waliolelewa katika eneo letu walikuwa wenye tabia na mienendo mizuri sana. Hesabika ilikuwa marufuku kwa uhusiano wa kimapenzi kati ya marika au watu ambao hawajaoana rasmi. Aidha, ilikuwa mwiko kwa mtu aliyeoa kufanya uzinzi. Heshima ilikuwepo baina ya watu wa umri tofauti tofauti. Mume aliweza kumheshimu mkewe, mke akamtii mumewe, watoto wakawatii wazazi na waliowapiku kwa umri. Uelewano na umoja ukapanda upendo, ukapalilia ushirikiano kisha ukavuna amani. Amani kwa jamii nzima. Mabinti kutoka Hesabika wakawa kivutio kwa wanaume kutoka vijiji vingine. Wakawa kama dhahabu. Thamani yao ikatambuliwa. Nikaivulia kofia mila yetu.

***

Nilikuwa nikitembea kwa mwendo wa asteaste kupitia kwenye vibanda vya soko vilivyokuwa mkabala na maduka ya mji ule. Mji huu ulijulikana kwa sifa za upigaji ramli. Watu wengi kutoka sehemu mbalimbali za nchi wangesafiri, hasa wakati wa ziara na mwishoni mwa juma kwa minajili ya kuangaliliwa shida zao. Hivyo basi, kutoka Ijumaa hadi Jumapili, waliohusika katika biashara hiyo wangeweza kupata pesa si haba. Waganga na waelekezi kwa pamoja. Mikahawa ya mji huo ikaweza kuingiza kipato kikubwa sana. Kuna wale waliokuwa wapishi katika mikahawa na mahoteli ya mji huo. Wapo waliowaelekeza wageni ambao pengine hawakujua makazi halisi ya waganga waliowataka.

Magari ya kila aina yangeonekana kuegeshwa kando kando mwa barabara za mji huo. Kwa wakati mwingine, nafasi za kuegesha

magari zingejaa, hivyo basi kulazimu mashamba yaliyokuwa karibu kutumika. Mji wa Weusisi ukajaa magari na kutapika mengine. Raha ikazidi. Kwa waliokuwa wanyonge wasioweza kustahimili raha hiyo, basi ikageuka karaha. Vijana wengi waliweza kujitosa katika mambo tofauti ili kujipa kipato chao. Wengi wakawa madereva, wengine watumbuizaji katika vilabu na sehemu za mvinyo na burudani. Waliokosa la kufanya wakawa makahaba! Hao ni wale waliotia maskio yao nta. Walioamua kwenda kinyume na desturi ya jamii. Wasaliti. Vijana wengi wakakosa masomo kwani walionea fahari kazi kama hii iliyopatikana kwa urahisi. Lao lilikuwa kufuata utamu wa asali ya kiganjani tu.

Kwa vile njia ya kuzunguka kwenye barabara kuu iliyofuatwa na magari ilikuwa ndefu, niliamua kupitia kwenye vichochoro vyenye njia ya mkato. Nikapiga hatua chache kutoka kwa barabara kuu na kuingia kwenye ujia uchwara ambao ulijaa giza la kaniki na takataka tele. Uvundo mkali uliokata pua kutoka kwa taka zile ulipiga pua yangu na kuniacha kuishiwa na pumzi. Nilijaribu kusitisha kupumua kwa kuziba pua yangu kwa mkono ili kuepuka mnuko huo lakini, nina uwezo usiozidi sekunde chache tu. Hivyo basi ilinibidi kuvumilia kwani mtaka cha mvunguni sharti ainame. Kulikuwa na mitaro iliyopitisha maji machafu yaliyotoka kwenye kina cha mji huo ambapo majumba ya kukodisha na mikahawa mikubwa mikubwa ilijengwa. Nilikuwa nimepiga hatua chache kwenye kiza kile kilichoogofya. Ghafla, nikaona kitu kilichopiga hatua kidogo kwenye mkono wangu wa kulia, kwa umbali wa mita takriban kumi hivi. Nilipokaza macho kwenye mwangaza huo hafifu, nikaweza kuona mnyama aliyekuwa kachukua umbo la paka mwenye rangi nyeupe. Alikuwa na mkia mrefu na macho yaliyokuwa makubwa. Macho yake makubwa kama ya bundi yaliwaka ajabu! Nikashtuka. Mwili wangu ukafa ganzi. Kilichonitia hofu zaidi ni kushuhudia jambo ambalo halikuwa la kawaida. Paka huyo aligeuka ghafla na kuchukua umbo la bweha kisha akatoa sauti kali sana ambayo iliniacha bila nguvu zozote.

Kijasho kikanitoka. Sikuyaamini macho wala masikio yangu. Nilidhani nilikuwa katika jinamizi kuu. Akapiga hatua kuelekea nilipokuwa nimeganda kama barafu huku mate yakimdondoka kwa hamu ya kunila. Kinywa chake kilikuwa wazi na aliponisogelea, akafungua niliweza kuona meno yake makubwa. Nikaogopa. Fikra zikanijia mara moja. Papo hapo nikapiga usiahi mkubwa kutokana na hofu. Sauti yangu iliweza kusikika kama mwangwi katika mji ukiokuwa umetawaliwa na ukimya wa asubuhi. Nikakamata mikanda ya mfuko niliokuwa nimebeba mgongoni na kutimua mbio. Nikanusurika.

***

Basi ikawa katika maisha yangu ya utotoni, bibi yangu alikuwa akinitolea hadithi kuhusiana na mizuka, mapepo na mazingaombwe. Hadithi zile ziliweza kunitia hofu sana hasa wakati wa usiku. Nakumbuka jioni moja baada ya mojawapo ya hadithi zile, nilipoenda chumbani mwangu sikupata hata lepe la usingizi. Nilikuwa nikijizoazoa tu kwenye kitanda changu kilichotengenezwa kwa miti na kufunikwa kwa ngozi ya ng'ombe kama tandiko. Tangu ujana wangu nilikuwa sijaona blanketi wala gondoro. Ngozi za wanyama kama vile ng'ombe au mbuzi ndizo zilizokuwa matandiko yetu. Nakumbuka nilivyokuwa nikitembea bila kiatu chochote miguuni. Visigino na nyayo zangu zikapasukapasuka kutokana na kutembea kwenye misitu iliyokuwa na miiba hatari na mawe yaliyokosa utu. Hadi nilipojiunga na shule ya upili ndipo nilipomeza tembe yangu ya pili katika kujua vitu vipya. Ninakumbuka hata wakati baba yangu alipopokea barua yangu ya kujiunga na shule ya upili ikiitaji blanketi na gondoro la shuleni linunuliwe, lilikuwa jambo gumu sana kwake kulifanya. Ilichukua ushawishi mkubwa kutoka kwa marehemu mama yangu ndiposa akakubali kufanya hivyo, ingawa kwa shingo upande tu.

Baadaye usingizi ulinivamia wakati wa jogoo la kwanza. Basi sikuwa na budi ila kulala fo fo fo kama mtoto mchanga. Saa chache baadaye niliamshwa na sauti ya kaka yangu ikiniita kutoka nje. Alikuwa mwingi wa papatiko na sauti iliyojaa woga kupita kiasi. Nilikuwa nimeloa jasho la kushangaza. Moyo nao ulikuwa umenikwenda kwa kasi kama upepo. Sikuamini. Kumbe nilikuwa nimepiga mayowe yaliyowaamsha kaka na dada yangu waliokuwa kwenye vyumba vyao vilivyokuwa mkabala na chumba changu. Waliniambia kuwa nilipiga mayowe kwa sauti ya mtu aliyeona maiti iliyofufuka, ndiposa kaka yangu akaja kujua ni nini hasa kilichojiri. Hofu kubwa ikanitawala wakati nilipofikiria hadithi ya bibi yangu usiku uliokuwa umepita. Hata hivyo, haikuwa mara ya kwanza kwangu kukumbwa na tukio kama hilo. Nikaahidi kuepukana na hadithi kama zile kutoka kwa nyanya yangu ingawa jambo lile halikuwa rahisi kama nilivyodhania. Ulikuwa wajibu wa wazee waliokuwa wamekula chumvi nyingi kutoa mawaidha kwa vijana wakati wa jioni baada ya kazi ya siku. Mawaidha hayo yangeweza kutolewa kwa njia ya hadithi. Hakuna kijana yeyote angesusia vikao vya hadithi, hivyo, ikanibidi kuandamana na uhalisia wa tamaduni za kwetu, kwani lisilo budi hubidi.

***

Niliposhtuka nilikuwa katika mtaro huku suruali yangu imeloa maji ya taka. Wakati huo sikuweza kuona kitu chochote tena mbele yangu ila giza kidogo tu. Nikajipa ujasiri na kuabiri gari nambari mguu niponye. Basi siku ile nikaamini kuwa kulikuwa na ukweli katika mambo yaliyokuwa yakizungumziwa katika jamii yetu. Nikawa mhasiriwa wa matukio ya hadithi nilizopuuza ukweli wake.

Karibu na lango la kuingia kwenye kampuni ya Ujadi Mills, niliwapata wazee watatu ambao walikuwa wafanyakazi wa pale wakizungumza kwa sauti ya chini. Mwangaza wa mataa ya umeme ya usalama ulikuwa umewatuliza na kuwapa uwezo ya kuongea

wakiangaliana ana kwa ana. Mmoja wao alikuwa binamu yangu ambaye alikuwa mkubwa kiasi cha haja. Alikuwa mtu wa miraba minne na ambaye aliwatishia watu kwa ukubwa wake. Hakuna mtu aliyewahi kumchezea kutoka utotoni mwake. Alikuwa mrefu kama mligoti na mwenye sauti nzito sana. Sauti iliyoogofya. Jina lake halisi lilikuwa Kinyale. Jina alilopewa na marehemu babu yetu. Jina hilo lilikuwa na maana ya "mizuka yangu." Basi ikawa amempa yeye kama urithi wa mizuka yake na jukumu la kuikimu baada yake kuiaga dunia. Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Wakati alipokuwa akiaga dunia alimwita na kumpa vifaa vyake vya uganga. Kinyale akawa hodari mkubwa katika mambo ya uganguzi wa kienyeji. Ukubwa wa mwili na sifa zake za uganga zilikuwa sababu tosha za kumfanya wa kuogopewa na kila mja.

Basi asubuhi ile alikuwa akizungumza na wafanyakazi wengine wawili. Kwa vile mimi sikuwa mfanyakazi wa kampuni ile, ilikuwa vigumu kwangu kujua ni nani hasa aliyekuwa akizungumziwa. Nilipofika karibu nikawaamkua kwa utaratibu sana. Uvundo uliotoka kwenye mavazi yangu kutokana na maji machafu ya mitaro nilikoingiza miguu uliwakatizia mazungumzo yao yaliyokuwa yamepamba moto kweli kweli. Nikawaelezea namna mambo yalivyotokea moja kwa moja. Kwenye mwangaza huo hafifu, niliweza kumtambua mmoja wa wafanyakazi wale ambaye alijulikana kama Mzee Kitumbo. Jina hilo lilikuwa limemfaa kwa namna alivyokuwa na tumbo kubwa. Alikuwa mtu wa urefu wa wastani. Alikuwa mweusi kama makaa na aliyekuwa na nywele nyeupe kichwani na kwenye ndevu zake ingawa hakuwa mzee kwa miaka. Pengine weupe huo wa nywele zake ulikuwa kutokana na jamii yao. Ilikuwa hali ya watu wa ukoo wao kuzeeka mapema. Ilikuwa hali halisi ya jamii yao na haingeweza kufichika. Inasemekana kuwa alipata nywele nyeupe alipokuwa wa miaka kumi na sita. Alikuwa akitwezewa na vijana wa rika lake hadi warembo walikuwa wakimkataa, huku wakidai kuwa alikuwa keshakonga. Hakuna mtu angeamini kuwa sio uzee bali hali

ya ukoo wao kwani kawaida mtu anapotoa mvi ni dhahiri shahiri kuwa kabugia chumvi nyingi. Ilimchukua muda mwingi kumshawishi hadi bibi aliyekuwa naye kuamini uvumi wa watu. Lakini hangefanyaje ilhali hivyo ndivyo mambo yalivyokuwa na kwa upande mwingine ndivyo watu walivyoamini? Vita vya ndani kwa ndani vikazuka kati ya uhalisia wa hali ya ukoo wao uliokuwa wa kuzeeka mapema na vile watu wasiokuwa wa jamii yao walivyoamini kuwa alikuwa kazeeka.

Yule mwanamume mwingine mfanyakazi nilikuwa simfahamu hata kidogo. Baada ya hadithi yangu kwa kifupi, binamu yangu aliniangalia kwa bezo akaniambia, “Hivi wewe Sheha umeishi Weusisi kwa miaka yote hiyo na hujawahi yajua mambo haya yote?” Akaniuliza kwa kejeli. “Hayo ni mambo ya kawaida na inabidi uyazoee kwani hutokea kila siku katika mji wetu na hata vijijini. Hata ukisoma hadi chuo kikuu bila kuelewa asili ya mambo ya jamii yetu, ni bure kabisa. Utaanza tena mwazo. Kumbuka mwanzo wa ngoma ni lele.” Akamalizia. Nilibaki kinywa wazi bila kusema lolote. Moyoni nikajua kuwa maneno ya binamu yangu yalibeba uzito mkubwa sana uliohitaji dharura. Nitajuaje haya mambo ya kwetu? Si nilikuwa nimesoma hadi chuo kikuu nikapata shahada ya uanasheria? Sikuwa na jibu kwa maswali hayo yote.

Niliporudi kwenye fahamu zangu nilisikia Kinyale akisema, “Sasa utalewa aje wakati uko kazini? Rafiki yangu Lewa lazima leo ajihadhari na mikosi wakati wa safari. Hata nimemshawishi kuwa punde tu basi litakapogurumishwa, aingie na aende moja kwa moja hadi kwenye kiti cha nyuma kabisa akatulie huko asionekana na ‘Uongozi’.” Akatua kidogo kuwapa wengine fursa ya kuchangia. “Kwani kalewa saa ngapi? Mihela ya ziara yetu tumepewa jioni tu?” Akaulizia Mzee Kitumbo kwa shauku kubwa. “Ndiyo. Yule bwana kapokea mihela na kutokomea hadi kwa Bi. Ntilie alikolala huko akilewa. Leo kaletwa hapa asubuhi na mapema na kaka yake mdogo

kusudi asije kosa kwenda safari hii, jambo linaloweza kumfanya akose kazi mara moja kwa kutotii amri za kazi." Akaendelea Kinyale. Yule mwanamume wa tatu naye akadakia kwa haraka, "Lakini Kinyale jua kuwa hiyo ndiyo hali yake halisi. Huyu bwana kaachiwa ulevi na babu yake wakati anaaga dunia miaka ishirini iliyopita. Hawezi kwenda kinyume na kanuni za babu yake. Amejaribu kuachana na ulevi lakini imekuwa kazi bure. Ni vigumu sana kwake. Yeye na pombe wamekuwa marafiki wa chanda na pete kama sio wa uta na upote." Akamalizia.

Hata kabla ya yule mwanamume kumalizia, niliweza kuona mtu akitoka kwenye lango kuu la kampuni huku akipepesuka kama meli katika mawimbi makali ya bahari. Nilijua fika kuwa alikuwa Lewa. Alikuwa amelewa chakari na hata alishindwa kutembea vizuri. Mwendo wake ukawa wa kupepesuka. Walipomwona wakakatiza mazungumzo yao kwa ghafla na kumwangalia kwa pamoja kama watu walioona ibilisi mwenye pembe. Lewa naye akatembea hadi tulipokuwa tumesimama na kuketi chini kwenye kijiwe kilichokuwa kimewekwa kando ya lango kuu. Akaanza kutoa maneno ya kilevi ambayo yalikuwa na ukweli uliokuwa umefichika kwa ndani. "Babu yangu alikuwa mwafrika halisi. Aliweza kutafuta mali nyingi sana kwa jasho lake mwenyewe. Hakuwatendea watu mabaya wala kumdhulumu binadamu yeyote. Alikuwa akila vyakula halisi vya kiafrika visivyo na kemikali zozote na ndio maana hakuwahi kulalamikia afya yake. Aliweza kuishi miaka mia moja na arobaini na tano na siku kumi na mbil…mbili. Sisi watu weusi hatuwezi kuwa kama wazuuu..ngu," akasita kidogo akameza mate kwa uchungu. "tumekula vyakula vya wazungu vilivyojaa kemikali mbaya ya kutumaliza pooole…pooole. Mara leo naumwa na mgongo, mara meno, tumbo au mwili mzima. Kesho walalamikia kuumwa na kifua, vivyi hivyo hadi madaktari wanakupima na kusema ukona saratani, kisukari au kifua kikuu. Ningerudishwa kwenye ujana wangu leo

singejiathiri kwa pombe kama nilivyo leo au vyakula vyenye bei kali na vilivyojaa mauti." Lewa alimalizia usemi wake.

Mzee Kitumbo alimwangalia kwa jicho la upekuzi huku kashangaa alikoyatoa maneno hayo mazito. Akamsaili, "Uliyoyasema Lewa ni kweli kabisa. Sio mshangao kwetu kuwa tunaishi miaka sitini kwa wale waliojaliwa na maulana. Hii ni kutokana na mambo mapya ambayo tumeiga kutoka bara za kigeni kama vile Ulaya na Amerika. Uhalisi wetu umetoweka na kuchukua mkondo mwingine wa maisha. Zamani watu walikuwa wakitumia moto wa kuni kupikia na kufanya mambo usiku. Leo umeme umekuja na umetuharibu macho yetu. Vijana wachanga wanavaa miwani kisa na maana, hawaoni vizuri." Mzee Kitumbo akatua alipoona kuwa yule mwanamume wa tatu alikuwa anataka kusema yaliyokuwa akilini mwake.

"Naam, muyasemayo ni kweli, lakini tusisahau hata wema wowote wa mila ya kigeni na teknolojia waliyoleta. Zamani kwa kawaida namna ya mawasiliano ilikuwa gumu sana. Watu walitumia ngoma na wakimbiaji kupitisha ujumbe fulani. Binadamu yeyote alipopotelea katika msitu mkubwa angewasha moto ambao moshi wake ungeweza kufuatwa na waliokuwa mbali kisha kumwokoa. Waliotumwa wangetumia muda mrefu sana kufika walikokuwa wakienda. Kwa sasa tuna simu za mkononi zinazotumika kuwapigia watu na kutuma ujumbe mfupi popote wakati wowote. Mawasiliano ni papo kwa hapo kwa kutumia simu. Barua pepe kwa upande wa ofisi inatumika kwa urasmi mkubwa. Imerahisisha mawasiliano kwa kiwango kikubwa sana. Tarakilishi nazo zimesaidia sana kufanya mambo makubwa na yaliyo zaidi ya uwezo wa binadamu kwa utaratibu mkubwa. Makosa ya binadamu ambayo yana madhara makubwa kwenye viwanda vyenye kiwango kikubwa cha usahihi yameondolewa. Utandawazi nao umeifanya dunia kuwa kitongoji kidogo sana. Mbona tunalalamikia kutoweka kwa mambo ya kale ilhali hatuoni manufaa ya kuwa na teknolojia ya kisasa?" Mwanamume yule alitua usemi

wake. Kila mmoja akanyamaza. Wakati huo, wafanyakazi wengine walikuwa washafika akiwemo dereva wa basi. Hivyo hatukuwa na budi kukatiza mazungumzo yale yaliyokuwa tayari yamechukua mkondo mpya.

# SURA YA PILI

Kampuni ya Ujadi Mills ilianzishwa mnamo mwaka wa 1964, punde tu nchi ya Kenya ilipojinyakulia mamlaka kutoka kwa wakoloni. Maisha mikononi mwa wakoloni yalisababisha uduni usiomithilika kutokana na ukandamizaji. Dhuluma anuwai zikamwangukia mwananchi. Hali ya kila mmoja ilikuwa nyakanyaka. Sio hali tena. Wakenya walikuwa mahadimu wa wakoloni waliojinyakulia mamlaka kutoka kwa wanyonge. Minyororo ya mkoloni ikawabana wengi kwenye mikono na miguu yao. Nguvu za minyororo hiyo zikazidi kuwa nyingi kila siku. Waliokosa pingu mikononi au kwenye miguu walikuwa nazo kwenye fikra zao. Ole wao! Akili zao zikapinduliwa na kulainishwa kwa dhamira ya kuiga mashauri ya vibaraka wa mabeberu. Wakenya wakawa kama wafungwa kwenye nchi yao wenyewe. Wakalishwa ngwamba. Vyungu vilivyotumika awali kupikia nyama na minofu mingine, vikasikika vikitoa mitokoso wakati huu vikupikia mitolilo. Basi mgeni akageuka na kuwa mwenyeji. Mateso ya kila aina yakaanza. Dhuluma zikaongezeka wala hakuwepo yeyote wakuwatetea. Kinywa cha kila mmoja kikabanwa. Kwa miaka mingi, wazungu wakapora Wakenya mali na kuharibu raslimali na miundombinu.

Kweli, mchovya asali hachovi mara moja. Waliodhaniwa kuwa wangeondoka baada ya siku chache, waliweza kuishi kwa kipindi cha siku moja, majuma, miezi kisha miaka ikapita. Miaka nayo ikaunga miongo. Wakenya wengi wakauawa kinyama bila rehema. Hapo ndipo ghadhabu iliwapanda wengi na kuunda vikundi vya kupigania haki, usawa na uhuru wao. Mababu zetu wakabuni njia za pekee za kukamilisha malengo ya kumfurusha mkoloni. Kwa dhiki na taabu hatimaye waliweza kushinda vita hivyo ambavyo vilihitaji ukakamavu na hekima. Kwa sasa tunasheherekea matunda ya waliosimama kidete na kusema kwa pamoja kuwa, "punda amechoka!"

Naam, kampuni ya Ujadi Mills ilikuwa imejengwa kwa sababu moja maalum – kuhifadhi na kudumisha utamaduni wa Kiafrika. Bwana Kolea ndiye aliyekuwa mwasisi na Mkurugenzi Mkuu wa Ujadi Mills. Ingawa alikuwa mwingi wa miaka, kwa mtazamo ungemfananisha na kijana wa makamo. Inasemekana kuwa, alikuwa tayari kafikisha miaka themanini na moja na miezi sita ila alionekana mwenye hali njema kiafya na kimwili. Marika wake wengi walitembea kwa mikongojo huku wakilalama kuumwa na kila sehemu ya mwili kama ilivyo kawaida ya wale waliofikia umri huo. Wengine walikuwa wakubebwa kutoka sebuleni kwenda uani kama walifanikiwa kuishi maisha ya Bwana Kolea. Mgongo hulalamika zaidi, miguu hununa na macho huchoka kufunguka. Kinyume na hayo, Bwana Kolea aliyekuwa wa kimo cha wastani alikuwa mwingi wa afya na uhai huku akiendesha mambo yake kama kawaida. Mbona Bwana Kolea alikuwa mwenye sura ya kijana wa makamo wakati alikuwa ashakonga? Naam, Kulikuwa na mambo kadhaa yaliyomfanya kuwa na sura ya ujana na ngozi laini. Bwana Kolea aliamini umuhimu wa vyakula halisi vya Kiafrika. Hangeweza kula chakula chochote kile, isipokuwa chakula cha asili. Lazima angedhibitisha na kuhakiki mahali kilipotoka, ndiposa aweze kukitia kinywani mwake. Mwili wake ulikuwa wenye afya njema kila wakati. Hadi kwenye uzee wake alikuwa hajawahi ingia kwenye mlango wa hospitali. Kama homa ingefanikiwa kumpata, alikuwa na dawa yake. Maumivu ya mwili pia yalikuwa na tiba yake.

Bwana Kolea alikuwa akiishi kwenye kasri. Alikuwa mwenye mali si haba. Aliweza kusanya mali nyingi sana kwa miaka yake aliyoishi. Bidii yake ilikuwa ya kuigwa na kila mmoja aliyemfahamu. Naye alikuwa kajaliwa familia iliyomuunga mkono kwa kila jambo. Mke wake, mabinti wake wawili na kijana mmoja wa kiume, waliifanya familia yake kuwa kamilifu. Zaidi, alikuwa na vijakazi waliohudumu kwenye kasri lake. Maelfu ya mifugo ilikuwa na walinzi wake. Idadi yao ikiwa kwenye viganja vyake. Ingawa bwanyenye huyu hakuweza

kusoma darasani, akili yake ilikuwa nyepesi kwa kushika mambo. Hakuwa mbumbumbu! Hakuna yeyote angeweza kumlaghai wala kumwibia na hata angefaulu kumnyenga, hangemkwapua. Bibi yake Natasha naye alikuwa mrembo. Hurulaini ajabu. Alikuwa na macho ya njiwa, kope za malkia, vidole vya malaika, nywele ndefu ajabu na sauti nyororo iliyovutia. Alikuwa kajaliwa umbo la nambari nane. Mwenye mwendo wa tausi. Aidha, alikuwa kajaliwa moyo wa ukarimu na upendo. Mapenzi ya dhati kwa Bwana yake, watoto wake na wafanyakazi wake kwa pamoja. Kweli, mkwara hautaji mafuta! Bwana Kolea alikuwa kachagua kweli! Akaendelea kupata tiba ya moyo na roho kutoka kwenye tembe aliyomeza yeye mwenyewe.

Kasri la Bwana Kolea lilikuwa na mpangilio wa kipekee. Kulikuwa na ratiba maalum ya kufanya mambo pindi kila mtu alipoamka, hadi wakati aliporejea kwenye malazi yake. Kulikuwa na wakati wa kufungulia mifugo na wakati wa kuwarejesha nyumbani. Kulikuwa na wakati wa kwenda sokoni na wakati wa kusalia nyumbani. Wakati wa kuswali na wakati wa kula kwa pamoja. Kuingia na kutoka kwenye kasri kulifuatia namna ratiba ilivyosema. Hakuna aliyeshurutishwa kufanya jambo lolote. Kila aliyekuwemo mle ndani alifahamu wajibu wake na wakati wake. Jambo lolote la mjio kama sio la dharura basi lazima lingengoja hadi wakati mwingine. Walinzi wawili walikuwa wamewekwa kwenye lango kuu. Wakakabidhiwa jukumu la kuwalinda waliokuwa ndani ya kasri hili kubwa - nasaba ya Bwana Kolea. Pindi tu ulipoingia kwenye lango hili, ungeweza kupatana uso kwa uso na uga mkubwa uliokuwa mbele ya kasri hili. Aila hii ilitumia uga huo kwa njia tofauti. Kulikuwa na sehemu ya kufanyia mazoezi. Vifaa vya kuinua, kusukuma, kuvuta, kuendesha na kubebea vilikuwemo. Sehemu za kuchezea mpira wa kandanda, mpira wa vikapu na mpira wa mikono zilikuwa zimetengwa na kuwekwa vifaa vyake. Kando ya uga huo kulikuwa na bwawa la kuogelea. Bwawa hili lilikuwa limezingirwa na bustani ya miti ya kivuli na maua yaliyopendeza machoni. Kutoka rangi ya chanikiwiti

iliyokolea kwenye majani ya miti ya bustani, hadi kwenye rangi ya kijivu hafifu iliyoonekana kwenye majani yaliyozagaa chini na kuipa mandhari yale utulivu wa kipekee. Rihi ya kuvutia ilishamira kutoka kwa maua yaliyokuwa na rangi za kupendeza machoni na kuwapa vipepeo sababu nyingine ya kurudi pale. Binadamu aliyefika hapo kwa mara ya kwanza angepata sababu ya kukawia, kwani makaribisho ya rihi ile yalikuwa ya kiwango kingine. Kila aliyetaka kukata upweke wa kukaa kwa nyumba aliweza kutoka na kupunga unyunyu kwenye bustani hiyo.

Ilikuwa siku ya Jumapili ambapo mabinti zake wawili, Anisa na Anasa walikuwa wametoka pamoja na Natasha kwenda sokoni kama ilivyokuwa ada yao. Kwa kawaida, yeye na mwanawe wa kiume Hari wangebakia nyumbani wakicheza mpira wa vikapu. Waliupenda sana mchezo huo. Alasiri hiyo, jua lilikuwa angavu, joto la kadri, hewa murua na upepo mwanana. Jua hili lilitoa miale yake kwa madaha na utaratibu – jinsi tu mwenyezi mungu alivyolikadiria. Ukimya wa kipekee ulikuwa umezunguka kasri la Bwana Kolea. Wafanyakazi wake walikuwa wamefukuzwa na ratiba ya jioni hiyo. Hari alikuwa kwenye chumba chake akicheza gitaa yake. Kwa jumla, kasri hili lilikuwa na vyumba zaidi ya kumi. Alikuwa stadi wa kucheza gitaa. Bwana Kolea naye alikuwa juu kabisa kwenye roshani ya jumba hili huku kashika gilasi ya maji ya matunda. Alikuwa kavalia chepeo ya rangi nyeupe, fulana nyepesi isiyo na mikono ya rangi nyeupe, kaptura nyeusi iliyomfikia mwenye magoti kisha kavalia kandambili miguuni. Alionekana mwenye mawazo tele kwa namna alivyokuwa akiuuma ulimi wake huku akifungua kinywa chake mara kwa mara na kufinyafinya macho yake kwa mkono uliokosa kazi. Macho yake yangetua mahali pamoja kama mtu anayetazama kitu kwa umakini. Ghafla, ile gilasi ikahisi kwamba mapenzi ya Bwana Kolea yalikuwa hafifu na kutaka kuondoka. Ikateleza kutoka kwenye mkono wake kuponyoka. Hapo ndipo Bwana Kolea alipofinyilia mkono wake na

kuikamata kwa nguvu isianguke na kumwaga vilivyokuwepo ndani yake. Akayarudisha mawazo yake pamoja.

Baada ya dakika chache, aliweza kumwona Hari akielekea kwenye uwanja wa mpira wa vikapu huku akiwa mwenye furaha gaya. Aliweza kujua haya kwa namna alivyokuwa akirukaruka huku akipiga mlunzi. Papo hapo akajua kuwa wakati wa kucheza na mwanawe ulikuwa umewadia. Akaanza kupiga mafunda makubwa ya maji yale matamu huku akitembea tembea bila kusema lolote. Kwenye ile hali, akaanza kujiongelesha kwa sauti akisema, "Hari kweli amekua. Mwanambee wangu keshabalehe. Amekuwa mjuzi wa mambo mengi katika kasri langu. Dada zake wawili wanamtazamia kwa kila jambo. Atakapofikisha umri ufaao nitaweza kumgawia sehemu maalum ya mali yangu. Nitamwonyesha kisha nitamwoza bibi yake. Naona maisha yake yatafana kweli." Uzungumzi ule ulikatizwa ghafla na sauti ya Hari. "Baba-aa!" Hari alimwita baba yake aliyekuwa kazama kwenye luja la mazungumzo ya nafsi. "Naam, mwanangu. Naja," akaitikia Bwana Kolea kwa mshtuko. "leo lazima nikushinde kwa vyovyote vile. Naamini umejipanga." Hari akamwambia baba yake aliyekuwa tayari kaanza kushuka kuelekea kwenye uga. Hari alikuwa wa miaka kumi na tano. Alikuwa ndio kwanza kamaliza masomo yake ya shule ya upili alikofuzu na kuitwa kujiunga na chuo kikuu cha Weusisi – kilichokuwa maarufu kwa kutoa madaktari wenye ustadi kwenye kazi yao. Bwana Kolea akaingia kwenye chumba chake akabadilisha mavazi kisha akajiunga na mwanawe kwenye mchezo huo.

***

Itakuwaje chaudere wa Bwana Kolea ndio kwanza anabalehe? Mzee wa miaka mingi kama hii anapaswa kuwa na familia iliyokomaa. Kwani alikuwa wapi? Haya ni baadhi ya maswali najua unajiuliza kwa sasa. Najiuliza pia, ila tofauti yangu na wewe ni kwamba, mimi nina majibu, ila wewe umekosa. Kama una hamu ya kutaka kujua,

basi huna budi kusogea. Tandika mkeka, keti na utulie kwa makini nikupashe yaliyojiri.

Mali ya Bwana Kolea ilipatikana kwa jasho na bidii za mchwa. Alizaliwa kutoka kwa familia ya wachochole. Watu wasio na chao. Alikuwa chaudere kwenye familia ya watoto kumi. Wote walitoka kwenye tumbo moja. Marehemu baba yake kama hakujaliwa bidii katika kutafuta mali, alikuwa na bidii katika kutafuta watoto. Mwaka baada ya mwingine kulikuwa na kitoto kwenye aila yake. Inasemekana mkewe alikuwa kachoka kubeba na kulea watoto. Alikuwa hoi. Hajiwezi. Lakini hakuwa na budi ila kutii mumewe kama ilivyokuwa desturi ya jamii yao.

Kwenye familia ile, chakula kilikuwa adimu kupatikana. Malazi yalikuwa ya kubahatisha na nyumba yao ilikuwa kama mahame. Ingeweza kusalimu amri wakati wowote. Ulitima ulikuwa umewazunguka kila upande. Bwana Kolea akatwikwa jukumu la kutafutia wadogo wake chakula wakati alipofikisha umri wa kuweza kufanya kazi za mikono. Kidogo alichobahatika kupata, akakipeleka nyumbani. Wakala na kulala njaa bila kusaza chochote. Kila siku ikawa siku ya kuloa jasho.

Kutokana na tabia za baba yake aliyekuwa mvivu na mkandamizaji vilevile, alipanda chuki kwani majukumu yake yalitwikwa mabegani mwake. Hakupata fursa ya kusoma kama watoto wengine. Akawa wa kudhihakiwa na kudharauliwa na marika wenzake. Hapo ndipo alipoapa kuwa lazima atafute mali yake mwenyewe. Safari ikaanza. Miaka mingi ilipita bila yeye kufanikiwa na zaidi majukumu ya kulea wadogo wake yalikuwa mazito kama nanga. Miaka ikapita bila yeye kujua, na kama alijua, hangeweza kufanya lolote. Akawa wa miaka kumi, ishirini, thelathini, arobaini hadi hamsini bila kuwa na ndoa yake. Mali yake aliweza kuisanya kwenye miaka yake ya kuanzia arobaini.

Msichana aliyekuwa aozwe akaozwa mwingine kwani Bwana Kolea alionekana asiye na haraka ya ndoa. Watu wakasema waliyosema. Akatia masikio yake nta kwani malengo yake yalikuwa makubwa. Hakuna aliyemwelewa. Baadaye ndipo alipokutana na Natasha na baada ya muda mfupi, wakapanga mipango ya harusi kisha wakaoana. Bwana Kolea wa miaka hamsini, Natasha wa miaka ishirini.

Bwana Kolea alijulikana kwa kutumia mitishamba katika kutibu magonjwa ya kila aina. Ujuzi wake mkubwa wa kutengeneza dawa kutokana na mizizi, majani, maganda na matunda ya miti tofauti ukawa chanzo cha umaarufu wake. Isitoshe, alikuwa akiwahimiza watu kutoasi utamaduni, kwani yeye alikuwa mfano kamili wa kuigwa na kila mmoja. Watu wengi waliweza kuepuka vyakula duni vya kigeni na kuanza kutumia vyakula vilivyotengenezewa katika kampuni yake. Kampuni hii ilikuwa imejengwa kwa lengo la kuendeleza utamaduni na kuimarisha afya bora ya wananchi. Iliweza kutengeneza dawa mbalimbali zilizouzwa kwa bei nafuu katika sehemu tofauti za nchi. Dawa hizi zilionyesha kuwa na uwezo mkubwa katika kutibu maradhi tofauti. Hakuna aliyelalamikia kukosa kupona baada ya kuzitumia kulingana na maagizo yaliyotolewa. Kila mja akameza tembe yake. Waliokosa basi wakapatana na madhila yao.

Bali na utengenezaji wa dawa na vyakula mbalimbali, kampuni hii ilikuwa imetenga sehemu kubwa ya ardhi kwa minajili ya kuweka wanyama pori. Wanyama wa kila aina waliishi humo. Sungura, tembo, kifaru, ndovu, simba, nyani, bakaya, pundamilia, nyati, nyoka na wengine wengi. Ndege pia walikuwa hawakosekani humo. Kulikuwa na tausi, nyuni, nderi, tai, kanga, mbuni, heroe na wengine wengi. Kampuni hii ikashirikiana na serikali iliyokuwa imebuniwa wakati huo, katika kuhifadhi raslimali. Hivyo basi wanyama na ndege hawa wakawa kivutio kikubwa cha watalii kutoka mataifa mengine. Mambo yakageuka! Aliyekuwa windo akawa mwindaji. Hata ingawa

bado barabara zilikuwa mbovu, idadi kubwa ya watalii ingeweza kushuhudiwa kila uchao. Serikali nayo ikazembea katika utengenezaji wa barabara muhimu, hivyo basi kusababisha idadi ndogo ya watalii walioweza kufika katika eneo hilo. Haidhuri, mja hupata ajaliwalo wala sio atakalo. Ujadi Mills ikapiga hatua kwa kuwekeza kipato chake katika kukarabati barabara hizo na kulainisha usafiri kutoka kwenye mji mkuu wa Weusisi.

Kulikuwa na wafanyakazi wengi sana walioajiriwa na Ujadi Mills. Kulikuwa na wale waliohusika na kuhakikisha kuwa vitu vyote vilivyohitajika vilikuwepo. Walikuwepo wafanyakazi waliohusika katika kuleta sehemu tofauti za miti kutoka kwenye msitu uliokuwa milki ya kampuni. Kuna wale waliokuwa wakifanya kazi ndani ya majengo ya kampuni kutengeneza dawa kutokana na sehemu za miti zilizoletwa. Kuwepo kwa kampuni hii kuliweza kuwapa watu wengi ajira na wakapata mahali pa kujitafutia chakula cha kila siku. Wakati kasri la Bwana Kolea lilikuwa viungani vya mji wa Weusisi, majengo ya Ujadi Mills yalikuwa maili kadhaa kutoka kwa mji huo.

Miongoni mwa wafanyakazi wale alikuwepo Bahati. Alikuwa akifanya kazi kama afisa msimamizi wa Ujadi Mills. Niliweza kumjua Bahati wakati baba yangu alipokuwa akitafuta ajira kwenye kampuni hiyo. Alipoenda akamwelezea haja yake, akamsikiza kwa makini lakini hakumpa jawabu tosha. Alimwambia kuwa wakati huo walikuwa na wafanyakazi wakutosha. Kama angetaka, angejiunga na wengine ila kwa kazi isiyokuwa na malipo. Baba yangu akakataa kata kata. Akaona kuwa kufanya kazi bila malipo ingekuwa utumwa. Akarudi nyumbani. Aliponielezea yaliyokuwa yamejiri baina yake na Bahati, nikaamua kujipeleka mwenyewe kwenye ofisi yake. Nilipofika kwenye lango la kampuni, nikawapata walinzi wawili.

“Shikamoo?” Nikawaamkua wale walinzi wawili. Wakasita kunijibu kwa sekunde kadhaa kisha mmoja akasema, “Marahaba, tukusaidie vipi kijana?” Akaniuliza. Nikaengaenga kidogo. Wakatazamana kwa

mshangao. Yule mlinzi wa pili akaniangalia kwa jicho la upekuzi na kuniuliza, “Umewaacha chokora wengine wapi ukaja huku? Tafadhali rudi ulikotoka kabla ya hamaki yangu kupanda.” Akasema huku akitoka alipokuwa amesimama na kunisogelea. Ujaka mkali na mbaya ukatoka kwenye mdomo wake na kupiga pua yangu kama kibunga kinachotokea kwenye jangwa la Kalahari huko kusini mwa Afrika. Meno yake yalikuwa na ukoga. Alikuwa beberu. Nilikosa la kufanya. Moyo wangu ulipiga kwa upesi. Nikaduwaa. Sauti yake ikanijia tena kwenye akili. “Umewaacha chokora wengine wapi ukaja huku?” Maneno yale yalinikata moyoni mwangu kama kisu cha mchinjaji. Nilikuwa na nywele timtimu. Kaptula yangu ilikuwa imebandikwa viraka viwili, kimoja kwenye makalio ya kushoto na kingine kulia. Viraka vile vikawa cheuzi kama macho ya binadamu ambaye si chongo. Vilikuwa vikubwa kiasi cha kugeuza rangi ya kaptula yangu kuchukua rangi yake. Macho yangu makubwa yalikuwa mekundu kutokana na vumbi. Nywele zangu zikabadilika na kuwa nyekundu vilevile. Midomo yangu nayo ilikuwa imekaukiana na kupasuka pasuka kwa uchovu na njaa. Miguuni nilikuwa bila viatu. Kweli, ulinganishi wa yule mlinzi ulikuwa yakini. Nilikuwa kama chokora. Hata hivyo, hakustahili kunidunisha wala kunidhalilisha vile. Nilipofungua kinywa changu kumjibu, alikuwa tayari ameshanifikia kwa fimbo yake nusura anipige. Hapo ndipo nilipopiga ukwenje uliosimamisha kila unywele mwilini mwangu. Akazubaa. Mlinzi wa kwanza akamkaripia kwa maneno, “Mwache ajieleze tafadhali. Haina haja kumpiga kijana asiyekuwa na makosa.” Aliposikia sauti ya mlinzi wa kwanza akatii. Akapiga mnyuso huku akirudi kwenye lango kuu.

Unyende wangu uliweza kusikika na wengi waliokuwa ndani na nje ya kampuni hiyo. Wengi wakaja kujua nini hasa kilichokuwa kimejiri. Bahati akasikia kivangaito na kuwa na shauku kuu ya kujua chanzo chake. Akaita mlinzi wa kwanza mara moja. Alipoelezewa matukio ya awali, akaniita. Mlinzi wa kwanza akaniamuru kuandamana naye

kwenye ofisi ya Bahati. Aliponifikisha ofisini mwake, Bahati akamwamuru kurudi kwenye kazi yake. Akaanza kunioji kwa upole. Akaomba msamaha kwa niaba ya mlinzi wake na kunihakikishia kuwa jambo kama lile halingetendeka tena. Kwenye huruma hiyo, nikapata fursa ya kuuweka moyo wazi na kumwelezea yaliyonileta humo. Nikamjuza kuhusiana na baba yangu aliyekuwa ofisini mwake siku mbili zilizokuwa zimepita pamoja na dhamira yangu ya kumtafutia kazi. Akamfahamu kwa urahisi. Nikamwelezea kwa kina, shida za familia yetu na namna tulivyokosa hadi chakula. Akanihurumia sana. Akaamuru baba yangu kuitwa mara moja. Naye akaja bila kukawia. Bahati hakuwa na mengi ya kusema. Alimpa barua iliyomweleza kuwa alipaswa kuanza kazi yake siku iliyofuatia. Akafurahi sana kutokana na hatua niliyochukua huku akinipongeza kwa ushupavu wangu. Hiyo ndiyo siku familia yetu iliangaza. Tukasalimiana na mafanikio. Pia hiyo ndio siku ya mwisho yule mlinzi wa pili kuonekana kwenye lango la Kampuni ya Ujadi Mills. Alipigwa kalamu mara moja.

***

Basi, baada ya miaka kadhaa baba yangu akiwa mfanyakazi kwenye kampuni hiyo, aliweza kukutana na Bahati kwenye hafla ya kufunga mwaka ya familia yetu. Wakati tunabarizi pale sebuleni, Bahati akanisimulia hadithi yake ya kabla ya kupata ajira kwenye kampuni ya Ujadi Mills. Yeye alikuwa ametoka kwenye familia hohehahe. Jamii yake ilikuwa ikiishi mbali na mji wa Weusisi. Wakati familia yao ilipogura kutoka walipokuwa wakiishi, alikuwa kijana aliyebalehe. Akalazimika kujiunga na Ngwata. Ngwata lilikuwa kundi la kulinda familia katika kijiji. Ilijumuisha vijana kumi shupavu. Ilikuwa ikitawala na kulinda nyumba kumi na tano. Inasemekana kuwa ngwata ilikuwa na usemi mkubwa sana katika jamii. Kuasi ngwata kulikuwa sawa na kuvunja kanuni ya serikali. Ngwata ilikuwa na watu waliokuwa na uhusiano wa karibu sana, hivyo, ilikuwa rahisi

kutatua shida za wahusika. Vijana hawa walijulikana kama 'askari'. Askari hawa walikuwa na majukumu ya kuchukua hatua pindi tu mtu yeyote alipokosana kufanya sawa na kanuni za ngwata. Zaidi ya hayo, lilikuwa jukumu la Ngwata kulinda wananchi huku kiwango kikubwa cha vijana wa makamo kikihusishwa kwa minajili ya kushika doria wakati wa usiku, uvamizi au hatari yoyote ilipotokea.

Bahati alikuwa kati ya 'askari' wale. Naye alikuwa mweusi kama makaa, mwenye kimo cha takriban futikamba tano unusu na aliyekuwa kajaliwa miguu mirefu kama unju. Sura yake ilikuwa ya kutisha. Alikuwa kajaliwa macho makubwa, ndevu na masharubu yaliyofunika kiasi cha nusu ya uso wake. Watu wakamwogopa na kutii sauti yake. Vijana waliokuwa vichwangumu wakalainika na kufuata utaratibu wa jamii. Zaidi, alikuwa na misuli iliyojaa kweli kweli, mwenye nguvu na mkakamavu. Kamati la Ngwata lilipoketi kwenye kikao likamchagua. Akajiunga na kundi la askari wa kudumisha usalama katika kijiji chao.

Siku moja, Bahati na kundi lake walipewa jukumu la kumsaka mwizi. Kwa kipindi cha miezi mitatu, wakazi wa kijiji cha Arali walilalamika sana kuhusu kupotea kwa mali yao kama vile mifugo na vifaa vya nyumbani kwenye njia za kutatanisha. Mifugo wao kama vile mbuzi, kondoo, kuku na bata waliweza kupotea pasipo kujulikana wapi walikoenda. Vifaa vingi vikiwemo vyombo vya kupikia kama vile sufuria, sahani, vijiko pia viliweza kupotea. Hakuna aliyeweza kufahamu nani hasa aliyekuwa akiwaibia. Muda ulivyozidi kusonga ndivyo malalamiko yalivyoongezeka. Wakazi wakaghadhabika. Kilio chao baadaye kikafikia Ngwata ambayo iliamuru mwizi yule achunguzwe mara moja. Bahati akaangukiwa na jukumu hilo. Akapewa uongozi wa kikundi cha askari wa kumtafuta mwizi yule. Viongozi wakamwambia kuwa alihitajika kuleta yule mwizi mara moja. Bahati akalipokea jukumu hilo kwa mikono miwili. Kazi ya kutafuta mwizi ikang'oa nanga. Bahati alijulikana kwa umakini wake

na ustaarabu wa kufanya mambo. Akaamuru kundi lake kujihami kwa ajili ya kusaka mwizi.

Hatua yao ya kwanza ilikuwa kubaini wakati mwizi yule alipokuwa akiiba. Mchana au usiku. Wakaingia katika kila nyumba kuwasihi watu wawasaidie. Wakaitenga siku ya kwanza na kumwambia kila mtu asalie nyumbani mchana kutwa. Hakuna mwizi aliyekuja siku hiyo. Siku ya pili vilevile. Hakuna kitu chochote kilichoibiwa. Wakajua pengine yule mwizi wakati wake ulikuwa usiku. Wakapanga namna ya kufanya. Waliamini fika kuwa mwizi yule alikuwa ametoka kijiji kingine kama ilivyokuwa kawaida ya wezi wengi waliopatikana. Usiku wa siku ya pili iliwabidi kuwa macho. Kundi lile lilizunguka Arali nzima na kujificha katika sehemu mbalimbali. Kuna sehemu za Arali ambazo zilikuwa marufuku kwa wakazi. Mchana na usiku. Zilikuwa zimetengwa kwa minajili ya kufanya maombi kwa mizimu na wenyeji walizifahamu. Wazee wa kijiji ndio walioruhusiwa kwenda huko ila siku maalum. Basi kiingilio cha Arali kikawa njia tatu peke yake maana sehemu nyingine ilikuwa msitu wa wanyama wakali sana ambao wangemshambulia binadamu yeyote ambaye angepitia pale wakati wa usiku. Katika sehemu hizo tatu kukawekwa askari wawili wawili. Kila askari alijihami kwa silaha kali za kitamaduni kama vile uta na upote uliojaa mishale yenye sumu. Zaidi, kisu cha mwindaji chenye makali kuwili kilikuwa karibu. Hata ingekuwa mwizi wa mbuzi na kuku alikuwa chui, simba au simba marara kutoka kwenye msitu uliokuwa karibu, nani alikuwa mwizi wa sufuria, vikombe na sahani?

Mnamo saa moja jioni, kila mtu alikuwa mwenye maficho yake. Wakati huo, giza kuu lilikuwa limefunika kila mahali kwani hakukuwa na mbalamwezi. Arali ilikuwa katika hali ya ukimya wa kaburi. Kila mtu alikuwa kwenye chumba chake. Wanyama wa pori wanaowinda wakati wa usiku walikuwa wakijitayarisha kwa mawindo yao. Bahati na kundi lake wakakawa sawa na wanyama wale.

Kila mtu akawa tayari kupambana na lolote ambalo lingetokea. Mnyama au binadamu? Wakangoja hadi ikafika saa mbili, saa tatu, saa nne. Hakukuwa na dalili yoyote. Baridi ya barafu ikakeketa kila mmoja kutokana na mawingu yaliyoungana na kuwa mazito. Haya yaliongeza giza zaidi. Upepo ulioambatana na baridi hiyo ungeweza kufanya miili yao kufa ganzi. Bahati alikuwa tayari kuwashauri askari wenzake watoke na waje siku iliyofuata maana baridi ilikuwa inakula miili yao kama chui anavyoparamia windo lake. Lakini hakutaka kutamauka mapema hivyo kwani ilikuwa siku yao ya kwanza. Ikafika saa tano. Kila mtu alikuwa keshakata tamaa ya kunasa mwizi yule. Saa tano na robo, dakika ya ishiriki ikawadia. Ilipogonga saa tano unusu, askari waliokuwa kusini mwa Arali wakaona kitu kilichotembea kwenye giza la kaniki kupitia kinjia kilicholindwa na Bahati. Wakasikia nyatunyatu kwenye majani ya kinjia cha kuingia. Kiwiliwili kikaonekana, kikapita kwa utaratibu.

Hawakuwa na haraka kwani alikuwa tayari mtegoni. Wakampa muda wa kutosha kutekeleza lengo lake. Bila ushahidi ingekuwa kazi bure. Wakanyamaza jii na kutulia kama maji mtungini. Wakangoja. Baada ya robo saa hivi, yule barobaro akatokea huku ameburuta beberu mkononi. Alikuwa na ustadi mkubwa wa kumbana mkono ili asitoe sauti. Bahati alikuwa tayari ashamwamuru mwenzake aende upande mwingine wa njia. Ikawa basi atakaporejea, wawili hawa wangekuwa kawa simba wawili waliozingira windo lao tayari kuliweka kinywani. Basi barobaro yule alipokaribia pale walipokuwa, wote wakamrukia kwa pamoja kama vile chui anavyomparamia paa ambaye kabebwa na mawazo na kusahau kuwa yeye ni chakula cha adui yake.

Kwa bahati mbaya, yule barobaro alikuwa ameshika kisu chake tayari. Wakati Bahati aliporuka, alipatana na makali ya kisu chake, kikaingia kwenye muundi wake. Goko lake likapasuliwa kuwili. Mwenzake akampiga mwizi yule aliposikia usiyai wa Bahati. Barobaro yule akazimia na kuanguka mara moja huku akipoteza fahamu. Wale

askari wengine wakaja na kumwokoa Bahati aliyekuwa akivuja damu kama maji. Alipofikishwa hospitalini daktari aliamuru mguu wake ukatwe mara moja kwani majeraha yalikuwa makubwa. Ingawa kawa mshindi, akawa kiguru kwa upande mwingine. Nikamhurumia. Wakati aliponiita ofisini mwake siku hiyo, sikuweza kutambua ulemavu huo kwani miguu yake ilikuwa imekingwa na meza yake. Bali na hayo, Bahati alikuwa kiguru shupavu na mwenye utu.

# SURA YA TATU

Nilikuwa bado sijayafahamu mambo ya ndani ya ukoo wetu. Aidha, mila ya jamii nilikozaliwa. Kwangu mimi nilidhania kuwa hadithi za bibi yangu kuhusiana na mambo halisi yaliyozunguka jamii yetu zilikuwa uongo tu na pengine uraibu kwa kila jamii kuelimisha watu wao, hadi pale alipouweka moyo wake wazi na kutujulisha kuwa hadithi zile zilikuwa na uhalisia na kila mtu alitarajiwa kuishi kulingana na mikakati yake. Ndipo nilipopata mgeuko mpya wa mawazo na fikra. Siku hiyo, sote tulikuwa tumejumuika pamoja katika chumba chake kikubwa. Chumba hiki kilikuwa tayari kimeishi miaka mingi kuliko yangu. Kama miaka yake ingelikuwa shilingi ya Kenya, basi ningeza kununua boflo moja na nikabaki na salio mfukoni. Licha ya miaka hiyo, kilionekana kuwa imara kama mwamba. Kisichotingizika kamwe.

Chumba hiki kilikuwa cha mviringo uliojengwa kwa miti kisha ikakandwa matope na kuunga ukuta. Kwa nje na ndani, ukuta huu uliweza kulainishwa kwa ustadi mkubwa sana. Mihimili tisa iliwekwa kuzunguka ukuta huu na kushikilia paa lake pasipo kuchoka. Ndani ya mviringo ule, kulikuwa na mwimo mmoja uliokuwa umechimbiwa katikati ya chumba hiki, na kulipa paa lake nguvu za kusimama thabiti. Paa hili liliezekwa kwa kutumia nyasi ndefu zilizokuwa tayari zimechukua rangi nyeusi kutokana na moshi wa kuni uliotoka kwenye sehemu ya kupikia kwa miaka kilichoishi. Sitaha yake ilikuwa imeundwa kwa kutumia miti iliyotoka upande mmoja wa ukuta kwenda hadi ule mwingine. Miti hiyo midogo kwa upana iliweza kuungana kwa pamoja na kukipa chumba hiki dari la kupendeza. Kishimo kidogo kiasi cha haja kilibakishwa kwa minajili ya kuruhusu vitu kupitishwa na watu kupanda kwenye dari lile.

Sakafu yake ilikuwa ya kipekee. Iliweza kuundwa kwa kutumia mchanga mwekundu na kisha kumaliziwa kwa kupakwa kinyesi cha ng'ombe. Mnyama huyu alikuwa wa manufaa sana katika eneo letu. Zaidi ya kinyesi chake, mkojo wake ulitumika wakati mwingine kama tiba wakati mtu alipokiuka miiko ya ndoa. Kinyesi hiki kiliweza kupewa muda wake kukauka wakati chumba kinajengwa na kisha kukipa chumba hiki mandhari ya kuvutia. Basi vijana wote kutoka kijiji chetu; Kikwetu, pamoja na vijiji vingine viwili, Kilimoni na Malishone tulilazimika kukusanyika kwenye chumba hiki.

Bali na kuwepo kwa bibi yangu, kulikuwa na wazee wengine waliokuwa na ufahamu mkubwa kuhusiana na tamaduni na itikadi za jadi. Wao walikuwa wamevuka milima na mabonde, misitu na nyika katika kusoma elimu ya ukoo wetu iliyokuwa nadra sana. Hii ni elimu iliyompa mtu katika jamii kuimarika kimawazo na kuweza kusikizwa na watu wengine. Ni elimu ambayo kila aliyekuwa nayo aliheshimika sana kama watu wanaozoa shahada kutoka vyuoni kwenye elimu ya kisasa. Bila elimu hiyo, hakuna aliyekuthamini hata kidogo katika jamii. Kwa sababu bibi yangu ndiye aliyekuwa mwenye miaka mingi zaidi kuliko wale wazee wengine, alichukua hatamu ya uongozi wa hafla hiyo. Hivyo basi, ndiye aliyekuwa na usemi mkubwa toka mwanzo hadi tamati ya kikao hicho. Baada ya sote kuwasili, akatushauri kuingia ndani ya chumba kile kilichokuwa na giza kidogo ingawa kulikuwa jioni na jua halikuwa limezama.

Jambo ambalo lilinitia hofu sana ni kuwa, kulikuwa na namna ambavyo vijana wa kike walitakiwa kuingia chumbani mle, tofauti na vijana wa kiume. Wavulana walitakiwa kuingia kinyumenyume, bila kugeuka mbele huku wamefunikwa macho kwa kaniki; ilhali wasichana walitakiwa kuingia kwa uso mbele bali wakiwa wamejitwika chungu kichwani. Ingawa nilikuwa nimefaulu mitihani

mingi sana ya darasini, mtihani huo niliuona kuwa mgumu sana. Basi ikawa tungepiga foleni kisha kufuatana kama siafu. Kufaulu mtihani kukawa kwamba lazima kila mvulana aingie kinyumenyume pasipo kwenda kando na foleni iliyopigwa. Kwa upande mwingine wa wasichana ikawa kuwa, chungu kilichokuwa kichwani kisianguke pasipo kushikiliwa. Kufeli mtihani kwa wavulana kulikuwa kukosa kufuata foleni hiyo kwa utaratibu na pengine kwenda kando nayo au kuanguka, basi mwenye kufeli angeondolewa na kutajika kama *king'enda;* kwa maana ya mwenye kiburi. Mtu ambaye hakutilia maanani masomo halisi ya jamii. Hivyo basi angeondolewa na kufukuzwa. Jambo lilo hilo lingefanyiwa msichana ambaye hangeweza kutembea akifuata foleni huku chungu kikiwa kichwani pasipo kuanguka. Kama chungu kile kingeanguka, naye angepata adhabu hiyo hiyo iliyopewa kijana wa kiume.

Nilikuwa nimeshika moyo wangu kwa woga. Sikuwa na uhakika kama ningeweza kutembea kinyumenyume kama walivyoamuru wale wazee. Mbele yangu alikuwa kijana mmoja ambaye nilikuwa nimewahi kumwona wakati mmoja kwenye hafla ya kutuzwa kwa mshindi wa mtihani wa kitaifa. Alijulikana kama Timora Waka.Tulikuwa pamoja miongoni mwa wale waliokuwa wameupita mtihani huo. Timora alitoka katika kijiji cha Malishone. Hakuwa akiishi mashambani kama sisi na wavulana wengine. Hivyo, muda wake mwingi alikuwa akiishi mjini, ingawa sikuweza kujua kama alifanikiwa kupata kazi. Baada ya kupiga foleni, tukaamuriwa kugeuka na kuangalia nyuma kisha tuanze kutembea kuingia kwenye chumba kile. Tukafanya hivyo. Basi Timora akawa nyuma yangu. Nyuma kidogo kwenye foleni niliweza kumwona rafiki yangu wa zamani aliyejulikana kama Azali. Mabarobaro watano waliokuwa wamejaa misuli na kuvalia kaptura iliyowabana kiasi cha haja, wakatokea kwa haraka kila mmoja na kaniki mikononi. Wakatufunga

kwa haraka na kwa nguvu kwenye nyuso zetu. Nikabaki kwenye giza bila kuona chochote. Kwa dakika nikawa kama kipofu. Firimbi ikapigwa kutuashiria kuanza safari. Tukaanza kutembea kwa utaratibu, kila mmoja akiwa makini asikose wala kwenda kombo na foleni ile. Kama kawaida ya kila mtihani, kila mtu alionekana kuwa mnyonge. Tukatembea kinyumenyume kwa hatua kama nane hivi. Hakuna chochote kingeweza kusikika kando yetu ila nyayo zetu tukitembea. Tukapiga hatua zingine kama tano hivi. Ghafla, nikasikia sauti kama ya kitu kilichoanguka kutoka juu hewani iliyonishtua. Nilizidi kupiga hatua bila kujali kwani sikutaka kukosea maagiza yale. Wakati huo nilikuwa nimepita kwenye mlango wa chumba hicho ila hatua kadha zilibakia niweze kufika kwenye lango. Nikazipiga kwa umakini mkubwa hadi nikaingia langoni. Nikashusha pumzi na kuketi karibu na washindi wezangu. Kaniki langu likaondolewa kwa upesi. Nikafungua macho. Nilikuwa na hamu ya kutaka kujua nani alikuwa kafeli mtihani huu. Nilishangaa kupata kuwa Timora ndiye aliyekuwa akijigaagaa pale chini baada ya kuanguka. Yeye hakuweza kupiga zile hatua kwa utaratibu. Nikamhurumia lakini sikuwa na uwezo wowote wa kumsaidia. Akabebwa hobelahobela kwa fujo na mabarobaro wawili waliokuwa wakingoja kwa hamu na ghamu kuona yule atakayeshindwa na safari. Akaamuriwa kwenda zake akaanze upya masomo ya jamii. Kutoka siku hiyo, sikuwahi kumwona Timora tena. Kwa upande wa wasichana, hakuna hata mmoja aliyefeli mtihani huo. Wote walifaulu.

Naam, ndani ya chumba hicho kulikuwa na uvundo ulioumiza pua. Kila mtu aliweza kusikika akipiga chafya. Ajabu ilikuwa, wale wazee walikuwa wametulia wala hawakupiga chafya. Kulikuwa na sanamu liliyochongwa na kuwekwa mbele ya chumba hicho lililochukua umbo la binadamu. Sanamu hilo lilikuwa na ngozi iliyochakaa na mapengo mdomoni mwake. Nikafahamu kuwa lilionyesha

mwanamke aliyekuwa kazeeka. Nalo liliwekwa mbele kidogo na sehemu walipokaa bibi yangu na wazee wale wengine. Nilipotazama upande wa juu wa chumba kile, niliweza kuona tari na juu yake kulikuwa kumewekwa vyungu vya kupikia vilivyotengenezwa kwa udongo, zana za vita kama vile nyuta, mishale, visu vya ghariba na vingine vingi. Vifaa hivyo vilikuwa vimehifadhiwa kwa minajili ya elimu pekee. Chumba hicho kilikuwa kama karakana ya uhalisia wa jamii yetu. Tukaamuriwa kuketi chini kwenye ngozi ya ng'ombe. Wasichana na wavulana pande mbili tofauti bila kutangamana. Baada ya kuketi na kutulia, nyanya yangu akatusihi tutege masikio na kushika kila neno ambalo lingetoka vinywani mwao.

Akaanza usemi wake uliokuwa umepangwa kwa mtirirko mzuri sana wa mawazo. Akasema, "Wajukuu na vitukuu wangu hamjambo?" Sote tukaitikia, "hatujambo nyanya. Ishi miaka na mikaka!" Hivyo ndivyo ilivyokuwa namna ya kumwamkua nyanya kama yule. "Basi umewadia wakati murua kabisa. Wakati wa kuwaelezea namna mnavyotakiwa kuishi na kuuhusiana kama vijana na kati ya watu wengine katika jamii," akatua kidogo kisha akameza mate. "jamii yetu ina mikakati na mipangilio fulani inayopaswa kutiliwa maanani. Pasipo kufuata kanuni kadha wa kadha kwenye maisha ya kila siku, mnaweza kwenda kinyume na matarajio ya miungu wa jamii yetu.

Tabia na mienendo yetu imejengeka katika misingi ya ukweli, utu na thamani kwa maisha ya binadamu. Juhudi zetu kama wazee ni kuhakikisha kuwa kizazi kichanga kinalelewa kwenye maadili na heshima kwa kila mmoja. Utu umewekwa mbele kuliko jambo lolote lile. Kuishi kwa amani, umoja na upendo kama watu wa jamii moja." Nyanya aliomba maji atulize kiu. Akaletewa maji kwenye kibuyu. Akapiga mafundo matatu mazito kisha akaendelea na hotuba yake. "Mtoto wa kiume alikuwa wa maana sana katika jamii. Alipozaliwa,

furaha ilijaa kwenye nyumba hiyo. Kwa kumzaa mtoto wa kiume, jamii ilikuwa na uhakika kuwa na mrithi wa mali ya familia hiyo. Basi alipozaliwa, jambo la kwanza lilikuwa kumtakasa. Ilikuwa lazima aoshwe kwenye maji yaliyotiwa mizizi, matawi, maganda na majani ya miti tofauti yaliyokuwa kapashwa joto kidogo. Waliohusika katika kumwosha mtoto yule ni pamoja na wazee waliokomaa na muuguzi aliyesamsaidia mama kujifungua. Pindi tu baada ya kuoshwa, jambo la pili lilikuwa kumrambisha asali ya nyuki ambayo ilikuwa imekaa kwa zaidi ya miezi minane. Asali hii ilikuwa inahifadhiwa pindi tu mama alipojulikana kuwa mjamzito. Asali ilikuwa na ishara ya kumfunza mtoto yule kuwa ulimwengu una mazuri yake kama anasa, furaha na amani mtu anapoishi vizuri. Kisha mtoto alikuwa akirambishwa shubiri. Shubiri hii nayo iliashiria kuwa dunia ina machungu yake pia. Kuna mambo yanayoleta vurugu, kukosana na mshtiti. Mtoto aliporambishwa shubiri angelia kwa sauti kubwa sana. Alipolia basi ingejulikana kuwa alikuwa katika hali ya kawaida.

Baada ya hatua hiyo, mama yake angepewa fursa ya kumwona mwanawe kisha kumnyonyesha." nyanya akatua kidogo alipoona kuwa Azali alikuwa na swali alilotaka kuuliza. Akamwambia aseme. "Nani alikuwa na jukumu la kumpa jina mtoto aliyezaliwa?" Azali akauliza. "Hilo ni swali nzuri sana mjukuu wangu." Nyanya akasema. "Jukumu la kumpa jina mtoto aliyezaliwa lilikuwa la wazee wa jamii ya baba yake mtoto. Wao ndio waliojua watu waliokuwa na tabia nzuri na za kuigwa katika ukoo wao ambao majina yao yangepewa yule mtoto," nyanya akamjibu kisha akaendelea na usemi wake. "Kwa upande wa mtoto wa kike, alipozaliwa familia ilifurahi kwa sababu moja tu; walijua kuwa mwanzo wa utajiri ulikuwa umewadia. Mtoto msichana alithaminiwa kwa kuwa angeleta mali kwa familia yao kuanzia siku ile alipozaliwa. Mwanamume ambaye alimtaka mtoto

yule wa kike, angeanza kulipa mahari baada ya siku thelathini kutoka mtoto alipozaliwa.

Mahari ilikuwa ikilipwa kwa kuleta ng'ombe hamsini, mbuzi mia mbili na kondoo mia moja. Hayo yote yalikuwa kando na kiwango fulani cha pesa kilichotakiwa kulipwa. Kwa hivyo, mtoto wa kike alikuwa chanzo cha familia yao kutajirika," nyanya akasema. Wakati huo, nyanya alionekana kutaka kumpisha bikizee mwingine kutoka katika kijiji cha Malishone. Yule naye alijulikana kama Bi. Zuhura. Alipopewa fursa ya kuendelea na hadithi hiyo alikumbana na swali kutoka kwa msichana aliyetoka kijiji cha Kilimoni. Msichana yule alijulikana kama Binti Saida. Naye alikuwa kajaliwa urembo na sura nzuri ya malaika. Vijana wengi katika vijiji hivyo vitatu hawakukosa kummezea mate malaika yule. Sauti yake ilikuwa ya kumtoa nyoka pangoni. Alikuwa nyota katika kijiji chao. Akauliza, "Je, wasichana walikuwa na uhuru wa kumchagua mchumba wao kutoka pahali popote?" Bi. Zuhura alikuwa wa haraka na mwenye ufasaha katika majibu yake. "Hapana. Msichana angeweza kutafutiwa mchumba wake pindi tu alipozaliwa. Mchumba wake angeanza kulipa mahari baada ya siku thelathini. Hivyo basi, wakati angekuwa mkubwa na kubalehe, mahari ilikuwa tayari ishamalizika kulipwa. Jambo ambalo lingekuwa limebakia ni msichana yule kupelekwa kwa bwana yake, awe anampenda au la, ilikuwa lazima!" Bi. Zuhura akamjibu Binti Saida. Watu walisikika wakiongea chini kwa chini katika minong'ono iliyosheheni kutoridhika na jambo fulani. Binti Saida akamwelekezea Bi. Zuhura swali jingine, "Lakini hamwoni kuwa tamaduni zenu zilikuwa kandamizi? Wasichana walikoseshwa uhuru wa uchaguzi wa wapenzi wao ilhali mmetanguliza kwa kusema kuwa tamaduni zenu zimejengeka katika uhuru na amani." Binti Saida alionekana mwingi wa ghadhabu. Midomo yake ilionekana kutetemeka. Kila mtu alikuwa amenyamaza huku tumemkodolea macho kama mzuka.

Bi. Zuhura alikuwa ameshangazwa na swali la msichana yule. Jibu la swali lake halikupatika kwa urahisi. Kijasho chembamba kikamtoka puani na kwenye kipaji chake. Kwenye mwanga wa taa ya kandiri iliyokuwa imewashwa katika hafla hiyo, haungeweza kumwona mtu vizuri sana. Akasafisha koo yake na kumjibu, "Una maswali magumu lakini nitakujibu mjukuu wangu. Lazima utambue kuwa jukumu la jamii kumtafutia mtoto msichana mchumba lilikuwa la maana sana. Kwanza, walikuwa wanamjua vizuri mwanamume aliyemchumbia, kwa matendo na jamii aliyotoka. Katika orodha ya wengi waliokuwa na nia ya kumpata msichana aliyezaliwa, ni mmoja tu pekee ndiye aliyechaguliwa na wazee wa kamati. Zaidi, wao walikuwa wanatuma mapendekezo yao katika muda wa siku kumi na nne baada ya kuzalikuwa kwa mtoto yule. Hakuna hata mmoja wao aliyekuwa anamfahamu mtoto yule, hivyo basi kama angekuwa kilema alikuwa wake. Vilevile kama angekuwa mkamilifu angekuwa wake pia. Jambo hilo liliweka usawa na haki kati ya kijana wa kike na wa kiume." Bi. Zuhura alikuwa amegonga ndipo na kumnyamazisha kila mtu. Watu wakaangaliana kwa mshangao mkubwa. Kweli, wazee wana busara si haba.

Baada ya jibu hilo, Bi. Zuhura akaendelea, "Kulikuwa na majukumu tofauti baina ya watu wa marika, jinsia na viwango tofauti katika jamii yetu. Mwanamume hakuwa na jukumu sawa na mwanamke. Wanaume walitakiwa kuwa viongozi wa kila wakati na popote pale walipoenda. Uongozi wao ulianzia kutoka kwenye familia zao hadi nje ya familia. Mwanamke hangeweza kupewa uongozi wowote. Alitakiwa kuwa kama mfanyakazi katika nyumba. Mwanamume alipewa majukumu mengine kama kulisha mifugo, kutafutia familia chakula, ujenzi wa nyumba na kazi zilizohitaji kutumia nguvu zaidi. Kwenda mawindoni kutafuta kitoweo cha wanyama pori ni jukumu lililopewa mwanamume. Kwa upande wa mwanamke, alikuwa

akifanya kazi za nyumbani kama vile kupika, kuosha vyombo, kufua nguo na kutunza watoto. Mwanamke angeweza kwenda sokoni kununua vitu vya kutumia huko nyumbani. Jioni wangeandamana na wanawake wengine kwenda kutafuta kuni za kupikia chakula na wengine kwenda mtoni kuchota maji. Wanawake walitumia migongo yao kubebea mizigo ilhali wanaume wangetumia mabega yao au pengine mikono," akamalizia Bi. Zuhura.

Wakati huo, watu wengi walionekana kuanza kusinzia kwa umbali, jambo ambalo nyanya yangu alikuwa tayari ameshaliona kutokana na jinsi walivyokuwa wakienda miayo. Basi Bi. Zuhura akasema kuwa angetaka kumpisha Bi. Zaina aliyetoka katika kijiji cha Malishone ili aseme namna watu walivyotakiwa kuhusiana kati yao kulingana na jinsia. Bi. Zaina, aliyekuwa kidogo akisinzia akashtuliwa. Akaanza usemi wake, "Nawashukuru nyote kwa utulivu wenu hadi sasa. Naam, kama jinsi mlivyoketi kwa sasa, wasichana sehemu yao na wavulana vilevile kwenye sehemu yao tofauti, vijana wa kike na wale wa kiume walikuwa hawaingiliani moja kwa moja kama vile katika kucheza na kulala. Wavulana walikuwa wakilala kwenye vyumba vyao tofauti na wasichana. Michezo ya wavulana ilikuwa tofauti sana na michezo ya wasichana. Wavulana waliweza kucheza miereka wakati wasichana wangecheza mchezo wa kuruka kamba. Elimu haikuwa kama vile ilivyo siku hizi. Hakukuwa na wazee wa shule kama ilivyo kwa sasa. Elimu ilikuwa ya kuwasikiliza wazee wa jamii walioelewa sana tamaduni kama tunavyofanya sasa. Vikao tofauti vilikuwa vinawafunza vijana wa kiume na kike majukumu yao. Hivyo basi, kila mmoja alilelewa akijua analopaswa kufanya," Bi. Zaina akakomea hapo.

Mambo hayo yote waliyosema yalikuwa yenye uzito mkubwa na uhalisia mwingi sana. Sikuwa nimejua mengi kama hayo kutoka kwa

jamii yangu. Nikawaza na kuwazua kisha nikauliza swali moja. “Mbona tusiige mwelekeo mpya wa kutilia maanani elimu ya kisasa yenye manufaa zaidi kuliko kufuata tamaduni zisizo na manufaa ila zinaturudisha nyuma?” Nikauliza. Swali langu lilionekana kuwakera wengi sana. Kila mmoja alimtazama mwingine kwa mshangao. Pia mimi nilishtuka. Pengine swali langu lingeniletea madhara makubwa kuliko nilivyodhani, bali nikapiga moyo konde na kujiambia, “liwe liwalo.” Nyanya yangu hakuonyesha mshangao wowote kwani alikuwa tayari amenizoea kwa kumwuliza maswali kama hayo kila wakati, hasa niliporudi nyumbani kutoka shuleni.

Bi. Zuhura alionekana kutaka kunijibu. Akasafisha koo yake kwa utaratibu kisha akasema, “Mwacha mila ni mtumwa. Kuiga mwelekeo wa elimu ya kisasa ni sawa na kujiuza kwa wazungu. Tamaduni zetu zina umuhimu mkubwa zaidi kushinda mfumo wa mambo ya kigeni. Watoto wanaposoma wanadharau mila yetu na kutudunisha. Tazama aina ya mavazi wanayovaa. Wasichana wetu wameacha kuvaa nguo zinazositiri sehemu muhimu za mwanamke. Wao wanavaa nguo zilizoacha matiti, tumbo, vifua, migongo na mapaja yao wazi. Wanatukosea sana. Wavulana nao wanaghairi kuja nyumbani na kuishi mijini kisha kuoa wanawake tusiowajua vizuri. Hii ni kinyume na tamaduni zetu. Zaidi, vijana wanasahau majukumu yao. Hivyo basi, kuiga mfumo wa kigeni ni sawa na kujitia kitanzi,” akamalizia Bi. Zuhura.

Jibu lake lilikuwa limetoka moyoni na alikuwa kalijibu kwa machungu aliyoshuhudia kutoka kwa vijana wengine waliokuwa tayari wamepotoka. Nilikosa swali lingine. Alikuwa ameninyamazisha kwa jibu lake lenye busara sana. Wakati huo hatukuwa na budi kufumukana. Nyanya yangu akatupa baraka zake na usemi wa mwisho wa kutubariki kama ilivyokuwa desturi.

Waliokuwa wakielekea katika vijiji vya malishone na Kilimoni wakaungana katika vikundi na kwenda kwa pamoja. Mimi nikaandamana na Azali. Tulipofika kwetu, nikamuaga naye akaelekea kwao.

# SURA YA NNE

Ilipotimia saa kumi na moja kamili, dereva alitusairi kuingia kwenye basi tayari kuanza safari. Mngurumo wa basi hili uliweza kupasua ukimya wa asubuhi ile na kuwaamsha ndege waliokuwa bado wamelala. Anga nayo ilikuwa raufu. Mawingu mazito ya asubuhi yalikuwa yametanda kote. Kinyume na jinsi yalivyokuwa wakati tulipokuwa tukiingia, sasa yalikuwa mazito zaidi. Kibaridi cha pekee kikayumbishwa na upepo ulioanza kuvuma huku na kule. Upepo huo ukakamilisha kazi yake na kusababisha matone madogo madogo ya mvua. Mvua ya rasharasha ikaanza. Matone hayo yaliweza kuungana kwa pamoja na kutiana nguvu. Rasharasha ikageuka na kuwa masika.

Naam, aliye na macho haambiwi tazama. Mvua, baridi, na upepo ukayafanya maisha ya watu waliokuwa wamejibanza kwenye kuta za majengo ya kampuni hii kufanya uamuzi na kulikimbilia basi. Wakaanza kuingia mmoja hadi mwingine. Kwa upande wa ndani, dereva, aliyejulikana kama Omwami, alionekana akipangusapangusa kioo cha mbele cha basi hili, ili kuwa na maono mazuri. Muye uliosababishwa na baridi uliweza kugumbika kioo hicho kwa ndani. Omwami alikuwa bonge la mtu, mwenye umri wa makamo na urefu wa wastani. Tabia zake zilikuwa za kupendeza kila aliyemjua na maneno yake yalikuwa safi kama msahafu. Alikuwa mcha mungu na aliyependa kuona wengine wakifaulu. Alikuwa mwenye stihizai si haba, hulka iliyomfanya kupendwa sana na watoto na marika kutoka kijiji alichoishi.

Kwa jumla, basi lile lilikuwa la viti sitini na viwili. Kwa kuwa wafanyakazi wake ambao walikuwa wakisafiri siku ile walikuwa thelathini na watatu, kulikuwa na nafasi ya takribani watu wengine ishirini na tisa. Kila mtu alikuwa na uhuru wa kuketi alipotaka isipokuwa kwenye kiti cha dereva na kile cha Tanasha, ambaye

alikuwa ameketi mkabala na Omwami. Mama mmoja aliyekuwa kabeba mtoto mchanga alisaidiwa kuingia kwa utaratibu. Kitoto kile kilikuwa kimemgandia mama yake kama ruba, kwa minajili ya kupata joto lililobakia kwa mama yake na zaidi, kukingwa kutokana na baridi ile ya kuumiza mwili. Wakati mama yake alipojaribu kutoa mbeleko ili kukileta kifuani kutoka mgongoni, kitoto kile kikagoma kama kihongwe huku kikipiga nduru. Hapo ndipo Omwami alipotoka kwenye kitu chake na kutembea hadi kwenye safu ya pili karibu na mama yule. Akakishika kile kitoto huku kapachika tabasamu usoni mwake. Akakituliza kwa upole na kukiondoa kutoka kwa mama yake kwa utaratibu huku akikibembeleza kama yaya. Kitoto kikatulia na kunyamaza. Mama yake akaketi kwa utaratibu na kukipokea kitoto chake huku kila mtu akistaajabu namna Omwami alivyokituliza kitoto hicho. Omwami akarudi kwenye usukani kwa madaha ya ushindi. Akangurumisha gari. Tukaondoka.

Lewa alikuwa tayari ameingia kwenye basi hilo na kutulia tuli huko nyuma. Kwenye viti vinne vya nyuma alikuwa peke yake. Wingi wa nafasi hiyo ulimchanganya sana. Angeweza hata kulala kama angetaka. Hiari ilikuwa yake. Akachagua kulala huku kashikilia chepeo yake usoni na kuziba macho na mdomo. Hata ingawa alikuwa amejinyamazia na kutulia, harufu mbaya ya pombe ilikuwa inamtoka. Ilipochangayika na uchafu wa mwili ikazidi kuvunda. Ikamsaliti. Kama haingelikuwa usafi wa basi hili, kiti kile kingelipata wageni wengi ambao mara nyingi hujialika kwenye karamu kama ile. Nzi.

Mdudu ninayemchukia kwa moyo wangu wote. Wakati nilipokuwa mdogo, mama yangu kaniambia kuwa jirani; Ajuza aliyekuwa kwenye jioni yake ya maisha, alipatikana na ugonjwa wa kipindupindu. Ukosefu wa maji safi na chakula ulikuwa umevamia kijiji chetu. Wakazi wakakosa matumaini ya maisha na kungoja siku yao ya

mwisho. Kutokana na mlipuko huo, kijiji kizima kiliadhirika na watu wengi wakafa. Hakukuwa na waganga wa kutibu wagonjwa, hivyo, aliyenusurika kama mama yangu na familia yake, walimshukuru mungu. Mama kanieleza kuwa, nzi walikuwa wengi wakati wa mlipuko huo na waliwashinda wanadamu nguvu. Dawa za kienyeji walizopuliziwa hazikufaulu kuwaua. Baada ya kunusurika kifo cha ndwele hio, akaapa kusisitiza usafi wa chakula, maji, malazi, na mwili kwa familia yake na majirani. Akachukia mdudu yule kwa vyovyote vile. Nikawa mrithi wa hulka yake.

Hivyo basi, uvundo huo ukafukuza kila mtu kuketi angalau mita chache kutoka kwenye kiti chake. Kwa vile nilikuwa tayari nimedokezewa namna mambo yalivyokuwa, nikaungana na wengine kuketi mbali kidogo. Bila shauku yoyote, safari ikaanza. Tanasha alikuwa kazama kwenye mazungumzo na Omwami asishuku lolote. Pia kwa maoni yangu, urefu kati ya nyuma na mbele ya basi alipoketi ulifanya uvundo huo kufifia na usiwe na nguvu za kushauri pua yake. Lewa hakutaka Tanasha kujua kwamba alikuwa kalewa chakari. Alikuwa kakosa kutumia busara na alipokabidhiwa pesa ya ziara jioni ya siku ya kuamkia safari hii, alienda zake akapiga maji. Kiu ya pombe ilimwelekeza kwenda kuikata mara moja. Maskini Lewa!

Minong'ono iliashiria kuwa, kama Tanasha angefahamu kwamba Lewa alikuwa kapiga mtindi, pengine angempiga kalamu mara moja. Tanasha alikuwa wa pili katika cheo kwenye kampuni ya Ujadi Mills, baada ya Bwana Kolea, aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu. Alikuwa mwanamke mcheshi na mwenye utu. Alithamini kila nafsi katika kampuni hiyo na wala hakumdharau yeyote kwa vyovyote vile. Hakuwa na mapendeleo yoyote. Ratili ya umuhimu wa kila mmoja haingeweza kuegemea upande wowote. Aliwaweka wafanyakazi wake wote kwenye kiwango kimoja. Maamuzi yaliweza kufikiwa kwa

njia ya uwazi na usawa. Kutokana na sifa hizi, aliweza kupendwa sana na kila mtu katika kampuni hii. Kwenye hafla za sherehe kama hii, ndiye aliyeandamana na wafanyakazi wake walipokuwa wakisafiri kwa niaba ya uongozi wa kampuni ya Ujadi Mills.

Alikuwa mwenye ngozi ya maji ya kunde na aliyejaliwa sura ya kuvutia. Ingawa alikuwa mama kwa watoto wawili, mwili wake ulikuwa na umbo la mnato machoni. Alikuwa mwenye kuvaa mavazi ya dhamani kubwa sana. Mavazi yake yalikuwa yakichukuana sawasawa na mapambo aliyovaa. Sio mikufu, bangili, vipini, chupio, herini, taji, kugesi na mapete aliyokuwa akivaa. Kila hafla ilikuwa na mavazi yake kama ilivyostahili. Zaidi, alikuwa na mazoea ya kuweka nywele zake huru bila kusuka. Kila alivyofanya hivyo, angeweza kuzipaka mafuta na kuzilainisha kwa kutumia machine ya nywele. Matokea yake yalikuwa dhahiri, zilinyooka sawasawa. Kwenye unyoofu huo, angechagua chupio lililofaana na mavazi ya siku ile na kuzishika kwa pamoja huko nyuma.

Kiwango cha pesa alichokuwa akipata kutoka kwa kampuni ile, hakikumruhusu kuishi maisha ya chini. Hata ingawa alikuwa mwenye pesa na mali nyingi, kiburi hakikuwa na nafasi katika maisha yake. Alimheshimu kila mtu. Kutokana na utu wake, aliweza kuwajengea mayatima na wajane kutoka katika eneo lake makao ya kuishi. Walikuwa wakipata kila walichohitaji pale kama vile mavazi na chakula. Malazi yao yalikuwa mazuri hata kushinda ya watu wengine waliokuwa wakifanya kazi. Sifa za utu, ukarimu na uzalendo wake ziliweza kujulikana ndani na nje ya kampuni ya Ujadi Mills.

Zaidi ya hayo, mwanamke huyu alikuwa mcha mungu. Aliamini kuwa kulikuwa na kiumbe mwenye nguvu zaidi kuliko miungu wa eneo lake. Kulikuwa na mungu anayetuliza mawimbi ya bahari na dhoruba ya nchi kavu inapopiga. Kulikuwepo mungu aliyeumba

wanyama pori, wanyama wanaoishi majini, pamoja na ndege wa angani. Tanasha alifahamu kuwa pumzi aliyopumua kila siku haikuwa kutokana na uwezo wala nguvu za binadamu, bali kutokana na nguvu za mwenyezi mungu. Naye alikuwa kasoma hadi chuo kikuu, alipopata shahada ya uzamili katika kitengo cha mambo ya kigeni. Elimu ya chuo kikuu haikumfanya yeye kuacha mila na desturi za jamii ya kwao. Kuna mambo fulani ya utamaduni angefuata na kuna mengine kwake hangeweza kuiga. Hivyo basi, kabla ya safari aliweza kumsihi Bwana Nena – aliyekuwa mpishi mkuu, kuomba ili jalali aibariki na kuilinda safari yetu. Ingawa sio kila mtu aliamini dini ya Tanasha, hakuna yeyote angeweza kupinga ombi lake.

Bwana Nena akasimama na kuwasihi watu wote kufunga macho na kuomba kwa pamoja. Kuna wale waliofunga na kuna wengine waliokosa kufunga macho yao. Wote waliokuwa wamevalia kofia iliwabidi wavue kama ishara ya heshima kwa mungu. Wakatulia tuli kisha Bwana Nena akaomba. Kwenye maombi yake hangeweza kukosa kumtaja mungu kama dereva wa safari ile na kisha kuomba dua njema na rehema kwenye safari. Imani ya wengi wa dini ile ikawahakikishia usalama na kukingwa kutokana na mihadhara ya safarini. Naam, kati ya watu waliokuwa wameshuhudia mabadiliko makubwa maishani, mmoja wao alikuwa Bwana Nena. Alikuwa ndio sasa ameokoka na kufuata dini mpya. Naye aliweza kujulikana kwa tabia zake mbovu sana. Alikuwa mwizi wa mabavu na jangili sugu wakati alipokuwa akiishi mjini. Angeweza kumwibia mtu yeyote pahali popote, ilimradi angepata kitu cha kutia kinywani. Maisha yake yalikuwa ya kuwadhulumu watu na kuwatendea mabaya.

Kisa kilichomfanya kukoma uovu na kukata kauli ya kuokoka kilimfunza maadili mema. Pengine angekuwa maiti leo kwani siku yake ya arobaini ilikuwa tayari imewadia. Ilisemekana kuwa, kuna

wakati alihusika katika kuwatimua wanasiasa waliokuwa wamekusanyika mjini Tulia katika uwanja mkuu wa Senana. Mpinzani wa mwanasiasa aliyetarajiwa kuhutubia wananchi siku ile alikuwa amemlipa, yeye pamoja na vijana wengine ili kutekeleza uovu huo. Mwanasiasa huyo hakutaka kushindwa kwenye uchaguzi uliokuwa umekaribia, hivyo, alitumia kila njia kumwangamiza mpinzani wake aliyekuwa maarufu sana katika eneo lake.

Watu walipoketi kwenye viti na kutulia huku wakimngoja mtarajiwa wao, vijana wale walianza sokomoko mara moja. Rabsha ikawakodolea macho wananchi waliokuwa na nia njema na kiu ya kusikia kiongozi wao. Wakaanza kurusha mawe kwa vishindo bila kujali mtu yeyote yule. Watu walipoona hayo, kitete kikawaingia. Wakaanza kukimbia kutafuta usalama. Inaaminika kuwa ghasia zile zilisababisha kifo cha mama mmoja aliyekuwa mjamzito. Hangeweza kukimbia na wengine. Alianguka chini na kukanyangwa na umati uliokuwa ukikimbia kuepuka mawe yaliorushwa kwao. Baada ya tukio hilo, askari wakaanza uchunguzi wao kujua ni nani kahusika na maovu hayo. Serikali nayo ina mkono mrefu. Waliweza kufahamu kuwa Bwana Nena ndiye aliyekuwa mhusika mkuu. Akatiwa mbaroni na kupelekwa rumande akisubiri uamuzi wa mahakama. Siku iliyofuatia akawasilishwa mahakamani kujibu mashtaka ya kusababisha rangaito na mauaji ya mama yule na uhai uliokuwa ndani yake. Ushahidi ukamkamata na akawa mwenye hatia hiyo. Pesa za mwanasiasa yule alizokuwa kapewa, zikamzamisha kwenye matukio ya kujuta. Akajimezea tembe yake kwa machungu. Zake arobaini zikatimia siku hiyo.

Huko jela aliweza kupata dhuluma zaidi ya alivyodhania. Akateswa kwa kichapo cha mbwa siku baada ya nyingine. Kazi ya sulubu ilikuwa ndio mtindo wake kila siku. Hakuna chakula alichopata na

kama kingepatikana, kilikuwa kidogo na kisichofaa kwa vyovyote vile. Uongozi ulikuwa haujali kamwe. Baada ya mwezi mmoja, alikuwa amekonda kama ng'onda na mwili wake ukawa kama gofu. Hali yake ya afya ikadhoofika sana. Akajuta matendo yake ila majuto ni mjukuu huja kinyume.

Baada ya miaka mitano ya mateso katika mikono ya askari katili, jela lilikuwa limemfunza maadili. Ulimwengu ulikuwa umempa dawa yake na kumtibu sawasawa. Serikali ikamwachilia huru kwani ilifahamu fika kuwa alikuwa hawezi kumwua hata nzi. Hapo ndipo alipokata kauli ya kuanza maisha upya la sivyo angekufa wakati wowote. Baada ya kutoka jela, akaanza maisha ya wokovu kwenye dini mpya. Dini ambayo alikuwa akiisikia tu kwa umbali, bali hangeweza kusema umuhimu wake. Waliomsikia na kumwona wakati huo hawangeamini kuwa alikuwa Bwana Nena. Alikuwa kabadilika sana. Kweli, mui huwa mwema. Kampuni ya Ujadi Mills ikampa kazi. Kazi ya upishi.

Kila mtu alikuwa mwenye furaha na tabasamu, mwingi wa tabaradi na nyuso zilizong'aa tulipoanza safari. Nilijifunga mshipi na kuegemea kwenye kiti changu. Msururo wa mawazo ulikuwa umejaa akilini mwangu. Niliona kuwa hata mimi nilikuwa katika safari. Safari ambayo nilijua tu mahali nilikotoka wala sikufahamu mahali nikoelekea. Nilimkumbuka rafiki yangu tuliyesoma pamoja katika chuo kikuu huko mjini. Naye alifahamika kama Hamisi. Alikuwa amesomea biashara. Hakusita kunihimiza kuhusiana na masomo yangu yaliyokuwa yamejaa mikosi. Mara kwa mara ningefanya kazi isizofaa kama kuuza mboga kibandani ili kutafuta karo na pesa ya matumizi. Wakati mwingine ningelala njaa kwa kukosa hata shilingi ya kununua chakula. Nilipobahatika kupata angalau kidogo cha kutia mdomoni, nilishukuru na hata wakati nilipokosa vilevile. Nguo zangu

zilikuwa chache sana na hata ningeweza kuvaa mavazi yale yale kwa siku tatu. Baba yangu hakuthamini umuhimu wa masomo yangu. Ingawa alikuwa akisaidia kwa kiwango kidogo mno, jukumu kubwa la kutafuta pesa lilikuwa langu. Mola naye hamtupi mja wake, humruzuku kutoka kwa mateso. Akanijalia nikamaliza masomo yangu ya chuo kikuu. Nikashukuru.

Hata hivyo, kilichonipa mawazo mazito na kunikosesha raha maishani ni kuona marafiki zangu, akiwemo Hamisi wakiwa kwenye kazi nzuri sana. Wao waliweza kupata magari ya kifahari na kuoa mabibi warembo zaidi. Maisha yao yalionekana kutimilika sawasawa na ndoto zao. Hamisi alikuwa amepata kazi kwa bwana mmoja aliyekuwa mwenye asili ya kihindi huko mjini. Kwani hatima yangu ilielekea wapi? Mbona nikafaulu katika chuo kikuu na kisha nikakosa kazi? Hayo yalikuwa baadhi ya maswali yaliyokuwa akilini mwangu siku ile. Niliweza kumfikiria baba yangu mzazi. Alikuwa ameketi kwenye kiti cha pili, safu ya pili. Kiti hicho kilikuwa nyuma ya dereva na kando ya Tanasha. Niliweza kukumbuka alivyokuwa akinishauri kila wakati, "Kwenda kinyume na utamaduni wa ukoo wetu kuna laana kubwa. Kuwakasirisha miungu wa babu zetu kuna hasara. Hakuna anayetakiwa kuiga utaratibu wa wazungu katika familia hii. Ndio maana nakushauri usijihusishe na mambo ya masomo ya kigeni. Ningekuwa na uwezo wa kuepuka kifungo cha dini ningeepuka, ila kwa sasa niko kwenye gereza la dini na utamaduni. Nikitoroka husuni hii, pengine madhara yake yanaweza kukudhuru pia wewe," alisema baba yangu wakati nilipokuwa najiunga na chuo kikuu.

Mawazo yangu yakanipeleka katika kuamini kuwa maneno hayo yalikuwa na ukweli. Tulikuwa tumefungwa pamoja naye. Hakuna mmoja angeweza kumwokoa mwenzake. Pengine nilikuwa nimeikosea miungu ya jamii yetu kwa kukosa kufuata maagizo ya

baba yangu mzazi. Inawezekana walikasirika na ndio maana maisha yangu yalikuwa yenye mikosi si haba. Nikajutia kuzaliwa katika jamii yenye mila kandamizi. Mila ambazo zilizuia mabadiliko na zilizothamini mambo ya kale na yaliyopitwa na wakati. Desturi zilizojengwa kwenye misingi ya mambo ya kale ambayo hayakuwa na umuhimu wowote.

Nikatamani mabadiliko katika fikra za wazee wa zamani kwenye jamii yetu. Jamii yetu ilizuia ufanisi na maendeleo makubwa. Ilizuia uchumi wa kipekee kutoka kwenye akili changa za kizazi kilichozaliwa. Niliamini kuwa elimu ya kigeni ilikuwa imenifungua kutoka kwenye ngome ya ujinga na tamaduni zisizo na mwelekeo. Ikanipa kujua namna ya kukubali kila mtu katika jamii, awe mwanamume au mwanamke, mdogo au mkubwa. Elimu ilipinga mambo mengi mabaya yaliyotendwa na watu wa jamii yangu. Ukeketaji ulikuwa umekithiri mipaka. Ndoa za mapema na lazima zilikuwa jambo la kawaida miongoni mwa wenyeji wa eneo letu.

Lakini, nilikula chakula na kunywa maji ya utamaduni wetu. Nilikuwa nimefungwa sana na hata pengine elimu na dini ya kigeni havingeweza kuniokoa kabisa. Peke yangu singeweza kuleta mwamko mpya pasipo wengine kunisaidia. Nikajiona mjinga hata zaidi. Nikafikiri namna ningeweza kujitoa kwenye lindi hili. Kama miungu hawa ndio walinikosesha kazi, maisha yangu yalielekea wapi? Mawazo yangu yalirejeshwa kwenye hali halisi na sauti ya Lewa. Alikuwa anabubujikwa na maneno kama mwendawazimu. Wakati huo mwangaza wa jua ulikuwa tayari unaingia. Miale yake ilikuwa inapitia kwenye vidirisha vya basi hili kubwa. Sasa ungeweza kuona kila kitu vizuri. Hapo ndipo nilipopata nafasi murua kabisa ya kumtazama Lewa. Naye alikuwa mchafu kama fugo. Nywele yake ilikuwa imesimama kama askari wa jeshi. Ute wenye povu ulikuwa

unamtoka kinywani kutokana na pombe aliyokuwa amekunywa. Tongotongo zilikuwa zimejaa machoni na udenda kumtoka mdomoni. Alikuwa hatazamiki.

Kwa sauti ya kukokoteza akasema, "Si..a..mi..ni kwa…mba…ma…o…mbi..ya Bwana Nena yalikuwa ya kutosha!" Kisha akafululiza kwa utaratibu, "Maombi kama hayo yana uwezo kushinda miungu tunaoamini? Tuko katikati ya vitu viwili vyenye nguvu. Mungu anayesema ana uwezo mkubwa sana na miungu wetu ambao wana uwezo mkubwa pia. Wao ndio wametulinda sisi, pamoja na mababu zetu walioishi ulimwenguni miaka mingi iliyopita. Walikuwa tangu enzi na jadi. Mungu wenu huyu ameletwa na wazungu. Ni mchanga sana na hana ufahamu wa mambo tunayofanya kila siku. Bado niko katika mtafaruku na sitofahamu kuhusu ukweli wa mambo haya!" Akasema Lewa.

Kila mtu alibaki kumwangalia kwa mshangao mkubwa. Wakashindwa namna ya kumjibu. Bwana Nena alimwangalia kwa jicho la dharau. Alihisi kuwa Lewa alikuwa amemdunisha; sio yeye pekee bali mungu anayepaswa kuheshimiwa na viumbe wote. Alitaka kumjibu kutokana na ghadhabu lakini akasita. Pia yeye alikuwa kazubaishwa na maneno ya Lewa hata akaanza kujishuku kama alikuwa anajua ukweli wowote. Wakati huo, Tanasha alikuwa amezama kwenye mazungumzo kati yake na Omwami pamoja na baba yangu. Hawangeweza kusikia chochote kutoka nyuma. Watu wakatulia baada ya Lewa kuketi kwenye kiti chake tena.

Tulikuwa tumesafiri kwa kipindi cha saa tatu hivi na tukaingia kwenye nyika. Masafa yale yalikuwa takriban maili mia nne na hamsini. Tulikuwa tayari tumevuka tambarare na vilima. Jua nalo lilikuwa angavu na joto la kadri. Watu walikuwa tayari wameanza kuchoka na wengine walipiga miayo. Hakuna aliyehitajika kuhitimu

chuo kikuu kujua kuwa walikuwa wamechoka tayari. Tukapita karibu na mbuga la wanyama wa pori. Mandhari ya mbuga hili yalikuwa yakupendeza na yenye mvuto wa kipekee. Mara tukaona kundi la pundamilia. Pundamilia wale walikuwa wakila nyasi huku wakupunga upepo kwenye kivuli cha mti mmoja mkubwa. Kila mtu alisimama kuchungulia kwenye vidirisha. Walikuwa hawajaona punda kama wale. Mabuti alipowaona aliuliza kwa sauti, "Sasa hawa punda walitoka wapi? Ni mtu aliyewapaka rangi au walizaliwa hivyo? Badala ya kuwekwa hapa bila kazi yoyote, mbona wasingepelekwa kwetu nyumbani ili kutusaidia kubebea mizigo? Nadhani wanaweza kuwa na manufaa zaidi kuliko punda wetu kwa sababu ni wanono na wenye afya nzuri," akakomea hapo.

"Ha ha ha," Alicheka Karembo, msichana wa Tanasha ambaye pia yeye alisafiri nasi. "Hawa wanaitwa pundamilia. Rangi yao huwa hivyo kinyume na punda wa nyumbani. Wamewekwa katika mbuga hili la wanyama kwa minajili ya kuhifadhi uhalisia wetu. Ni kinyume cha sheria ya nchi kuwaua au kuwawinda wanyama kama hawa kwa sababu kama hizo ulizotaja. Lengo la kuwaweka hapa ni kuwavutia watalii kutoka nchi za kigeni kama vile Amerika, uropa na zingine. Wao huzuru nchi yetu mara kwa mara kuwaona na huleta pesa nyingi. Hivyo basi, ni vizuri kuhifadhi utamaduni wetu," akamalizia Karembo. Mabuti akanyamaza huku akitabasamu kwa jibu alilopewa.

Karembo alikuwa binti wa Tanasha na ndiye aliyekuwa chaudere wake. Alikuwa amepokea masomo yake ya shule ya upili katika shule moja ya kitaifa. Kwa kipindi kile, alikuwa akingoja kujiunga na chuo kikuu Uigereza. Alikuwa na kaka yake mdogo aliyekuwa katika darasa la tano. Watoto hawa walikuwa wepesi wa kushika mambo hasa darasani. Kaka yake alipoona mnyama yeyote wakati wa safari angeweza kumtaja kwa jina lake. Sio wanyama pekee, bali pia magari

tofauti tuliokutana nayo. Maneno ya Karembo yalionekana kumshangaza Mabuti. Akasema, "Naona vita vikubwa kati ya ugeni na uhalisia. Ugeni unasisitiza tuige mambo yake kama vile elimu, dini na teknolojia mpya huku tukitelekeza utamaduni unaosemekana kuwa kandamizi wakati hao wageni ndio wanalipia kuja kuona wanyama tuliowahifadhi katika mambuga yetu. Kwa upande mwingine nasi tunatumia mambo ya kigeni kama vile basi hili ambalo tunasafiria. Tumeacha kukimbia na kutumia moto kuwasiliana kama ilivyokuwa zamani. Utofauti huu wa mawazo unatupeleka wapi? Tutafuata mwelekeo upi?" Aliuliza Mabuti kwa wasiwasi.

"Tunapaswa kuiga mambo ya kigeni yanayofaa na kukoma yale yanayoweza kupotosha. Aidha, tunapaswa kudumisha na kuthamini mambo ya kitamaduni ambayo yanatuletea manufaa bali sio balaa na kuturudisha nyuma," Karembo alimwambia Mabuti. Mazungumzo kati ya Mabuti na Karembo yaliweza kuwasaidia wengi katika basi hili waliokuwa wakisikiliza kwa umakini mkubwa. Mabuti alijua kuwa maneno ya Karembo yalikuwa kweli na yenye uzito mkubwa sana. Akabakia akiwatazama wanyama wengine huku akistaajabu. Safari hii ilionekana kuwafumbua wengi macho, akiwemo Mabuti.

# SURA YA TANO

Katika safari kama hizi, kampuni ya Ujadi Mills ilikuwa ikiwapa wafanyakazi wake fursa ya kusoma na kujifunza mambo mapya, hususa yaliyohusiana na utamaduni kama ilivyokuwa lengo kuu la kuanzishwa kwake. Bali na kuwasafirisha wafanyakazi wake kwenye sehemu tofauti na kuwapa morali ya kazi, iliwaruhusu kuja na watu wasiozidi watatu kutoka kwa familia zao. Ndio maana Tanasha alikuwa ameandamana na watoto wake wawili. Mimi pia sikuwa mfanyakazi katika kampuni hii ila niliambatana na baba yangu.

Kwa wakati huo, tulikuwa tumesafiri kwa saa nne unusu bila kupumzika hata kidogo. Safari hii ilionekana kuwa ndefu sana. Watu walikuwa hoi. Haja za kawaida zilikuwa zimetukaza sana. Kubwa na ndogo. Kuna wale waliotaka kula na wengine walitaka angalau watoke nje ya gari wapunge upepo vizuri. Kawaida ya mwanadamu ni kutembea kwa uhuru wala sio kufungiwa kama mfungwa. Hata hivyo, nilimhurumia Mama Azara aliyekuwa amebeba mtoto mchanga. Kwa muda tuliokuwa tumesafiri, niliweza kuulizia jina lake na kulipata kwa usahihi. Alikuwa mama aliyesaidiwa na Omwami kutuliza mtoto wakati safari ilikuwa ikianza. Alihisi kuwa safari hiyo ilikuwa kama nanga. Malaika yule alikuwa amemtapikia na pia kukojoa. Zaidi hata yeye alihisi amechoka na alikuwa akilia hata alipopewa matiti anyonye.

Tanasha aliweza kutambua kuwa watu walihitaji kupumzika kidogo na zaidi kujisaidia. Lakini hatungesimama mahali popote pasipo na maduka wala mikahawa ya kununua chakula. Hivyo, Tanasha alitaka tufike pahali penye maduka au mahoteli ili wasimame hapo. Wahenga hawakukosea waliponena kuwa maji ya kifuu bahari ya chungu. Lewa alikuwa kashindwa kabisa kujizuia. Hali yake ilikuwa sawa na ya yule malaika. Alikuwa hatazamiki.

Akaamua kwenda kumwamuru dereva asimamishe gari. Aliposimama, suruali yake ilikuwa kaloa kutokana na mkojo. Karembo na kaka yake mdogo hawangeweza kujizuia kucheka walipomwangalia. Wakacheka kwa sauti kubwa iliyomzindua Tanasha, dereva na baba yangu, wakatazama nyuma kwa mshangao. Macho ya Tanasha yalipatana ana kwa ana na macho ya Lewa aliyekuwa tayari kasonga mbele karibu nao. Lewa akaganda kama barafu. Alikuwa amemwamusha simba aliyekuwa amelala. Ghadhabu ya Tanasha ikapanda. Macho yake yalikuwa kama msumeno moyoni mwa Lewa. Hakujua afanye nini. "Mbona usijieleze bwana Lewa? Ingekuchukua muda kiasi gani kwako wewe kusema ulitaka kujisaidia badala ya kuchafua basi kama mtoto mchanga? Upumbavu wako utakwisha siku moja. Waambie babu zako wakufungue kutoka kwa kifungo cha mila. Ulevi hautakusaidia kwa chochote, pengine utakukosesha mambo mazuri," Tanasha alimwambia Lewa.

Kwa wakati huo, tulikuwa tayari tumefika kwenye maduka. Akamwomba dereva kulisimamisha basi kisha akawaambia watu washuke waende wajisaidie kwenye vyoo vya mkahawa mmoja hapo tuliposimama. Lewa alipoona basi limesimama, alitoka mara moja na kwende mbele kidogo mahali palipokuwa na miti mifupi ili ajisaidie kama kawaida ya mambo halisi ya nyumbani. Hakuna aliyejua choo kilikuwa nini hasa. Ni kazini tu ndiko kulikokuwa na vyoo, navyo vilikuwa havitumiwi sana na wafanyakazi. Mara watu wote wakamfuata Lewa. Tanasha ndiye aliyewakosoa na kuwaambia kuwa lazima wangetumia vyoo la sivyo wangejipata matatani kwa kuchafua mazingira. Zaidi ya hayo, askari wangewakamata kwa kuvunja sheria za mji.

Kwenye vyoo hivyo kulikuwa na sehemu tofauti ya wanaume na wanawake. Baada ya waliotaka kujisaidia kumaliza, zamu ya kutafuta chakula ikawadia. Mikahawa ya hapo na mahoteli yote hayakuwa na chakula walichotaka. Kulikuwa kumepikwa vibanzi, banjia, kuku wa

kukaangwa, nyama choma, pilau, wali, ugali, halua na vyakula vingine vya aina hiyo. Wao walitaka kuona ugali waliyozoea kula kwao. Ugali ya wimbi, mawele au mtama. Nyama ya kuku wa kienyeji, mboga za kienyeji na pengine maji ya mtoni. Walitarajia kupata vyakula vya kiasili lakini mambo yalikuwa tofauti kabisa. Wakabakia kuzubaa huku wakifuatana kama kondoo.

Hili lilikuwa funzo kuu kwao. Waliweza kutambua kuwa dunia ilikuwa na mengi kuliko utamaduni wao. Tanasha basi akabaki kuwatazama tu wakijionea ulimwengu ambao ulionekana kuwa mpya wakati huo. Alifahamu fika kuwa hawangeweza kupata chakula walichotaka. Kwa vile hakutaka watu watumie muda mwingi maana tulikuwa katika safari, akawaita wote na kusema, "Jameni ndugu zangu, ni vizuri sana kushikilia tamaduni na itikadi zetu, lakini tusisahau kuwa mabadiliko ni lazima. Unapoenda ulaya unaishi kama mlaya. Najua kwa sasa mmefahamu kuwa hakuna vyakula kama vile tumezoea huko nyumbani. Kwa vile hatutaki kutumia muda zaidi, nawasihi kwa leo tu, leo tule chakula cha mzungu. Pengine hata kitakuwa kitamu zaidi kuliko mnavyofikiria," akasema Tanasha huku akielekea kwenye hoteli iliyokuwa karibu. Akaingia na kuanza kula pamoja na watoto wake wawili.

Kweli, pasipo na budi hubidi. Tukafuatana kwa pamoja na kuingia katika mkahawa mmoja uliokuwa na wafanyakazi waliokuwa wakiwaita watu kwa umbali. Nilipoketi, Mabuti na Lewa wakaja kuketi karibu nami. Nikaagiza pilau kwa nyama mara moja kwani njaa ilikuwa imenizidia sana. Lewa aliposikia hivyo naye akachukua menyu na akaikagua kwa mshangao. Akaisoma kwa ghaibu. Akaagiza sharubati kubwa. Nilishangaa vile sharubati ingemshibisha lakini nikashindwa kumwuliza. Mabuti naye akaagiza 'Cocktail' kama ilivyokuwa imeandikwa kwenye menyu hiyo. Punde si punde, msichana mmoja akaja huku kabeba pilau na nyama na kisha akaiweka kwenye meza karibu na mimi. Alikuwa mrembo na

mwenye tabasabu usoni. Rangi yake nyeusi iliweza kuambatana sawa na mavazi yake meupe aliyovalia. Nywele zake za kubandika zilikuwa zimemlalia kwenye mabega na kupita hadi mgongoni. Kinyume na wahudumu wengine waliokuwa na vitabataa vichwani, huyu alionekana tofauti. Hakuwa kajifunga chochote kichwani, ilhali anatakiwa kujifunga kama ilivyo desturi ya wahudumu wa mikahawa na mahoteli. Nikashangaa. Alikuwa kavaa blauzi nyeusi iliyokuwa na vifungo vikubwa. Kifungo cha kwanza kutoka juu kilikuwa hakijafungwa. Cha pili kilikuwa kimefungwa sawasawa bali cha tatu kilionekana kuchoka na kazi yake na kufunguka. Alikuwa kajaliwa chuchu kubwa ambazo kifungo kile kilishindwa kustahamili. Basi kati ya kifungo cha pili na cha nne, kukawa wazi baada ya cha tatu kuchoka na kazi. Pengo hilo likasababisha mvutano kati ya chuchu zake mbili na kuapa kutoka nje, lakini hazingeweza kutoka kwani kanchiri ilimwokoa. Vikawa vita kati ya vifungo, kanchiri na chuchu zake. Kwenye upande wa kulia, niliweza kulitizama jina lake kwenye beji lilibandikwa kifuani. Saida likawa ndilo jina lake. Alipoona macho yangu yamekazwa sana kwenye kifua chake, akashtuka na kujingalia. Kwa mshangao akagundua kifungo kilichokuwa wazi na kukifunga kwa haraka.

Kwa bahati mbaya, matukio hayo yaliweza kushuhudiwa na meneja wake aliyekuwa akimwangalia kwa umbali. Nilipotazama upande wake nikaona mkazo wake wa macho kwa Saida haukuwa wa kawaida. Akalazimisha tabasabu usoni kisha akaelekea kwenye sehemu yake ya kuchukua pesa. Saida akajua mambo hayangependeza. Ghaidhi yake ingempata. Akatoka kwa haraka ili kuleta alichokuwa kaagizwa. Tukatazamana bila kusema lolote. Kila mmoja alikuwa kesha bebwa na fikra za mwanadada yule. Alitunata kama gundi kwa namna alivyokuwa kama sumaku. Zaidi, mwendo wake ulipendeza na alikuwa kabarikiwa na makalio makubwa yaliyoviringika vizuri. Akasababisha hisia kuamka. Naam, kama

wanavyosema, ukimwamsha simba aliyelala, utalala wewe. Kila mmoja akamtamani Saida.

Saida alirejea huku kabeba sharubati na 'cocktail' kuwapa Lewa na Mabuti mtawalia. Lewa na Mabuti walishangaa walipoona chakula walicholetewa. Lewa akamwambia Saida, "Hiki sio chakula. Sikujua kuwa sharubati itakuwa hiki ulicholeta. Rudisha hiki na uniletee chakula kama hiki.," alisema Lewa huku akiashiria kidole chake kwenye chakula changu. Mabuti naye alipoona kuwa kaletewa juisi, akamwambia, "Asante kwa hiki kinywaji. Tafadhali niletee pilau nyama zaidi." Saida akatoka pale na kisha akaleta vyakula jinsi walivyokuwa wameagiza.

Wakafurahi sana. Kisha tukakunywa maji. Kila mtu alisikika akisifu chakula kile. Kuna wale waliosema kuwa hata vyakula vyao vya nyumbani havikuwa na ladha kama hiyo. Naam, wakati huo, wafanyakazi wengine walikuwa wanatusubiri kurudi kwenye basi. Omwami akatupigia mbinja na kutuita kwa kuashiria. Tukamtafuta Saida ili kulipa deni la chakula lakini mhudumu mwingine akasema kuwa Saida alikuwa ametumwa nyumbani na afisa msimamizi kwa kuvalia namna isivyositahili kazini. Sote kukashangaa na kuangaliana. Lewa alisikika akiuliza, "Kwani mnataka wasichana kuvalia kama mabibi za watu? Hivyo wataonekana washamba na watakosa kutuvutia sisi wanaume. Saida ameivaaa…aaaa." Mhudumu yule akamtazama Lewa kwa butwaa bila kusema chochote. Tukatoa pesa na kulipa. Akatupea risiti kila mmoja, tukaelekea kwenye basi letu. Mawazo yangu yalikwama kwa Saida aliyefukuzwa siku ile kwa mavazi yake. "Ilikuwa kusudi ama ni bahati mbaya kapatikana? Kama ni kusudi basi tembe yake kameza leo hii." Nikajiwazia.

Tanasha alifurahi sana aliposikia kuwa walikubali chakula kipya. Akamwamuru Lewa kubadilisha mavazi yake yaliyokuwa machafu na yenye harufu mbaya. Hakuwa na nguo zozote alizobeba. Ajabu! Alilazimika kununua shati na bombo mpya. Kwa vile kila mfanyakazi

alikuwa tayari amepewa kiwango fulani cha pesa ya matumizi wakati wa safari, Lewa hakuwa na sababu yoyote ya kukosa kununua mavazi. Akaenda na kununua kisha akaingia kwenye sehemu ya kujisaidia akabadilisha. Sote tukaingia kwenye basi tukaendelea na safari yetu.

Mara hii, ndani ya basi kulikuwa na harufu ya kuvutia. Ingawa Lewa alikuwa amebadilisha mavazi, hiyo haingekuwa sababu tosha ya kutoweka kwa harufu ya mkojo, matapishi na pombe. Kumbe Tanasha alikuwa ameamuru basi lile lioshwe wakati tulipokuwa tunakula. Nikampongeza kwa jambo hilo. Wakati huu kila mmoja alionekana kujawa na furaha si haba. Kashiba, katulia na kuwa tayari kumalizia safari.

Lewa alikuwa tayari karejea katika hali yake halisi. Alikuwa anajifahamu kwa wakati huo. Pombe iliyompa uwezo bandia wa kupayuka ilikuwa imemwishia. Kumbe yeye ni mtu wa maneno machache tu. Alikuwa ametulia kitini mwake. Hana neno. Hakuna aliyeweza kuamini kuwa ni yeye. Gari lilikuwa limetawaliwa na ukimya mkubwa kama wa kaburi. Kilichokuwa kinasikika kwa wakati huu ni minong'ono ya watu pekee. Dakika zikaunga saa. Safari yetu ndefu haikuwa na budi kutimilika kwani hakuna refu lisilokuwa na mwisho. Safari yetu ya saa zaidi ya nane ilifikia kikomo. Tuliingia kwenye mji mkubwa wa Jibambe. Mji huu ulikuwa wa asili na jadi. Nao ni mji uliokuwa na mambo mengi ya kigeni na kitamaduni. Ulikuwa unajulikana kote nchini kwa asili ya mambo muhimu kwenye jamii ya kale na ya kisasa. Kanisa la kwanza la kigeni lilianzishwa hapa. Barabara zake zilikuwa shwari sana na za kupendeza. Mataa ya ulinzi yalifuatana kando ya baraste kuu kwa utaratibu mkubwa. Majengo yake yalikuwa ya taadhima kubwa, marefu na yenye miundo tofauti. Magofu ya kale na yaliyokuwa kwenye historia ya binadamu yalikuwa yanapatikana kwenye mji huu mkubwa. Kila wakati, watalii walikuwa wakimiminika kwa wingi

kuzuru mji huu ili kujionea mambo kwa macho yao wenyewe. Pengine hadithi walizokuwa wakipewa wakiwa mbali nao hazikuweza kuwapa taswira kamili ya mandhari yake. Zaidi ya hayo, mji huu ulikuwa umezungukwa na bahari iliyokuwa na sehemu nyingi za kujibarizi. Maji yalikuwa yakipwa na kuacha sehemu nzuri sana ya mchanga wa baharini. Watu waliweza kupata fursa ya kujibarizi na kupunga upepo kwa furaha kwenye ufukwe wa bahari hili kubwa. Uliposimama kwenye ufuo huu ungeweza kuona namna vyombo vya maji kama vile meli, mashua, na merikebu vilivyokuwa vikipita kwa ustadi mkubwa. Kando kando ya bahari kulijaa mashua na madau madogo madogo ya wavuvi na waogeleaji waliokuwa wakijitosa kwenye maji kwa shabaha ya kutafuta mawe ya thamani sana ili kuwauzia watalii. Zaidi, madau yale yalitumika kusafirisha mizigo na watu wachache waliokuwa na hamu ya kuona maji na utulivu wa bahari. Nikayapenda mandhari yale. Kilichonivutia zaidi ni kuona namna watalii wale walivyothamini vitu vya asili ya kitamaduni. Wengi walizuru kwa sababu ya kuvinunua. Baadhi ya vitu vilivyowavutia wageni ni vyakula vya kitamaduni, ala za kivita kama vile nyuta, mishale, mapanga ya kikale na mikuki. Mavazi yakupendeza yaliyotengenezwa kutokana na ngozi za wanyama kama chui, ng’ombe na wanyama wengine. Ngozi za majoka makubwa makubwa yaliyoishi zamani zilikuwa na mvuto wa kipekee kwa watalii.

Kwa sababu ya wingi wa kazi na hela kupatikana kwa urahisi, wenyeji wengi waliweza kuhamia kwenye mji huu ili kujikimu kimaisha. Aliyebahatika kuingia kwenye kazi hiyo alijiona kama hohehahe aliyelala akaamkia kuwa tajiri wa kutajika. Kulikuweko watu waliojitokeza kwa lengo la kutoa maonyesho kwa watalii kuhusu jinsi uganga unavyofanyika. Kuna wengine pia walikuwa wakiuza mitishamba kutoka kwa mizizi, maganda na majani ya miti tofauti tofauti. Tulipofika hapo tuliweza kushangazwa na jinsi watu walivyotumia vitu tulivyoona kuwa vya kawaida kujipatia pesa. Hapo

ndipo nilipofahamu kuwa lengo la kampuni ya Ujadi Mills kuwaleta wafanyakazi wake hapa lilikuwa kuwafunza mambo kama hayo zaidi ya kuwafanya wao kujibarizi.

Tulipofika tulipelekwa kwenye hoteli moja ya kifahari hapo mjini. Ingekuwa makazi yetu kwa siku tatu ambazo zingefuatia. Kila mmoja wetu aliweza kupewa chumba chake cha kulala. Wafanyakazi waliokuwa na watoto wachanga au waliotaka kukaa pamoja wakapewa vyumba vikubwa zaidi. Hakukuwa na kazi kama kupika chakula katika hoteli hiyo. Pale tuliishi raha mstarehe. Chakula kilikuwa kinaletwa na wafanyakazi, kuanzia kiamshakinywa, chamchana hadi chajio. Maisha yalionekana kuwa yenye raha isiyokuwa na kifani. Nikayatamani maisha kama yale. Maisha ambayo pesa iliongea kwa namna yake. Maisha ya kufanya lolote bila ya kuhofia gharama yake. Hayo ndiyo yaliyopaswa kuwa maisha ya mtu aliyekuwa amesoma hadi chuo kikuu kama mimi. Niliweza kukumbuka maneno ya mhadhiri wangu katika chuo kikuu aliyekuwa na uraibu wa kujigamba na kujishaua kila wakati kutokana na mali yake. Alikuwa akisema kuwa elimu inaleta pesa, mali, magari na manyumba makubwa. Pesa inaleta uhalisia wa maisha. Kuishi kama mfalme ni chaguo na vilevile kuishi kama maskini ni chaguo maishani. Maneno hayo yalinikera hadi nikajiuliza namna kuishi kwangu kama maskini kulikuwa chaguo langu ilhali nilikuwa nimejitahidi kwa udi na uvumba kutafuta kazi.

Kilichonishangaza sana ni kusikia namna wazee wengine wachache walivyokuwa wakisema kando na ukarimu huo. Walikuwa wakisema maisha kama yale ni utumwa tu. Niliweza kumsikia Mzee Kitumbo akisema kuwa maisha kama yale hayakuwa na uhuru wowote. Uhuru wa kuamka kila asubuhi na kufanya waliyotaka. Hakukuwa na mashamba ambayo kama wanaume walipaswa kwenda kulima. Wao walipewa kazi ya kukaa ndani ya nyumba kama wanawake. Hakukuwa na mifugo wa kulisha wala kichaka cha kukata miti ya

ujenzi. Hapo ndipo niliweza kujua kuwa uhalisia wa kwetu ni mambo tuliyofanya kila siku. Namna tulivyoyafanya na wakati na majira ya kufanya mambo hayo. Kubadilisha mawazo ya wazee waliokolea katika utamaduni lingekuwa jambo gumu sana na pengine lisilowezekana.

Siku ya kwanza ilikuwa imetengwa kwa minajili ya kuweza kupumzika baada ya safari ndefu ya mjini. Kwenye vyumba vyetu, wale wahudumu walikuwa na kibarua kigumu cha kuwaonyesha watu namna vifaa tofauti vinavyopaswa kutumika. Ushamba wetu ulikuwa mkubwa sana. Haidhuru! Hakuna aliyezaliwa akijua kila jambo. Watu waliingia kwenye vyumba vyao, wakaoga, wakala na kulala fo fo fo.

Nilipoingia kwenye chumba changu sikuweza kupata usingizi. Kutokana na uchovu wa safari nilihitaji kuoga kwanza. Nikaingia kwenye mkaragazo oga na kuoga bila haraka. Nilipotoka kwenye bafu nilipata chajio tayari kishawekwa kwenye meza ya sebule. Kilikuwa chakula kilichofaa jina chakula. Matunda ya kila aina yalikuwa yameletwa. Maji ya matunda yaliyokuwa baridi vizuri yalikuwa mezani. Nikatamani maisha kama yale kwenye aushi yangu. Wakati wa habari ulikuwa umewadia. Ikanibidi kuwasha runinga ili niweze kutazama habari na matukio ya siku ile. Hakukuwa na kitu kipya kwenye habari zile.

Wakati wa mapumziko kati ya habari, niliweza kuona tangazo kutoka kwa kampuni moja mashuhuri mjini. Tangazo hilo lilikuwa linawataka watu kutuma maombi yao ya kazi kama vile uelekezi wa watalii. Walipeana anwani ambayo watu walitakiwa watume barua za maombi ya kazi kwa muda wa majuma mawili yaliyofuatia. Nikaandika hiyo anwani kwenye kitabu changu ambacho nilikuwa nikibeba kila wakati nilipotembea kisha nikazima runinga yangu na kulala. Usingizi nao ukanibeba mzima mzima.

Katika usingizi wa siku hiyo niliweza kuota ndoto ya kushtua sana. Niliweza kumwona baba yangu mzazi wakiwa pamoja na marehemu mama yangu kwenye sehemu fulani ya nyumba yetu. Ilikuwa majira ya usiku wa manane. Jamii yetu ilitambua masaa yale kama ya mazindiko. Giza la kaniki lilikuwa limegumbika changu cha kulala. Nilikuwa nimelala kichalichali huku nimejifunika ngozi ya ng'ombe iliyokuwa kama blanketi. Usiku huo ulitawaliwa na mvua kubwa sana iliyonyesha.

Kulikuwa na ngurumo za radi huku umeme ukiwaka na kupitisha mwangaza hadi ndani ya chumba changu. Ghafla, niliweza kuona kitu kilichokuwa na mwangaza tofauti na wa umeme. Mwangaza huo ulipokaribia, niliona kiwiliwili cha mtu aliyejivika kilemba cheupe kwenye kichwa chake. Nilipomtazama kwa umakini niliweza kumfahamu. Alikuwa baba yangu mzazi. Nyuma yake alikuwa kafuatwa na mganga mmoja aliyekuwa mashuhuri sana wakati huo kisha marehemu mama yangu akamfuata nyuma. Sikuweza kujua namna walivyoingia ndani ya chumba changu pasi na fahamu zangu. Pengine waliingia kwa kunyatanyata.

Mganga huyo alikuwa amebeba jogoo aliyekuwa na manyoya mekundu na maji kidogo kwenye kibuyu alichoshika kwa mkono wa kushoto. Kibuyu hicho kilikuwa kimetengenezwa kutokana na tunda la mbuyu baada ya kokwa zake kutolewa. Maji yale hayakuwa ya kawaida, kwani yalikuwa ya rangi ya kijani kibichi. Wakasogea moja kwa moja hadi wakakaribia kitanda changu. Yule mganga akainama na kufungia uzi wa sufu kwenye mojawapo ya matendeguu ya kitanda changu. Alipoinuka aliweza kuweka matawi ya mti fulani uliokuwa na harufu mbaya sana kisha akamnyunyizia yule jogoo maji yale. Baadaye akachukua yule jogoo na kumshika miguuni kisha akaanza kunipepea kwa mabawa yake.

Kilichonishangaza ni kuwa, yule jogoo hakuweza kutoa sauti yoyote kama ilivyo tabia ya kuku. Kwa kipindi hicho mganga yule alipokuwa

akifanya hayo, baba na mama yangu walikuwa wamepiga magoti karibu na kitanda changu huku wameinamisha vichwa vyao chini. Hakuna aliyeweza kunitazama. Nilishtuka zaidi wakati yule mganga aliponikodolea macho ya gololi huku amenishika kinywa changu. Nikatoa usiahi mkubwa kisha sikuweza kuona mtu yeyote karibu na mimi. Nikashtuka kutoka kwenye jinamizi lile. Nikaamka. Moyo wangu ulikuwa unanipiga kwa mwendo wa kasi sana.

Ndoto hiyo iliweza kuashiria mambo mengi sana. Nikatambua kwa uhakika kuwa wazazi wangu walikuwa tayari wamenifunga kwenye tamaduni za kwetu. Nilijua kuwa ni lazima ningechukua hatua nyingine mara moja la sivyo singeweza kufanikiwa kutokana na elimu yangu ya chuo kikuu. Niliamini pia kuwa mungu ni mwenye nguvu zaidi kuliko miungu wale.  Ingawa nilikuwa mcha mungu kwa muda ambao nilikuwa katika chuo kikuu, nilikuwa nimetamaushwa na hali ya maisha ilivyokuwa kwa wakati huo. Nilikuwa nimegoma kusali kila juma hadi nikaanza kuwa na tashwishi na maombi yangu. Bali na hayo, sasa nilikuwa nimepata mwelekeo mpya. Niliamini tena. Niliamini kuwa mganga hakufaulu kufanya uchawi wake kwangu. Mbona basi akapiga mayowe kabla ya kumaliza shughli zake na kutoweka? Nikaamini kuwa maulana ana nguvu zaidi ya miungu. Wakati ulikuwa umewadia. Wakati na wasaa wa kujiami vilivyo ili kupambana na hasimu huyo. Mtazamo wangu ukabadilika na kuchukua mkondo mpya.

## SURA YA SITA

Siku iliyofuatia tulianza ziara yetu rasmi. Ziara ya kujua mambo ya kitamaduni ya maeneo mbalimbali ya mji wa Jibambe. Kwa muda ambao tungekuwa kwenye ziara yetu, tungezuru maeneo ya Kikoani, Mishekini, Tondora na Weriji. Hivyo ndivyo Tanasha alivyokuwa ametudokezea. Maeneo hayo yalikuwa na mambo muhimu ambayo tungejivunia kuyajua. Basi tukakusanyika asubuhi na mapema kwenye basi la kampuni ya Ujadi Mills. Wakati huu hatukuwa na mizigo kama ilivyokuwa wakati tulipokuwa tunakuja kwani tuliiacha kwenye vyumba vyetu vya malazi ya hoteli hiyo. Kila mtu alikuwa mwenye furaha iliyokuwa bayana kwenye nyuso zetu.

Mji huu ulikuwa na joto lisilo la kawaida. Watu walikuwa wakiloa jasho ingawa ilikuwa bado asubuhi. Jua lilionekana kutoka kwa hasira na upepo wa bahari kufukuza mawingu yasionekane tena. Miale yake ilikuwa na ghadhabu kuu ungedhania watu wa mji huu walikosea miungu wao. Mavazi mazito yangechangia kuloa jasho zaidi. Waliokuwa wenyeji wa mji huu walikuwa wamezoea joto. Kwao ilikuwa hali ya kawaida.

Kinyume na joto hili lililotawala mji huu, namna ya mavazi ya wafanyakazi wa Kampuni ya Ujadi Mills haikubadilika. Wanawake walikuwa wamejivika nguo zilizofunika miili yao yote kama ilivyokuwa desturi yao. Kichwani na kiunoni kulikuwa na kanga ya kujifunikia. Watu wa jamii yetu wanathamini mwanamke kujifunika kichwani hadi kwenye kisigino. Sio hali ya kawaida kwa mwanamke kukosa leso wala sio leso moja, mbili. Moja ya kichwani na nyingine ya kiunoni hadi miguuni pake. Ni lazima kama ibada kwani ishara yake ni heshima. Heshima kwa mumewe na wazazi wake. Tabia za wenyeji wa mji wa Jibambe zilikuwa tofauti kabisa na tabia za kijijini tulikokuwa tumetoka. Vijana wa kike hapa walikuwa wamevalia mavazi yaliyoacha wazi sehemu zao za mwili. Kuna wale waliokuwa wamevalia suruali zilizowabana mapajani kiasi cha kushuhudia kila

bonde na mlima kwenye miili yao. Baba yangu alikuwa kabeba lubenga ambalo alijivika na kumsitiri pakubwa kutokana na joto la mji mpya.

Omwami akaketi kwenye usukani na kutuelekeza Kikoani. Hapa tulikuwa tumeletwa kwa minajili ya kuogelea. Sehemu hii ilikuwa imejaa watalii wengi. Kuna wale waliokuwa na asili ya kihindi na wengine asili ya Uingereza. Wapo waliotoka kwenye nchi ya ureno na wengine kutoka Uswisi. Kuna wale waliotoka Uturuki na wengine kutoka Brazili. Vilevile, kulikuwa na waafrika waliokuwa wakifurahia maji ya bahari. Bahari nayo ilikuwa imejaa. Wanawake walikuwa wakitembea huku wamevaa bikini za rangi tofauti. Walikuwa nusu uchi. Tulipofika hapo na kushuka kutoka kwenye basi letu, watu walisimamisha shughuli zao na kututazama kwa mshangao. Walidhani tulipotea njia. Kwenye bahari wakati kama huo hakuna mtu anayevaa kama sisi. Walishangazwa na namna tulivyokuwa tumevalia. Katika joto kama lile nani angevalia mavazi yaliyofunika mwili mzima? Nani angeweza kuogelea kwa suruali ndefu? Nilihisi kuwa mavazi yetu yalitusaliti. Uhalisia wetu uliweza kutambuliwa mara moja. Tulionekana washamba wasiojua namna ya kwenda na wakati na majira. Hata hivyo, pilipili usio ila haipaswi kukuwasha hata kidogo. Baada ya mduwazo wa dakika kadhaa, kila mtu aliendelea na kazi yake. Wakatuita bene, ila haikutudhuru kwa vyovyote vile.

Kwenye hali kama ile, wafanyakazi wa kampuni ya Ujadi Mills waliona ni kama kuasi tamaduni zao. Itakuwaje mtu kama baba yangu kuvua nguo mbele ya watu ambao ni rika ya watoto wake kwa minajili ya kuogelea? Kanuni za mila zinazopeana mikakati na mpangilio wa mambo ziko wapi? Waliokuwa wakifanya mambo kama hayo walikuwa wametoka kwenye jamii gani? Hayo yalikuwa baadhi ya maswali ambayo kila mmoja wetu alikuwa akijiuliza. Ulikuwa mwiko kuona sehemu fulani za mwili wa mtu mzima katika

jamii yetu. Sehemu kama vile kifua, mapaja, mgongo, makalio yalioachwa wazi, chuchu au sehemu yoyote ile inayopaswa kuwa fiche. Baadhi ya wafanyakazi tuliokuwa tumesafiri nao walibaki wamezubaa, karibu na basi wasijue la kufanya. Hakuna aliyetaka kuwatazama waliokuwa wakiogelea. Kulingana na takwimu za kikwetu, idadi kubwa ya wanaume huogelea kwenye mito peke yao. Hakukuwa na mwingiliano kati ya wanawake na wanaume hata wa marika tofauti. Watu wengi walibaki kujiuliza maswali yasiyo na majibu. Kwani Tanasha alituleta huku mjini ili kuasi tamaduni zetu? Mbona akatuleta hapa ilhali anajua tamaduni na itikadi za kwenye tumetoka? Maswali yakawa mengi bila majibu.

Wakati huo Tanasha alishuka na watoto wake wawili, wakaelekea kwenye chumba cha kubadilisha mavazi na kwenda moja kwa moja kuogelea. Alifahamu kuwa lazima ushamba wa tamaduni uondolewe kutoka kwa akili za wafanyakazi wale. Alikuwa kasema kuwa aliyetaka kuogelea angefanya hivyo wala sio lazima. Ilikuwa hiari. Hiari ya nafsi kuchagua kuasi mambo yaliyokuwa kama miiko isiyokuwa na faida yoyote. Fursa ya kuweza kufahamu mambo ya kunatia na mengine ya kukubali.

Kweli, uhalisia una nguvu. Utamaduni una uwezo mkubwa kuliko binadamu mmoja. Mila ni nyororo thabiti na imara kama mwamba. Nyororo inayohitaji nguvu kubwa zaidi kama utafaulu kuivunja. Nguvu kushinda kitu chochote kile. Wengi walipigwa na butwaa kubwa na kurudi ndani ya basi kutulia pale au labda kulala wasione yaliyokuwa yakiendelea. Lewa hakuweza kuwaangalia wenzake wakirudi kwenye basi kulala. Akasema, "Kwani ni lini nyinyi mtajua kuwa hakuna manufaa ya kuiga tamaduni kandamizi? Wale wazungu wanaogelea na familia yao kwa furaha. Tanasha vilevile ashazoea kufanya mambo haya na hakuna chochote ambacho amekosa. Hajapungukiwa hata kidogo. Yafaa tujue kuwa kutofanya mambo mengine ni kujinyima raha. Tumejifunga sisi wenyewe. Mimi

nilikuwa tayari nishajipanga kupiga mbizi kwenye bahari. Tayari nilijibebea bombo yangu ya kuogelea. Namfuata Tanasha." Alisema huku akitembea kuelekea kwenye bahari kwa madaha kama kuwashauri wengine wamfuate.

Lewa alikuwa ameshawahi ishi kwenye mji huu katika miaka yake ya ujana. Kumbukumbu zake wakati tulipokuwa tukisafiri zilikuwa mbali. Alikuwa amelewa chakari. Mabuti alipoona kuwa rafiki yake Lewa ameshakata kauli ya kwenda kuogelea, naye alikuwa kama bendera kufuata upepo. Akaelekea hadi kwenye chumba cha kubadilisha nguo na kisha kwenda kuogelea. Wale wengine kama baba yangu alienda zake kutazama mawimbi ya bahari kwenye sehemu tofauti mbali na sehemu ya kuogelea. Alithamini sana utulivu na ukimya. Angepata muda murua kabisa wa kuweza kufikiria yaliyokuwa yanamsibu. Akaelekea kwenye ntimbi na kukalia jiwe moja lililokuwa kaachwa wazi baada ya maji kupwa. Wakati wa nkindiza hiyo, mengi yaliibuliwa. Miguu yake iliyokuwa tupu, bila viatu ilizikwa kwenye mchanga uliokuwa na unyevu. Takataka za kila aina ziliweza kuonekana kwa sasa, baada ya maji kuondoka. Kwenye taka zile, aliweza kumwona samaki mchanga. Naye alikuwa bado hajui kuogelea na alikuwa amekwama kwenye shimo dogo huku akipigania maisha yake yaliyokuwa hatarini. Angekawia pale kwa dakika moja zaidi, angekufa. Akamamania kuvuta pumzi iliyokuwa nadra. Pengine mama yake mzazi alikuwa hafahamu matuko na mawimbi ya maisha kwa samaki yule mdogo. Baba yangu akaona kuwa samaki yule alikuwa kwenye hali sawa na mimi. Alitaka kunisaidia ili kuwa na maisha mema lakini hangeweza. Basi akawa msamaria mwema. Akamchukua yule samaki kwa mkono wake na kumtupa kwenye maji mengi ya bahari. Akaogelea na kwenda zake. Kila mmoja akapata fursa ya kumeza tembe yake. Chungu au tamu kwa pamoja. Ridhaa ya nafsi kuchagua ikachukua mkondo wa matendo na fikra za kila mmoja wetu.

Siku iliyofuata tulienda maeneo ya Mishekini. Hapa hakukuwa na mambo ya kuogelea bali ilikuwa sehemu ya mji ambayo ilikuwa chanzo na chimbuko la dini ya kikristo. Ilisemekana kuwa kanisa la kwanza la dini hiyo lilikuwa limejengwa humu. Kama tulivyohadithiwa na mwelekezi wa watalii pale, jengo hilo lilijulikana kama 'maadali'. 'Maadali' ya kwanza kabisa ilianzishwa na mgeni wa asili ya uingereza aliyetalii nchi yetu katika mwaka wa 1945. Shabaha yake hasa haikuwa kujenga 'maadali' bali ilikuwa kuzuru maeneo ya mji huu kwa likizo aliyokuwa nayo kutoka uingereza. Basi alipoelezewa namna watu wa sehemu hiyo walivyokuwa wakiishi, akaamua kutengeneza mahali pa kuabudia, kwa wachache ambao wangetaka. Alipojenga 'maadali' ile, alianza kwenda kuabudu kila jumapili huku akiandamana na familia yake pekee; mke na watoto wawili.

Wakazi wakaanza kuwa na wahaka na maabadi yake mapya. Wazee waliweza kutumwa kwake kumhoji kuhusiana na 'maadali' yake aliyojenga. Busara yao ikawaelekeza kushuku kuwa bwana yule alikuwa na lengo la kupotosha watu kwenye dini mpya. Hawakupendezwa na hatua ya mgeni huyo. Wakatafuta namna ya kufanya. Wazee wa kijiji walimtumia vitisho kuwa, kama hangeweza kuacha dini potofu na kuharibu 'maadali' yale wangemnyamazisha mara moja. Vuta nkuvute ikatokea. Vita kati ya utamaduni na dini vikazuka. Mwenyeji akapigana na mgeni. Mashindano ya miereka baina ya dini mpya na tamaduni za watu wa mji huo yakaanza huku watu wakitazama wakiwa na hanjamu kuu ya kujua nani angembwaga mwenzake. Wazee walikuwa wameshikilia ndi kwenye uamuzi wao wa kumtaka yule bwana arudi kwao mara moja. Bwana yule akawa kama duduvule ambalo haliachi mti hadi litoboe. Vitisho kutoka kwa wazee wa kijiji havikumfanya moyo wake kwenda kasi. Hakuwa na wasiwasi wowote kwani dhamira yake ilionekana kutimia. Alijua kuwa alihitaji muda wa kuwarai watu kadhaa kuja mwenye 'maadali' yake ili kuongeza idadi ya kondoo; wafuasi wake.

Akaanza na mzee mmoja aliyekuwa kafukuzwa kutoka kwenye kamati ya maandalizi ya matambiko. Sababu zake kufukuzwa ni kwamba alikuwa ameifanyia familia yake madhila yasiokuwa na kifani. Mzee yule alijulikana kama Kokoto.

Kokoto alikuwa mwenye roho mbaya sana. Aila yake ilikuwa yenye raha na amani kutoka wakati alipofunga ndoa na bibi yake aliyekuwa bikira wakati huo. Wakaishi kwa miaka kumi na kujaliwa watoto watano. Wavulana wanne na msichana mmoja. Wakati huo ndipo alipochaguliwa na wazee wa kamati ya mazindiko kuwa mmoja wao kwani alikuwa ametimiza kanuni za kuwa mwanakamati. Wazee wale walikuwa na kanuni zilizotumiwa kumsajili yeyote aliyepaniwa kujiunga nao. Lazima mwanamume awe na familia iliyoimarika yenye mke na watoto. Asiwe na doa lolote katika maisha yake kuhusiana na tabia zake kama vile kesi katika mahakama ya wazee wa kijiji. Awe amepitia jando na aliyetairiwa mara mbili kama ishara ya kutimiza kiwango cha miaka iliyohitajika na zaidi kuonyesha kuwa ni mtu aliyejua tamaduni na desturi kwa kina. Kokoto alikuwa amefikia na kuhitimu kwenye mambo hayo yote. Akachaguliwa.

Mambo yaliendelea vizuri kwenye miaka miwili ya kwanza kama mwanakamati wa wazee wa mazindiko. Katika mwaka wake wa tatu, mambo yakaanza kwenda segemnege. Muda wake mwingi alikuwa akiutumia kwenye vikao vya wazee. Hakuwa na muda wa kutosha wa kutumia na familia yake hasa mke wake aliyekuwa akimchunga kama mbuzi malishoni. Akapata fununu kuwa bibi yake alionekana na mwanamume mwingine aliyekuwa hasidi wake wa jadi. Naye alikuwa akimmezea mate bibi yake. Basi alipopata nafasi ya kuwa karibu naye wakati bwana yake alipokuwa kwenye vikao vya kamati, akautumia muda huo kumshawishi ampe haki aliyonyimwa kwa miaka mingi. Paka alipoondoka panya akatawala. Akaiparamia haki ile kwa ulafi kama sio uroho. Kibuyu hiki kikawa na asali iliyopiku utamu wa asali yake ya nyumbani. Akawa mchovya asali asiyefanya

mara moja. Wawili wale, kwa hiari wakameza tembe zao kwa pamoja huku Kokoto akila kokoto. Balaa!

Kokoto naye kwa ujanja wake akatuma wapelelezi kuhusiana na tetesi hizo. Kijana aliyetumwa alikuwa mwenye busara kubwa sana. Akapeleleza hadi akapata ukweli wa mambo. Akangoja wakati murua walipokuwa kwenye nyumba ya bwana yule kisha akamwarifu Kokoto. Kokoto naye alikuja mara moja na kuwafumania bibi yake na bwana yule. Hasira ya mkizi ikampanda na kumshauri awamalize wote kwa kutumia panga lake lililokuwa na makali kuwili. Akaingia kwenye nyumba yake kwa kunyatia hadi kwenye chumba cha malazi. Sauti iliyotoka mle chumbani iliashiria raha isiyokuwa na kifani. Kazi ilikuwa imetimilika. Bwana yule alikuwa kalipisha kisasi chake bila vita bali makubaliono baina yake na bibiye Kokoto. Naam, akasimama kwa muda huku akitaka kuhakiki kuwa haikuwa ndoto. Akadhibitisha. Akaweka panga lake tayari kumshambulia mwindaji wa mke wake. Wakati alipokuwa kaduwaa huku akiwaza la kufanya, alisikia sauti kubwa kutoka nje ya chumba hiki. Sauti ya kupasua masikio. Sauti hiyo iliwashtua wazinzi na kuwafanya kukatiza raha yao kwa ghafla. Bwana yule akadondoka kama makanga wa matwana za mjini bila kujali mavazi yake. Alijua kuwa kanaswa kwenye mtego wa Kokoto, hivyo lazima angefanya jambo kunusuru maisha yake. Kokoto alikuwa amegeuzwa na mlio huo akasahau alikuwa mawindoni. Alikuwa ameduwaa akitaka kujua nini kilichokuwa kinafanyika huko nje wakati alipopigwa kwa nguvu kwenye kisogo. Pigo hilo la kifaa mbutu lilimwangusha chini na kumwacha akijigaagaa sakafuni. Windo lake likatokomea kwenye kichaka na kumwacha kwenye maumivu makubwa. Uhasama ukajengeka kati yake, bibi yake na bwana yule.

Kokoto akahapa kumfunza bibi yake somo. Akamtesa kwa kichapo cha mbwa. Akazembea kwenye majukumu yake kama kiongozi wa jamii yake. Kweli, fahali wawili wanapopigana, nyasi ndio huumia.

Watoto wao wakawa nyasi. Wakakosa mavazi na chakula. Inasemekana kuwa kitindamimba wao alipatwa na ugonjwa wa unyafuzi kwa ukosefu wa lishe bora. Maisha ya aila hii yakachukua mwelekeo mwingine. Wakawa kicheko kwa jamii. Matukio hayo ndiyo yaliyosababisha yeye kufukuzwa kutoka kwa kamati ya mazindiko. Mzee yule wa kigeni alipomwendea kwa madhumuni ya kumrai, aliweza kumpata kwa urahisi sana.

Sasa mambo yakawa kwenye mteremko. Muingereza akapata msaidizi mmoja ambaye kwake alikuwa kama halaiki. Akaanza kumfunza jinsi ya kutekeleza ibada. Haikuwachukua muda mrefu kabla ya familia yake kujiunga na dini mpya. Idadi ya wafuasi ikaanza kuongezeka kila juma. Kutokana na mambo waliyokuwa wakishuudia wakazi wa eneo hilo, walianza kuamini dini hii mpya. Mgeni yule pamoja na mzee wake na familia zao wakawarai watu zaidi na kanisa lao likajaa. Kulikuwa na matendo ya miujiza na kuombea wale waliokuwa na mahitaji tofauti. Kwenye hali ya ulitima kama hii, kuna yeyote aliyekosa mahitaji? Kila mtu aliweza kuamini kuwa kulikuwa na ukweli kwenye dini mpya. Imani yao hiyo ikarahisisha mambo na waliweza kupata majibu kwa mahitaji yao. Wazee wa maabadi wakashindwa na mwingereza. Wakakata tamaa. Hivyo ndivyo dini mpya ilivyoanza hapa nchini mwetu.

# SURA YA SABA

Siku zilivyozidi kusonga, ndivyo matumaini yangu ya kumpata binamu yangu Taru yalivyodidimia. Taru alikuwa kijana niliyempenda sana kutokana na juhudi zake masomoni. Aliwahi kuwa wa kwanza katika taifa nzima kwenye mtihani wa kitaifa na ambao pia ulikuwa wa mwisho wa darasa la saba. Taru alikuwa mpenda raha. Watu walimpa jina la utani; Msanii kutokana na mtindo wake wa mavazi. Alikuwa njorinjori. Kaptura yake ingeweza kuwa suruali ndefu kama ingevaliwa na mtu wa urefu wa wastani. Naye alikuwa na uraibu wa kuvaa suruali zilizobana mwili wake. Aidha, mashati yake yalikuwa yenye michoro ya wanawake waliobobea katika sanaa ya uimbaji. Aliona fahari kubwa sana kuhusishwa nao kwani ndoto yake ilikuwa kuwa mwimbaji wa nyimbo za 'reggae'. Angesuka nywele zake na kuzilainisha vizuri. Viatu vyake vilikuwa havipatikani mashambani ila tu katika miji mikubwa mikubwa. Ndio maana basi akaamua kuja kuishi humu mjini. Hata hivyo, maisha ya mjini hayakuweza kumbadilisha hata kidogo. Alibaki yule yule Taru mwenye bidii za mchwa katika mambo aliyofanya. Nilipoulizia mahali alipokuwa akiishi, niliambiwa kuwa alikuwa akiishi mtaa uliojulikana kama Tuzame. Watu nyumbani walijua Tuzame kwa kutajwa tu ila hakuna hata jamaa wao mmoja aliyekuwa amefika kwake. Nilipoulizia kuhusu mtu kwa jina Taru Kembu kama alivyojulikana kwa majina yake rasmi, niliambiwa hakuna mtu kwa jina hilo aliyewahi ishi kwenye mtaa huo. Watu niliokutana nao walikuwa wakinitajia watu wengine ambao nilihisi kuwa sio Taru Kembu niliyekuwa nikimtafuta.

Matukio ya kumkosa binamu yangu sawa na ndoto ya usiku wa kwanza kwenye mji huu yalinivunja moyo zaidi. Nilimkumbuka marehemu mama yangu na kujawa na huzuni kubwa sana moyoni.

Mbona aliaga dunia kabla ya kunifungua kutokana na uwezo wa uganga na utamaduni? Nilihisi kama pingu zilizokuwa zimenifunga zilikuwa tayari zimepotea na kifo cha mama yangu. Funguo zake zikaenda na mwendazake. Kama kungelikuwa na kipuri, basi aliyejua na kufahamu kilipokuwa angekuwa sio mwingine ila baba yangu. Nikaamini kuwa, kifo cha mama yangu kilisababishwa na miungu. Walikuwa wanalipiza kisasi kwa kuwa sikuweza kufuata mikakati ya utamaduni. Nilikuwa nimeasi kidogo na kuungana na dini ya kigeni. Mama yangu alipatana na kifo chake wakati alipoenda kupiga ramli kwa minajili ya kumwangamiza jirani yake aliyetaka kunyakua sehemu yetu ya ardhi. Sehemu hiyo ilikuwa mali ya umma na hakuna aliyejua nani aliyekuwa mmiliki halisi wa ardhi hiyo. Baba yangu vilevile alitaka sehemu hiyo ya ardhi kwa vyovyote vile. Basi alipoona kuwa upinzani kati yake na jirani yule ulikuwa umeanza kukita mizizi ya chuki na uhasama, akamwamuru maskini mama yangu kwenda kumwona mchawi. Basi mama yangu hakuwa na budi kufanya kama alivyoshauriwa. Hakuna mwanamke aliyeweza kumjibu bwana yake ila kufuata maagizo moja kwa moja. Wakati alipofika, mchawi yule alimpa maagizo fulani ambayo alitakiwa kufuata kwa utaratibu pasipo na kukosea. Inasemekana kuwa, mchawi yule alimtaka mama kufanya jambo gumu sana na la kutamausha. Alitakiwa kupeana kafara ya mwanambee wake la sivyo yeye angekufa! Kifunguamimba huyo akawa ni uhai wangu.

Basi mama yangu hangeweza kufanya hivyo. Uhai wa kifunguamimba wake; mimi, ulikuwa muhimu sana kushinda sehemu hiyo ya ardhi. Hakuweza katu. Akakataa katakata. Jambo kama hilo huwa lenye kusababisha ghadhabu kubwa sana kwa miungu. Maskini mama yangu hakuweza kuepuka kifo. Baada ya siku saba, alipoonekana kuwa alikataa matakwa ya mchawi yule, usiku huo alipigwa na radi akafa. Baba yangu akabaki mwenye majuto mengi

sana lakini alijua kuwa hayo yote aliyasababishwa yeye mwenyewe. Akaimeza tembe yake ya kumpoteza bibi yake huku mama mzazi akimeza yake ya kufanya uamuzi wa kutonidhuru.

Habari za kifo cha mama yangu zilienea kwa haraka sana kama moto kwenye nyika. Watu walimtaja mama yangu kuwa mchawi kwani walijua sababu za kifo chake. Mchawi alikuwa mtu wa kufukuzwa kwenye jamii yetu. Wakasema kuwa mama yangu kalaaniwa hadi ahera. Fikra za mchawi zilikuwa za kuharibu, kuangamiza au kuua. Jirani yule naye alipofahamu matukio yale ya mama yangu akaapa kulipiza kisasi kwa namna yake.

Kutajika na kujulikana kama mchawi kwa mama yangu kuliweza kuwazuia watu wengi kuhudhuria mazishi yake. Jambo hilo lilinikera sana. Nikafahamu kwamba kulikuwa na mauti katika kuiga na pia kuasi miungu wa kwetu. Miiko ipo katika utamaduni. Mtu yeyote anayeenda kinyume na matarajio ya jamii yetu lazima mazao ya uasi yaonekane. Furaha uwepo wakati tunamzika mzee aliyekula miaka yake yote na asiye na hulka mbaya wala sio kwa aliyeishi na kufa akiwa bado mchanga. Wazee waliweza kuishi hadi uzulufu ukaingia na wasifahamu lolote. Mazishi yao huwa yenye nyemi wala sio nyende. Furaha ya kipekee.

Basi ikawa nilikuwa tayari nishaandika barua ya kutafuta kazi iliyotangazwa kwenye runinga siku ya kwanza ya safari yangu ya mjini. Baada ya kuandika nikatuma kupitia barua pepe kama yalivyokuwa maazigo yake. Ingawa niliandika barua hiyo, sikuwa na chembe ya matumaini kwamba ningeweza kupata kazi hiyo. Wakati huo tulikuwa tayari tumerejea nyumbani kutoka safari yetu. Nilikuwa nimemaliza majuma mawili kwenye hospitali huku nimeugua ugonjwa usijulikana. Baba yangu naye aliamini kuwa matibabu ya kienyeji yangeweza kunisaidia pakubwa ikilinganishwa na ya kigeni.

Mawazo yake yote yalikuwa kwenye waganga wa kienyeji. Nilivunjika moyo zaidi aliponisihi niende kwa mganga yule yule aliyesababisha kifo cha mama yangu kwa minajili ya kupata matibabu. Nikakataa katakata. Nikakata kauli kwenda kwenye hospitali ya serikali iliyokuwa takriban kilomita mia mbili kutoka nyumbani kwetu.

Baada ya kupimwa na madaktari, hawakuweza kupata ugonjwa wowote ingawa nilikuwa mwenye maumivu sana. Nilijihisi mnyonge sana. Wakanishauri nilazwe hapo kwa majuma mawili wakinichunguza. Baada ya hayo majuma, niliweza kupata afueni na kuruhusiwa kurudi nyumbani. Wakati nilipokuwa nikirejea nyumbani, nikaamua kupitia kwenye posta ili kuangalia kama pengine kungekuwa na ujumbe wowote ulionihusu. Nikatembea hadi posta. Nilipofika hapo nilibahatika kupata kibarua kilichokuwa kimeandikwa jina langu juu kwenye bahasha. Lakini hilo halikuwa jina langu halisi. Ni kweli kwamba jina la kwanza lilikuwa langu lakini jina la pili halikuwa langu ila anwani ilikuwa yangu. Watu ni wengi na pengine kulikuwa na mtu mwenye majina kama hayo. Nilipatwa na wasiwasi mkubwa lakini nikaambiwa kuwa ile barua ilikuwa imelimatia pale kwa muda wa majuma matatu hivyo niichukue. Nikafanya hivyo.

Nikakichukua na kukifungua huku shauku kubwa ikionekana usoni mwangu, kisha nikaanza kusoma. Kilikuwa kimeandikwa,

*Kampuni ya Kigeni na Kikwetu,*

*S.L.P 200-013,*

*Zama, Malini.*

*Tarehe: 01.01.2016*

*Kwa Kazamoyo Wema,*

*S.L.P 008-912,*

*Weusisi, Hesabika.*

*KUH: NAFASI YA KAZI*

*Ujumbe huu ni kukujulisha kwamba tulipokea barua yako ya kuomba kazi na kampuni ya Kigeni na Kikwetu. Tungependa kukufahamisha kuwa, kiwango chako cha elimu kiko juu sana na kimetufurahisha na zaidi kuturidhisha. Hivyo basi tumekupa nafasi ya kwanza ya kazi mara moja. Unatakikana kuja kazini tarehe 14.01.2016. Mshahara wako tuliokupangia utakufurahisha. Kumbuka kuwa usipofika kazini siku ambayo tumekuita nafasi yako itachukuliwa na mtu mwingine.*

*Shukrani.*



*Matokeo Juma,*

*Rasilimali Watu,*

*Kigeni na Kikwetu.*

Nilishikwa na bumbuwazi na majuto niliposoma barua hiyo. Moyo wangu ukadinda kupiga kwa sekunde kadhaa. Nikaduwaa. Mawazo mengi na majuto yakanijaa kutokana na namna nilivyopoteza fursa ya kubadilisha maisha yangu. Nikaona kuwa tonge langu nimenyang'anywa mdomoni. Lakini nani kafanya hayo yote? Hakuna wa kulaumiwa. Sikujua kuwa barua ilikuwa imetumwa tayari. Nilikuwa tayari nimechelewa kufika kazini kwa zaidi ya mwezi mmoja. Nilijua kuwa nafasi yangu ilikuwa imeshapata mtu mwingine.

Hata hivyo sikukata tamaa. Niliamua kwenda hadi mjini kujua ukweli wa shauku yangu. Pengine wamehifadhi nafasi hiyo kwangu. Singeweza kuamini kuwa nimekosa kazi niliyokuwa nikitarajia kwa hamu kubwa. Kesho yake nikafunga safari ya kuelekea mjini Zama kujua ukweli halisi. Nikasafiri kwa basi la kwanza. Safari yangu nayo ikafana. Nikafika salama wasalmini. Nikaelekea kwenye ofisi za kampuni hiyo asubuhi na mapema kwani nilikuwa tayari nimeonyeshwa wakati wa safari na wafanyakazi wa Ujadi Mills. Nilipata ofisi zile zimefungwa. Hapo ndipo nilipofahamu kuwa nilifika kabla ya wakati halisi wa wafanyakazi kuingia kazini. Ilikuwa saa mbili kasorobo. Nikaketi kwenye kiti kilichokuwa karibu na mlango wa kuingia ofisini na kutulia kwa umakini huku nikisubiri.

Nikiwa nimeketi pale niliweza kufikiria namna nitakavyokuwa nikifanya kazi hii ya kwanza maishani mwangu. Namna nitakavyopata pesa nyingi na kujenga nyumba ya kifahari na pengine ninunue gari kama rafiki yangu Hamisi. Mawazo yale ya matumaini yalinifanya nitabasamu na kucheka peke yangu. Nikadhani mimi ndiye niliyekuwa na funguo za mlango uliokuwa mbele yangu. Nikafurahi sana. Tabasamu yangu ilipatana moja kwa moja na macho ya binti mmoja aliyekuwa akiingia pale. Kwa namna alivyokuwa amevalia niliweza kujua kuwa yeye ndiye aliyekuwa wa kufungua

mlango huo. Alikuwa amevalia viatu vya mchuchumio na sketi nadhifu iliyokuwa imepigwa pasi ikawa sambamba. Mkononi alibeba mkoba uliokuwa wenye ngozi ya kifahari na uliopambwa kwa uhodari mkubwa. Kamba za mkoba huo zilipita kutoka begani mwake kwenye mkono wake wa kulia na kuteremkia karibu na kwapa lake huku zikiacha nafasi katikati. Kwenye mkono wa kushoto, alikuwa kashikilia faili iliyokuwa na rangi ya manjano. Kiwikoni mwa mkono huo, alikuwa kavalia saa iliyokuwa ya kupendeza ajabu. Nywele yake ilikuwa ndefu na iliyokuwa imenyooka na kulala vizuri kutoka kichwani hadi mgongoni. Alikuwa amekata nyusi zake kisha kuzichora kwa weusi uliokuwa umekolea. Kope zake nazo zilikuwa zikimetameta kwa pamoja. Mdomoni alikuwa kapaka rangi iliyochukuana vizuri na mavazi yake. Alikuwa kama malaika.

Alipofika karibu nami aliniangalia kwa jicho la upekuzi na dharau. Macho yake makali yaliashiria kuwa hakunitaka pale kwani akufukuzaye hakwambii toka. Sikujua kwa nini. Nikaanza kushuku pengine ni kutokana na mavazi yangu. Kwangu, nilijiona nadhifu. Shati langu na suruali yangu ya kaki vilikuwa havina dosari yoyote ila vilikuwa vikubwa kwenye mwili wangu mdogo. Mavazi yangu yalinipwaya mwilini. Yalikuwa bwangabwanga. Kabla ya kufungua mlango alisita kisha akaniuliza, “Wewe ni nani?” “Naitwa Kazamoyo Juma,” nikajibu. Hilo ndilo lililokuwa jina langu la pili wala sio Mwema kama ilivyokuwa imeandikwa katika barua ya kazi. “Wataka nini hapa asubuhi hii tena mapema?” Akaniuliza yule binti. “Nimekuja hapa baada ya kupokea barua iliyoniita kazini kwa kampuni hii,” nikajibu kwa ujasiri mkubwa. “Oh, so you are Kazamoyo Mwema? Hiyo barua tulikutumia mwezi mmoja uliopita kama niko katika fikra zangu. Nafasi yako tayari tushaipea mtu mwingine. Umechelewa. Samahani,” binti yule alinijibu kisha kufungua mlango na kuingia.

Jibu hilo liliniumiza moyo sana. Likanikera. Majuto yakanijia moja kwa moja. Kwanini sikwenda kwenye posta mara moja? Lakini ningewezaje kwenda ilhali hata nilikuwa mgonjwa sijiwezi? Nikajihisi kama bonge la barafu. Nikakufa ganzi mwili mzima. Niliona maisha yangu kama meli iliyo baharini bila nahodha. Meli ambayo ingeweza kuzama au kwenda upande wowote katika bahari. Pengine mawimbi au dhoruba zozote zile zingeweza kuiangamiza. Maisha yangu yalikuwa kama yametiwa shubiri. Machungu kwa mambo niliyokuwa napitia. Sikuamini masikio yangu hadi pale nilipoamua kutoka mahali pale na kwenda popote nikitafuta kazi. Hatua nyingine ya kujiua ikanijia. Pengine ningejirusha baharini mara moja ningeepuka machungu ya dunia. Lakini nilikuwa na nafasi ya kuishi maisha mema. Singejiua.

Kwenye kwi kwi kwi za machozi nikajitoa kitini pole pole na kuanza hatua moja, mbili, tatu…kutoka nilipokuwa nimeketi. Mwili wangu haukuwa wangu tena. Maisha yalikuwa yamenitonesha kidonda ndungu na hata zaidi, fursa ya kazi nikaipoteza. Hatua kama nne kutoka pale, niliweza kumwona mwanamume wa umri wa makamo akiingia ofisi ile ile aliyoingia yule binti. Alikuwa mfupi kama nyundo na aliyekuwa amevaa suti iliyokuwa imenyooka kiwango cha kusimama peke yake kama ingesimamishwa. Akanitazama kwa umakini na mshangao mkubwa. Nikazidi kutembea kwani sikutaka kupatana na maswali yasiyo na matumaini tena. Baada ya hatua zingine kama mbili hivi, yule mwanamume aliweza kuniita. Ingawa hakuniita kwa jina langu, nilipotazama nyuma aliniashiria nirudi ndipo nikajua mimi ndiye niliyeitwa. Nikavuta machozi kwa utaratibu kisha nikageuka na kurudi hadi pale alipokuwa amesimama.

Akanishauri nimfuate. Nikamfuata hadi ofisini mwake. Tukaketi kwenye viti karibu na meza yake iliyokuwa na sanamu za wanyama

wa pori. Ukutani nako kulikuwa na michoro ya wanyama wa porini kama vile simba, ndovu, kifaru na tembo. Zaidi, kulikuwa na michoro ya vyakula mbalimbali vya kienyeji na picha za wazungu waliokuwa wakinunua bidhaa hizo. Mezani kulikuwa na tarakilishi na kitabu kikubwa cha rekodi. Bwana yule alivua koti lake na kuliweka nyuma ya kiti chake likawa limening'inia. Akasafisha koo yake kisha akaniuliza, "Mbona walia? Ni nini chanzo cha kilio chako?" Sauti yake hiyo ilikuwa yenye utu ikilinganishwa na sauti ya binti aliyenikuta nje ya ofisi hiyo mwanzoni. "Nimekuja hapa ili kujua kama nafasi yangu ya kazi niliyoitiwa bado ipo. Nilipofika binti mmoja akaniambia kuwa nafasi yangu ya kazi ilichukuliwa na mtu mwingine. Barua iliyoniita kazini nimeipokea jana tu na nafasi yenyewe iliniita mwezi mmoja uliopita," nikamweleza. "Binti yule amekwambia ukweli. Hapa ni kazini na lazima tuendeshe mambo sawa na vile yalivyopangwa. Lakini nimekuona nikakuhurumia sana. Pengine nikutafutie kazi ya kusafisha vyoo vya kampuni hii. Tayari tuna wafanyakazi wa kutosha lakini nitakupa hiyo kazi maana naona unaweza kuifanya vizuri zaidi. Sio kuosha vyoo peke yake. Ikibidi utakuwa unafyeka nyasi kama zitahitaji kufyekwa. Aidha, kusafisha mazingira ya kazini na uchafu lazima uondolewe. Uko tayari kufanya kazi kama hiyo?" Akaniuliza bwana yule. Moyo wangu uliruka. Kwa mara ya kwanza nimesikia neno kazi. Nikafurahi. Lakini kazi hii ni gumu tena ya chini kwa mtu wa elimu ya juu kama mimi. Nikawaza. Bwana yule alihitaji jibu. Nikamwambia, "Pengine uniambie pesa utakayokuwa ukinilipa. Kama itaniridhisha nitaifanya." Bwana yule alinikazia macho na kuniambia, "Malipo ni mia mbili kwa siku," akasema. Pesa hiyo ilikuwa kidogo sana ikilinganishwa na hali ya maisha ilivyokuwa. Zaidi ni hali yangu mjini. Sikuwa na mahali pa kukaa. Ningeanza wapi? "Sawa, ingawa pesa hiyo ni kidogo na sina mahali pa kuishi kwa sasa," nikamwambia. "Kwa sasa nitakupa chumba chako cha

kuishi. Utakapopata hela utaanza kujilipia mwenyewe. Sasa unaweza kwenda na kuanza kazi mara moja. Kuna mkubwa wako atakayekuelekeza mahali pa kazi na malazi," bwana yule akamaliza.

Nilijihisi kuwa mungu wangu kajibu maombi yangu. Nikamshukuru kwa utu wake na ukarimu kisha nikatoka ofisini mwake. Niliweza kupata mwanamume mmoja aliyekuwa mkubwa wangu. Akanionyesha chumba changu cha kulala ambacho kingekuwa makazi yangu kwa muda usiojulikana. Nikaanza kufanya kazi.

# SURA YA NANE

Kazi za kila siku kwenye kampuni hii zilikuwa zinachosha na kuniacha katika hali ya unyonge. Unyonge kutokana na uchovu na zaidi njaa iliyokuwa ikinila matumbo. Ingawa pesa niliyokuwa nikipata ilikuwa inatosha kwa chakula, singeweza kununua kitu kingine chochote. Maisha ya mkono mdomoni. Kama ningehitaji kununua kitu chochote kama vile nguo mpya au kiatu kipya, basi ingenibidi kukosa chakula kwa siku mbili ndiposa nitoshe pesa ya kununua. Niliona kuwa maisha hayo sio yale niliyotarajia. Nikaamua tu kuvumilia pengine zamu yangu ingefika na kupata ufanisi wa kipekee siku moja. Hiyo ndiyo iliyokuwa ndoto yangu ya kila siku. Kujinusuru kutokana na ulitima wa ukoo wetu. Kila wakati nilikuwa nikipata bezo kutoka kwa wafanyakazi wenzangu tuliokuwa tukiosha vyoo na kukata nyasi pamoja. Mmoja alijulikana kwa jina kama Kombo. Naye alikuwa mbumbumbu hajui moja kuunga moja ukapata mbili. Alikuwa hajawahi kuona mlango wa darasa hata siku moja. Kila siku angelalamikia hela kidogo tulizokuwa tukipata. Malalamishi yake na yangu yalikuwa sawa. Tofauti ni kuwa, yake aliyasema kwa sauti ila yangu yalipitia moyoni na akilini pasipo kuyasema kinywani. Tuliogelea kwenye bwawa sawa. Zaidi alikuwa akisema kuwa pesa ile haingetosha hata chakula chake. Kombo alikuwa akiishi pamoja na rafiki yake aliyeitwa Tumaini. Tumaini alikuwa kijana wa makamo lakini wa umri mdogo kuliko Kombo. Alikuwa amemaliza masomo yake ya darasa la saba. Ingawa alikuwa amepita mtihani wake vizuri, hangeweza kujiunga na shule ya upili kutokana na kiwango cha mapato cha wazazi wake. Wao walikuwa maskini hohehahe, wasiokuwa na mbele wala nyuma. Alipoona kuwa mambo nyumbani yamezidi, aliamua kukimbilia mjini kutafuta kazi yoyote. Hivyo ndivyo alivyojipata kwenye kampuni ya Kikwetu na Kigeni.

Muda kwa muda tungeweza kuongea na Tumaini na kunieleza jinsi alivyokuwa na matumaini ya kuendeleza masomo yake. Alikuwa na ndoto ya kuwa daktari. Tumaini alikuwa na kipawa cha uimbaji pia. Wakati wa jioni angeweza kutuimbia nyimbo zake za taarab alizokuwa akitunga kila siku. Nyimbo zile zilikuwa na ubunifu mkubwa sana na zilikuwa zinahusu maisha yake. Maisha yaliyotawaliwa na matukio ya kutisha sana na kuvunja moyo. Siku moja tulikuwa tumepumzika kwa kujilaza kwenye nyasi katika uwanja wa michezo uliokuwa karibu na kampuni hiyo. Kombo alikuwa ametoweka pindi tu baada ya kazi; kwenda kumwona mama yake aliyekuwa mgonjwa nyumbani. Alikuwa amenidokezea kuwa siku hiyo hangerudi kwa hivyo nilikuwa na ridhaa ya kulala kwenye chumba chao na Tumaini. Tukamuaga na kumwombea mama yake dua njema.

Tulipokuwa kwenye nyasi zile pale uwanjani, Tumaini aliniimbia wimbo. Wimbo huo uliimbwa,

*Mzazi wangu nakwimbia, kila neno kukutamkia,*

*Ingawa heri kanitakia, ufanisi kuniwazia,*

*Tamaduni kanifungia, elimu yangu kudidimia*

*Kwa sasa nina machungu, yakupoteza mwelekeo.*

*Kwenye mji nikatorokea, ndani yake nikatokomea,*

*Sina popote kuegemea, sina yeyote kutegemea,*

*Nahisi mmenikosea, ila mimi nawaombea*

*Mungu awajalie, yenu mawazo mgeuze*

*Uganga umewatawala, itikadi kutekeleza,*

*Mabinti mwawaoza, kwa wazee walozeeka,*

*Matambiko mmezama, mmekosa kuelewa*

*Masomo ndio ngome, na ufunguo maishani*

*Ndugu zangu mkakeketa, katika umri wa sita,*

*Kila siku mkiteta, tamaduni kufuata,*

*Faida gani mlopata, kwa kuiga yalopita,*

*Ningekuwa na uwezo, elimu wangepata*

*Natazamia siku yangu, yenye mola atajibu,*

*Dua yangu kuhitimu, ndoto yangu ya kutibu,*

*Mikosi kwa mizimu, kanipa kutonijibu,*

*Ila njia yangu ndefu, natafuta usalama*

Wakati alipokuwa akimaliza ubeti wa mwisho wa wimbo wake, tayari machozi yalikuwa yanamlengalenga. Nikamhurumia sana. Tumaini alihisi kuwa maisha ya utamaduni wa kwao yalimkosesha amani na furaha maishani. Wimbo wake uliweza kuibua hisia za machungu ya jamii yake. Nikamshauri aache kulia kwani hakuwa peke yake katika vita vya kuepuka tamaduni kandamizi. Nikamwambia kuwa hata

mimi nilikuwa kwenye masaibu hayo hayo tu na labda yangu yalikuwa makubwa kuliko yake. Ingawa sikuwa na uraibu wa kutoa hadithi ya maisha yangu kwa mtu yeyote, niliapa kumwelezea Tumaini, niliyokuwa nimepitia. Tumaini alionekana kujawa na ujasiri na akanihurumia zaidi baada ya kumpa hadithi yangu na vile masomo yangu ya chuo kikuu yalivyokuwa hayajanisaidia hadi wakati huo. Aliweza kuniambia kuwa kulikuwa na matumaini ya kupata kazi nzuri na kuishi maisha mazuri. Wakati huo giza lilikuwa karibu linaingia. Tukaelekea kwenye chumba chao na baada ya chajio tukalala.

Kila siku, urafiki kati yangu na Tumaini ulizidi kukua. Tukajipata tukitumia muda mwingi pamoja. Kombo alipoona kuwa Tumaini ameasi urafiki naye, akaamua kumfukuza kutoka kwa chumba chake. Tumaini hakujua namna angefanya. Hakuwa amemkosea wala kumdharau Kombo kwa vyovyote vile. Kwa kawaida mimi na Kombo hatukuwa na mkabala mzuri sana. Alikuwa akiongea maneno yakuvunja moyo wangu. Pengine ni kutokana na ujinga wa kuzaliwa. Basi ikabidi nimpokee Tumaini baada ya kufurushwa na Kombo. Tukaanza kuishi pamoja kwenye chumba changu nilichopewa na yule mkuu wa kampuni hiyo.

Tuliweza kuishi kwa furaha. Kila siku baada ya kazi, tungelala kuchelewa kwa sababu ya hadithi tulizokuwa tukitoleana. Maisha yakaanza kuwa na mwelekeo, maana safari yetu ilichukua mkondo mmoja. Chuki na upinzani ukazuka kati yetu wawili na Kombo. Basi siku moja akatupata tumetulia na Tumaini wakati wa mchana tukingoja kurudi kazini saa nane alasiri. Tuliamua hatuli chakula cha mchana maana tulitaka kuweka akiba ya kununua kitabu cha hadithi kwa muda wa mwezi mmoja. Kombo alipofika akasema, “Nyinyi sasa elimu yenu itawasaidia vipi? Ona vile mmekosa hata chakula na

midomo imewaparara na kukaukiana. Heri mimi ambaye sikusoma na bado mizimu ya kwetu inanitafutia kazi na chakula kila siku. Maskini nyinyi." Usemi wake huo ulinikera sana. Nikaelewa kuwa mcheza na tope haogopi kuchafuliwa. Kabla ya kumjibu, Tumaini alikuwa tayari kusema, "Watu wana dhamira tofauti maishani. Leo wewe ndio kujaliwa kesho ni zamu yangu. Hivyo ndivyo maisha yalivyo. Unahitaji watu wanaoweza kukusaidia kupanda ngazi ya maisha hadi kufikia kilele," akamalizia "Hilo ni lako. Mimi simhitaji yeyote. Nimejitosheleza," akasema Kombo. Ilinibidi nimjibu sasa. Maneno yake yalikuwa yamejaa kiburi. "Kombo, kila mtu anamhitaji yule mwingine. Hakuna mtu ambaye amejitosheleza. Hujasikia wahenga walisema kuwa aliyekupa wewe kiti ndiye aliyenipa mimi kumbi?" Nikamjibu. "Nyinyi mna ujinga mkubwa. Nitawaacha na upumbavu wenu wa kudhani elimu ya wahenga itawasaidia," akasema Kombo huku akiondoka na kwenda zake. Baada ya kuondoka, tukabaki tukicheka kwa kumkatiza kwa uungwana. Wakati wa kazi ulikuwa tayari umefika. Tukaelekea kazini tena.

Kombo akawa anatafuta jinsi ya kututenganisha na Tumaini. Alikuwa akijaribu kwa kila namna lakini hakuweza. Kumbe kuishi na mtu kwa muda mrefu kunakupa fursa ya kumjua na kumwelewa uhalisia wake. Tumaini hakuwa anamjua Kombo kama vile alivyojitokeza. Ilikuwa dhahiri shahiri kuwa Kombo alikuwa kama mbwamwitu aliyejivika ngozi ya kondoo. Hiyo haikuwa hali yake halisi. Alikuwa mwenye kiburi na kujishaua. Basi ikawa siku moja nilikuwa nimeitwa kuhojiwa kuhusiana na kazi niliyokuwa nimeandika barua kuiomba. Siku hiyo singefika kazini wakati wa asubuhi kama inavyostahili, hivyo basi tukakubaliana na Tumaini kwamba anifanyie kazi yangu ya asubuhi kisha ningekuja kuendelea wakati wa alasiri. Hatukutaka mkurugenzi mkuu kujua. Bora kazi ingefanywa ipasavyo nini tena

shida? Nikaenda kwenye mahojiano. Kombo aliweza kufahamu mpango wetu. Akaamua kunitenda.

Alipongoja siku hiyo nikakosa kuja wakati wa asubuhi, basi akajua mtego wake ulikuwa karibu kunasa nyama. Alifika kwa mkurugenzi mkuu; yule bwana aliyenipa kazi kwa siku ya kwanza. Akamwambia kuwa nilikuwa nimesusia kazi bila kufahamishana. Bwana yule alishangaa sana na akamwambia kuwa angetaka kuniona siku iliyofuatia. Kesho yake nikaitwa ofisini mara moja. Bwana yule alikuwa mwingi wa ghadhabu. Sikuwahi mtazama kwa umakini usoni mwake. Alikuwa na kovu kwenye uso wake ambalo lilikuwa linafanana na la binamu yangu Taru. Sikutilia hilo maanani maana nilikuwa na kubwa lililoniandama. Kutoka nianze kufanya kazi kwenye Kampuni hii, sikuwahi jua jina halisi la bwana huyu. Watu walikuwa wakimwita 'boss' wengine 'mkubwa' na wengine 'Meneja'.

"Wewe kijana uliamua kujiweka kwenye makaa ya moto, sio?" Hilo ndilo lililokuwa swali lake la kwanza. Likanishtua. Nikakosa jibu. "Hapana mkubwa, tulikuwa tumeagana na rafiki yangu Tumaini anisaide kwenye kazi ya asubuhi kisha nikirudi alasiri niendelee. Nilikuwa na jambo la dharura sana pia niliona jambo kama lile lilikuwa ndogo kiasi cha kutohitaji ufahamu wako. Nikarudi alasiri na hakuna jambo lililoharibika," nikamjibu. Jibu langu lilishangaza bwana yule. "Waonekana mahiri wa lugha na mwenye busara katika kujibu maswali. Majina yako kamili waitwa nani?" Akaniuliza. Mara hii niliweza kuona tabasabu usoni mwake. "Kwa majina naitwa Kazamoyo Juma," nikamjibu. Uso wake uling'aa mara moja. Sikujua ni kwa nini. Kwani alifahamu jina langu? Nikawaza. "Kazamoyo…kaza..Moyo. Unatoka wapi?" Akaniuliza bwana yule. "Nimetoka kaunti ya Hesabika mjini Weusisi," nikamjibu. Bwana yule aliruka kutoka kwenye kiti chake na kunikumbatia. Machozi

yalimdondoka. Alikuwa amenifahamu. Alikuwa binamu yangu Taru. Katika harakati hiyo niliweza kujiwa na fahamu zangu na kujua kuwa wakati wangu ulikuwa umewadia. Kumbe kutoka siku ile aliponipa kazi katika kampuni yake alikuwa hajanifahamu? Sadfa ilikuwa imetukutanisha. Akaita yule binti tuliyekutana siku yangu ya kwanza. Kumbe alikuwa katibu binafsi wa bwana Taru kama nilivyojua wakati huo. Taru akaagiza kinywaji mara moja. Tukaletewa soda. Kwa mara ya kwanza nilijihisi kuwa kama mfalme. Sikuweza kuamini niliyokuwa nikishuhudia. Kesi ya maovu niliyokuwa nimeitiwa iligeuka na kuwa chanzo cha upanzi wa ngazi katika maisha yangu. "Samahani kwa kukosa kukutambua mara moja wakati tulipokutana siku ya kwanza. Sikuweza kukutambua ingawa nilikuwa na tashwishi kidogo. Sura yako haikuonekana geni sana kwangu ila nilikuwa na shaka. Nilikuwa nimekusahau machoni maana hatujaonana tangu tulipokuwa watoto wadogo," akasema Taru.

"Hata mimi sikukufahamu mara ya kwanza bwana Taru. Nilikuwa nimekusahau machoni pia. Tangu tulipokuwa kwenye uwanja wa kitaifa kutunukiwa ushindi, sijawahi kukuona tena," nikamwambia. "Nilitaka kukuona pindi tu nilipopokea barua yako ya kuomba kazi. Ni wewe tu niliyekupa nafasi ya kwanza maana ulikuwa umehitimu kiwango kikubwa cha masomo. Pili, wewe ni binamu yangu na nakujua kwa bidii yako kwenye masomo," akasema Taru. "Asante. Nashukuru kwa sifa ulizonimiminia. Ni ukweli usiofichika. Bali niliipata barua yako mwezi mmoja baadaye lakini nikaamua kuja kuona kama bado naweza pata nafasi yangu. Kwani mja hupata ajaliwalo sio atakalo," nikamjibu Taru. "Sasa umefika ndugu yangu. Kama wasemavyo wahenga kuwa ndugu ni kufaana wala sio kufanana. Hiyo nafasi ya kazi bado nimeifadhi na nilikuwa nikingoja Kazamoyo Juma, binamu yangu na rafiki wa jadi," Taru akaniambia. Maneno yake yaliweza kunipa mwelekeo mpya wa mawazo.

Nikamkumbuka Kombo na majivuno yake ya kusema kuwa yeye hakuhitaji yeyote kupanda katika maisha. Nilifurahishwa na sadfa ya mambo ilivyochukuana kwa utaratibu. Nikaona upendo wa dhati na undugu wa kipekee.

"Kuanzia kesho utabadilisha maisha yako. Utakuwa mdogo wangu kazini. Mshahara wako utakuridhisha. Zaidi utapewa gari la kifahari la kampuni na nyumba ya kulala," akaniambia Taru. Sikuweza kujizuia kumkumbatia Taru. Machozi ya furaha yalinijaa machoni nisijizuie. Niliona kuwa mungu alikuwa mwishowe kajibu maombi yangu. Yule katibu binafsi wake alitupata huku tumekumbatiana. Hakuweza kuamini macho yake. Akashangaa ni jambo gani hilo lililotufanya kukumbatiana. Hakukawia pale. Akaondoka hata kabla ya kusema alilokusudia. Baadaye nikatoka hofisi mwake na kuelekea chumbani mwangu nikiwa na furaha tele.

# SURA YA TISA

Tumaini hakuweza kuamini kuwa siku iliyofuata ningekuwa kwenye ofisi yenye hadhi. Siku hiyo ndiyo ningehamia kwenye nyumba yangu ya kifahari. Ilikuwa imehifadhiwa tayari. Nilipofika kwenye chumba changu na kumweleza yaliyotokea, hakuamini niyomwambia. Alikuwa mwenye furaha gaya.. Akanikumbatia na kunipongeza. Nilikuwa kama maskini aliyelala akaamkia kuwa tajiri. Ndoto yangu ya jumla ya miaka thelathini ndio sasa nilianza kuona kama haikuwa budi kutimia. Nikamfikiria binamu yangu Taru. Nikakosa kuona namna ningemshukuru. Damu ni nzito kuliko maji. Hivyo ndivyo mila za kikwetu zilivyotufunza. Kuwasaidia ndugu zetu na kuwa na utu kila wakati. Huo ndio uliokuwa uhalisia wa kwetu. Wazee wa zamani walijua kuwa ndugu ana thamani kubwa zaidi kuliko kitu chochote kile. Huo ndio uliokuwa uhalisia kamili. Usiku huo sikuweza kulala kwani nilikuwa nangoja kuona mwanzo mpya wa maisha yangu. Ukweli wa mambo ukitendeka kama nilivyoambiwa na Bwana Taru.

Hayawi hayawi huwa. Siku niliyoingoja kwa hamu sana ikawadia. Sikujua namna ningetembea wala kuvalia. Nilikuwa na suruali yangu nyeusi na shati langu nyeupe. Hata ingawa sikuwa na tai kama wakubwa wengine, nilikuwa nimeng'aa kama mbalamwezi. Baada ya kuvalia, nikaelekea ofisini mwangu. Nilikuwa hatua chache kutoka chumbani mwangu nilipokutana na Kombo akija kuelekea chumbani mwetu. Kama ilivyokuwa kawaida yake ya kuongea hata kabla ya salamu akasema, "Wewe bwana kang'ara sana leo. Waenda kwenye mahojiano ya kazi tena ama kavaa hivi kwenda kusafisha vyoo?." Nilimwangalia kwa bezo na kumwambia, "Kazi nimeshajaliwa na maulana. Naenda ofisini." Kombo alibaki kazubaa na kujishika tama kama aliyefiwa. Hakuweza kuongea tena. Ndio sasa alikuwa

ameshajua kuwa nimekuwa mkubwa wake. Akaelekea kwenye chumba changu kumtafuta Tumaini pengine ampe ukweli wa maneno aliyosikia. Lakini Tumaini alikuwa kayafahamu hayo yote.

Nilipofika nilimkuta katibu wa Bwana Taru tayari keshafika. Aliponiona na zaidi kwenye mavazi niliyokuwa nimevaa akashangaa. Hakuweza kuyaamini macho yake. Labda aliponiona alidhani ni mgeni aliyekuja kumwona mkubwa wake. Siku iliyopita alikuwa ametukuta na Bwana Taru ofisini tumekumbatiana lakini hakuambiwa nini hasa kilichokuwa sababu ya tendo lile. "Habari ya asubuhi?" Nikamwamkua. "Njema. Waenda wapi leo naona umevaa tofauti na siku zingine?" Akaniuliza. "Siendi popote ila naja mumu humu ofisini. Kwa sasa mimi ni mdogo wa mkurugenzi mkuu!" Nikamjibu. Binti yule hakuweza kugeuka. Alikuwa kama aliyeganda. Alijua kuwa mambo kwake pengine yangeharibika. Namna alivyonitendea nilipokuwa mgeni wake ilimfanya kumaka. Alihisi kuwa wakati wake wa kupata matunda ya matendo yake ulikuwa umefika. Nikamwacha kwenye kiti chake na kuingia ofisini mara moja.

Ofisi ile ilikuwa tayari imeoshwa. Ilikuwa kubwa na yenye mapambo ya kuvutia machoni. Kulikuwa na vitu tofauti asili na vilivyoundwa kwa ustadi mkubwa. Kiti changu kilikuwa cha kuzunguka. Hapa ndipo nilipoona kuwa maisha yaliyokuwa hadithi yalikuwa ndio hayo. Nikaketi pale kwenye kiti bila kujua ningeanza kufanya nini. Nikaegemea kwenye kiti hicho. Nilimshukru maulana kwa zawadi ya kazi. Sikuweza kuamini kufungwa katika tamaduni tena. Mambo yalikuwa wazi kama mchana kuwa utamaduni ulikuwa umeshindwa. Uhalisia wangu ulikuwa umewadia. Ndoto yangu ilikuwa ndio sasa inatimilika.

Juma hilo la kwanza lilikuwa lina shughuli nyingi sana. Nilikuwa na Bwana Taru kila siku kunionyesha majukumu niliyotakiwa kufanya. Kazi yangu pale ilikuwa kuunganisha watalii na biashara yetu. Kutafuta namna kazi tuliyokuwa tukifanya kwenye kampuni itakavyojulikana kwa umbali iwezekanavyo. Zaidi, mimi ndiye niliyepewa usimamizi wa wafanyakazi wote waliokuwa chini yangu. Kazi ya kuajiri au kupiga kalamu mtu yeyote ilikuwa mikononi mwangu. Juma hilo pia niliweza kuhamia kwenye jumba langu mpya. Jumba lililokuwa na kila kitu nilichohitaji. Runinga kubwa ilikuwa sebuleni mwa jumba hili lenye vyumba vinane. Kulikuwa na vyumba vya wageni na kisha chumba changu cha kulala. Jumba hili lilikuwa na baraza kubwa na viti vya kutulia pale nje ukitazama jua likitua. Chakula kilikuwa na mpishi wake. Nguo zilikuwa na dobi wake. Kulikuwa na mfanyakazi wa kupiga deki. Mambo yakawa sawasawa. Kabla ya chochote kile, Bwana Taru aliweza kunipa kiwango cha pesa kilichonisaidia kununua mavazi mapya ya kazi. Sio tu ya kazi, bali mavazi nadhifu. Ingawa nilikuwa tayari mjuzi wa kuendesha gari, ilinichukua muda kidogo sana kwangu kuzoea kuendesha peke yangu. Dereva niliyepewa alikuwa mwenye umahiri na hodari wa kuendesha gari. Akanifunza vitu kadha wa kadha nilivyokuwa nimesahau.

Baada ya mwezi mmoja wa kufanya kazi kama mdogo wa meneja, niliweza kupokea mshahara wangu wa kwanza. Hiyo ilikuwa hela. Pesa ya mwezi kwenye nafasi hii ilikuwa mara elfu ikilinganishwa na malipo ya kazi ya kuosha vyoo. Maisha yangu yakachukua mwelekeo mpya. Kila mtu pale alikuwa amefahamu kuwa bahati yangu kanipata. Yule binti katibu akajua kuwa mola hamtupi mja wake. Kinyongo chake na chuki vikageuka kuwa upendo kwani hakuwa budi. Ingawa urafiki wangu na Kombo ulikatika mara moja, sikuweza kumtupa Tumaini. Nilihisi kuwa jukumu la kumwonyesha njia

lilikuwa juu yangu. Baada ya miezi tatu hivi, nilimshauri akajiunge na shule ya upili huku nikimlipia karo. Tumaini alifurahi sana aliposikia hayo. Akaitikia kwenda shule na kusoma ili kutimiza ndoto yake ya kuwa daktari. Nami nilimlipia karo yake yote. Akaacha kazi ya kuosha vyoo na kuwa mwanafunzi tena. Ilinibidi kumtembelea shuleni mara kwa mara kumjulia hali. Alikuwa amejiunga na shule moja ya kitaifa mjini kwa maana alikuwa ameupita mtihani wake vizuri sana. Kila wakati nilimshauri kutia bidii masomoni. Naye hakuniangusha hata kidogo. Nafasi yake ilikuwa namba moja wala sio mbili. Alikuwa mwanafunzi mwenye jitihada sana.

Niliamua kwenda nyumbani kwetu kumwona baba yangu na ndugu zangu wikendi moja. Sikuwa nimefika nyumbani tangu nilipokuja mjini baada ya kupata barua ya kazi iliyokuwa imeenita. Baba yangu alikuwa na wasiwasi mwingi kwani hatukuwa na njia mwafaka ya kuwasiliana. Hivyo basi, hakuweza kujua namna nilivyokuwa nikiishi mjini. Nina hakika kuwa alienda kwa waganga kunitafuta. Kama alipata jawabu mimi sijui. Kwenye gari langu nilikuwa nimebeba kila kitu. Sio matunda, sio nguo, sio chakula, sio simu za mkononi wala sio pesa. Nilifahamu kuwa nilikuwa na mzingo mwingine wa kuelimisha dada yangu na kaka yangu waliokuwa shuleni. Kama nimebahatika kupata pesa kwa nini nisiwasaidie ndugu zangu?

Safari yangu ilianza asubuhi na mapema. Sikutaka kwenda na dereva wangu kwetu nyumbani. Niliona nimpe fursa hii apumzike kabla ya juma la kazi kuanza. Nikamwacha kwenye nyumba yangu mjini. Safari yangu ilikuwa shwari sana. Nikafika mjini Weusisi salama. Watu wa mji huu walionijua walikuja kunisalimia. Hawakuweza kuamini mabadiliko ya maisha yangu. Wengi walidhani haikuwa mimi bali mzuka. Kwani watu wakienda mjini wanakuwa matajiri? Walibaki wameshangaa. Hakuna aliyekuwa na jibu la swali kama hilo.

Baada ya kukaa kwa kipindi cha nusu saa hivi, niliamua kuelekea nyumbani. Ingawa njia ya kuingia kijiji chetu ilikuwa mbaya, ilinibidi kuendesha gari langu kwa utaratibu na umakini mkubwa. Baada ya nusu saa nikafika kiamboni mwetu.

Nilipofika kwenye njia ya kuingia nyumbani, niliweza kumwona baba yangu nje ya nyumba yake kuu kuu iliyokuwa imeezekwa nyasi. Alikuwa amekalia kiti cha miguu mitatu huku akinolea panga lake. Sikuweza kumuona dada yangu wala kaka yangu. Nikapiga honi. Mara ya kwanza hakugeuka. Nikakaribia tena kisha nikapiga honi. Mara hii baba yangu alishtuka na alipoona gari tayari liko kwenye nyumba lake, akakimbia na kujificha kwenye chumba chake. Pengine alidhani ni polisi waliokuwa wamekuja kumkamata ingawa sikujua kwa kosa gani. Kaka yangu aliyekuwa akitoka malishoni alinifahamu baada ya kushusha kioo cha mlango wa gari. Alikuja karibu na gari langu huku akirukaruka. Baba yangu naye alipotuona tumekumbatiana na kaka yangu baada ya kutoka kwenye gari, alikuja pole pole kwa shauku kubwa. Akanisalimia kwa sauti ya unyonge. Hakuwa na furaha kama kaka yangu. Alishangaa nilikokuwa nimetoa gari la kifahari kama hilo. Zaidi ni pesa niliyokuwa nimebeba pamoja na vitu vya dhamana kubwa nilivyokuwa nimenunua. Nikamsihi kaka yangu kubeba vitu hivyo kutoka kwenye gari langu kisha tukaenda kwenye kivuli na baba yangu kuongea – Jua lilikuwa angavu na kali.

Kwenye kivuli cha mti mkubwa uliokuwa kwetu nyumbani tuliketi pamoja na baba yangu. Hadithi yangu ya vile nilivyopata na kukosa kwenye maisha ya mjini ilianza. Nikamsimulia namna nilivyokuwa mwosha vyoo kwenye kampuni ya Kikwetu na Kigeni. Nikamwadithia kuhusu marafiki zangu; Tumaini na Kombo. Hadithi yangu ya vile nilivyopatana na Taru Kembu; binamu yangu.

Hakuweza kuamini. Nikwamweleza vile Kombo alivyochangia kupata kazi kwangu. Nikamwambia kuwa mimi nilikuwa mkubwa na mwenye mshahara mkubwa na jumba la kujivunia. Zaidi nilikuwa na gari la kifahari. Baada ya kumweleza kuhusu rafiki yangu Tumaini na vile nimemsaidia kujiunga na shule ya upili kuendeleza masomo yake, baba alitokwa na machozi. Ilikuwa uchungu kuona machozi ya baba yangu. Sikujua ni nini hasa kilichosababisha machozi chake. Nikajipa kutotaka kujua.

Wakati huo, Kaka yangu alikuwa tayari ametoa vitu vyote vilivyokuwa kwenye gari. Akavileta tulipokuwa tumeketi na baba yangu. Nikampa baba mavazi yake yaliyokuwa yakupendeza sana. Ingawa nilidhani kuwa baba yangu angekataa kata kata kuchukua mavazi kama hayo, nilishangaa sana alipoyapokea kwa moyo mkunjufu. Kaka yangu naye alikuwa mwenye furaha sana kupokea mengi kutoka kwangu. Bali na hayo yote, sasa nilikuwa nataka dada yangu kuwekewa vitu ambavyo nilikuwa nimemletea. Nikauliza kaka yangu mahali alipokuwa dada yangu. Aliniangalia kwa macho ya huzuni. Akaniambia, "Dada yetu hayupo tena kwenye nyumba yetu. Ashaolewa majuma mawili yaliyopita." Nilimwangalia alipokuwa akisema maneno yale kisha nikamtazama baba machoni. Niliona kuwa baba  alikuwa amesaliti familia yake. Niliona tamaa ya utajiri ndani ya moyo wake. Akatazama chini kwa haya.

Furaha yangu ya siku ilikuwa imekatizwa ghafla. Nilimkumbuka maskini dada yangu na umri wake wa miaka tisa. Alikuwa kaozwa kwenye ndoa asiyoijua mwanzo wala mwisho wake. Nilipotazama kwenye nyumba yetu sikuona hata mali kutoka kwa ndoa yake. Hali ilikuwa vilevile nilivyoacha. Baba yangu alikuwa akibumbujikwa machozi muda huo wote. Nilipoulizia mwanamume aliyeozwa dada yangu niliambiwa alikuwa Bwana Tamaa. Kwa vile nilivyokuwa

nimemjua, Bwana Tamaa alikuwa wa takriban miaka sabini na saba. Alikuwa mzee aliyekuwa amekula chumvi si haba. Alikuwa na mabibi wanne na dada yangu aliozwa kama bibi wa tano. Alijulikana kwa kuwanyanyasa wake zake na kuwadhulumu sana. Watoto wake kwa jumla walikuwa thelathini na wawili. Uchungu wa kumpoteza dada yangu kwenye misingi ya utamaduni uliniparamia kama nyani anavyoparamia mti wa matunda. Sikuweza kuzuia machozi kutoka kwenye macho yangu. Nilitamani kumwona kaka yangu aliyeacha masomo yake katika kidato cha pili arudi shuleni. Kwa sasa nilikuwa na uwezo wa kuwasomesha hadi chuo kikuu kama mimi. Nilihitaji kufanya jambo mara moja.

Nilisimama mara moja na kumwamuru kaka yangu aingie kwenye gari. Nikalingurumisha gari na kumwacha baba yangu kwenye kivuli huku ameshangazwa na mwendo wangu. Hakujua mahali nilikokuwa naenda na kaka yangu ila alishuku tu. Kaka yangu alinielekeza hadi kwa Bwana Tamaa. Tulipofika nyumbani kwake, tulimpata yule mzee akivuta sigara yake huku ametulia kwenye kivuli cha nyumba yake iliyokuwa imepinduka upande mmoja. Ilikuwa na dalili za kuanguka wakati wowote ule. Aliposikia mngurumo wa gari akasimama kujua ni nini hasa kilichotokea. Dada yangu alikuwa ndani ya nyumba hiyo alitanmtayarishia chamsha. Akatoka na kusimama kwenye mlango wa nyumba. Hakujua ni nani waliokuwa wamewatembelea.

Nililigeuza gari mara moja na kumwambia kaka yangu ashuke. Tukaelekea mahali dada yangu alipokuwa kasimama na kumshika mkono ghafla. Alikuwa mnyonge wala hakuitaji kushikwa na watu wawili. Tulidhani angeghahiri amri lakini alikuwa tayari kuondoka. Nywele zake zilikuwa za kitim tim na chafu kutokana na kazi nyingi alizokuwa akifanya. Nikamhurumia. Bwana Tamaa hakuweza kuamini aliyokuwa akishuhudia. Kitambo aanze kupiga kelele,

tulikuwa tumetoweka kwenye makao yake na dada yangu mkononi. Tukaelekea nyumbani kwetu. Tulikuwa tumekuja kuharibu tamaduni mbaya. Tamaduni ambazo zinakandamiza na kukatisha ndoto za wasichana wa umri mdogo sana. Baba yangu hakuweza kuongea kitu chochote alipotuona na dada yangu. Aliamini kuwa wakati wa kuacha tamaduni za kale ulikuwa umewadia kwani aliweza kushuhudia mazao ya elimu. Kwa mara ya kwanza, dada yangu aliweza kuona jambo lisilo la kawaida. Alifurahi sana nilipomwambia kuwa angeweza kuendelea na masomo yake ya darasa la saba. Kaka yangu naye alikuwa tayari kuendelea na masomo yake ya kidato cha pili. Kwa vile nilikuwa najua kuwa pengine mzee yule angekuja kumchukua dada yangu wakati wowote, niliamua kumpeleka kusomea katika shule ya mjini nilikokuwa naishi. Tukaanza kuishi naye. Kaka yangu naye alijiunga na shule ingine ya bweni mjini pia. Baba yangu ndiye aliyebakia nyumbani. Nikamtafutia wafanyakazi na kisha nikamjengea nyumba na kumnunulia kila kitu alichohitaji. Akapata mwamko mpya wa mawazo.

# SURA YA KUMI

Ilikuwa takriban miaka sita sasa baada ya kuwa mdogo wa mkurugenzi mkuu wa kampuni ya Kikwetu na Kigeni. Mambo mengi yalikuwa yametendeka. Baba yangu alikuwa ameacha kazi kwenye kampuni ya Ujadi Mills. Jambo kuu lililochangia yeye kuacha kazi ni umri wake uliokuwa tayari umefikia kikomo. Kazi za pale kwenye kampuni zilihitaji nguvu za barobaro ambazo hakuwa nazo kwa sasa. Jambo la pili likawa, alikuwa tayari keshapata pesa nyingi na hakukosa chochote alichohitaji kwani kila mwisho wa mwezi nilikuwa nikimletea pesa na nyingine nikamwekea akiba. Kwa sasa maisha yake yalionekana kuwa mazuri zaidi hata kinyume cha matarajio yake ya awali. Hali yake ya afya ilikuwa inaumbika kila siku na kuwa nzuri. Magonjwa yalikuwa hadithi kwake. Kila nilipoenda nyumbani hakusita kunihimiza na kunipongeza kwa kazi nzuri niliyofanya. Nami sikukosa kumshauri kuhusiana na tamaduni zenye ukweli na umuhimu na zile hazifai kamwe kuigwa. Alikuwa akifurahia sana. Nikajua nitarithi baraka kutoka kwake; kwani baraka za mzazi zina manufaa mengi sana.

Kampuni ya Ujadi Mills iliweza kuhamishwa kutoka mji wa Weusisi hadi mji mkuu wa Zama. Sadfa iliweza kuifanya kujengwa karibu na kampuni ya Kikwetu na Kigeni. Maana tulikuwa tunafanya kazi ambazo zilikuwa na uwiano, mara nyingi tungefanya mambo kwa pamoja. Tukawa kama ndugu wawili wa mama mmoja. Urafiki kati ya wafanyakazi wa kampuni hizi mbili ulikuwa wa chanda na pete. Kwa ushirikiano huo, tuliweza hata kuongeza faida kutoka kwa kazi tulizokuwa tukifanya. Naam, kama wasemavyo wahenga kuwa umoja ni nguvu usambe ni utajiri. Tulithamini kila mmoja kutoka pande zote. Kampuni hii ilipohamia mjini Zama, ilichukua wafanyakazi wengine wapya kutoka mjini. Bila shaka kazi za mjini zilihitaji

kiwango fulani cha elimu ambayo watu kama Kinyale, Mzee Kitumbo, Lewa, Mabuti, na wengine hawakuwa wamefikia. Ingawa hawakufukuzwa kabisa kwa kuachishwa kazi, Bwana Kolea aliweza kuwaacha na sehemu fulani waliyoikuza kuingiza kipato. Bwana Kolea, Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Ujadi Mills alikuwa amefikia umri wake wa kuacha kazi na pengine kustaafu. Alikuwa na lengo la kumwachia Tanasha uongozi wa kampuni hii lakini alidinda akisema kuwa ilikuwa mbali na nyumbani. Bwana yake Tanasha hakutaka ahamie kwenda kukaa mjini kwa sababu kulikuwa na mengi ya kufanya nyumbani. Alipoona kuwa binti yake Karembo alikuwa amehitimu masomo ya chuo kikuu, akamshauri Bwana Kolea kumwajiri Karembo badala yake. Ushauri wa Tanasha ulichukuliwa na Bwana Kolea mara moja. Akampa Karembo usimamizi wa kampuni ya Ujadi Mills.

Mara kwa mara tulikuwa tukikutana na Karembo katika hafla mbalimbali baina ya kampuni hizi mbili. Tukawa marafiki wa uta na upote kama sio chanda na pete. Bwana Taru naye aliweza kuridhishwa na uongozi wangu wa kampuni ya Kikwetu na Kigeni. Kwa miaka saba sasa alikuwa amepata faida zaidi ya vile aliwahi kupata kutoka alipoanzisha kampuni hiyo. Akaamua kunipandisha cheo basi nikawa Mkurugenzi mkuu. Kipato changu cha pesa kikaongezeka sawa na majukumu. Nikajua kuwa polepole ya kobe humfikisha mbali. Ufanisi hauji kwa siku moja tu ila kwa jitihada za mja za kila siku. Naye mungu hamtupi mja wake.

Tumaini alikuwa katika mwaka wake wa tatu katika chuo kikuu kusomea udaktari. Bidii zake za mchwa katika masomo ziliweza kumsadia sana. Niliweza kumlipia karo ya chuo kikuu. Naye hakusita kunishukuru wakati alipokuja kwangu hasa katika ziara zake. Akawa kama mtoto wangu wa kwanza kwenye familia isiyo na mama mzazi.

Dada yangu naye aliweza kumaliza masomo yake ya shule ya upili. Ingawa hakuweza kuendelea na masomo ya chuo kikuu kwa sababu alikuwa katosheka na hayo, alipata mchumba aliyesoma sana na aliyekuwa na mali. Akamwoa kutokana na urembo wake aliokuwa kajaliwa na maulana. Wakaishi kwa furaha si haba kwenye maisha yao ya ndoa. Akameza tembe yake ya ndoa.

Wakati wangu wa kutafuta mchumba uliwadia. Marafiki zangu tuliokua pamoja walikuwa na familia. Nilihisi kuwa nilikuwa tayari nimefanya mambo yaliyokuwa muhimu hasa kwa familia yetu. Nikaamua kumwendea baba ili kupata ushauri wake. Nilifika kwake bila kumwambia kuwa ningemzuru kwake kijijini. Nilipofika tukala na kunywa pamoja kama baba mzazi na mwanawe. Baadaye niliweza kumdokezea yaliyokuwa yamenileta huko kijijini. Akanitazama kwa tabasamu na kufurahi kwa hatua niliyochukua. Akasema, "Mwanangu, nilikuwa natarajia kusikia hatua kama hiyo kutoka kwako. Nilikuwa nasubiri wakati kama huu ufike nikiwa bado hai. Subira huvuta heri. Nakushukuru. Ningependa kukujulisha kuwa wazee wa ukoo wa jamii yako walikuwa tayari wameshakutafutia mchumba." Alisita alipofika hapo. Akaniangalia kwa umakini kisha akaendelea. "Je, ungependa kumwoa mwanamke mwigine ama utamwoa yule yule uliyehifadhiwa?" Akaniuliza. Nilikosa jibu la swali kama hilo. Kwa kawaida sikuwa nimemwona msichana aliyesoma kutoka kijiji chetu ambaye tungeambatana kimawazo. "Lazima nijue kwanza msichana ambaye wazee waliniwekea kama bibi yangu. Je wamjua?" Nikamwuliza baba yangu. Hapo alisita kidogo kisha akasema, "Hiyo huwa siri kati ya baba mtoto na mwanawe hadi wakati utakapoletewa mke wako kwenye nyumba yako. Lakini kwa kipindi kirefu nimeweza kutambua kuwa kuna mambo ambayo hata nikikulazimisha kuyafanya, hayana faida yoyote kwako. Tamaduni zetu zimeanza kupitwa na wakati. Wazee

walioganda na kushikilia tamaduni kandamizi bado wanalia umaskini hadi leo. Kama ninavyojua kwa sasa, wewe waitaji msichana wa hadhi yako bali sio bunga ambaye hajasoma. Uliyewekewa kama bibi yako hajapata masomo ya kigeni kama wewe," akamalizia. "Baba, mimi siwezi kumwoa msichana hajasoma. Nitamtafuta mwenye hadhi kama yangu kisha nimlete ' ungwatakki na tuoane," nikamwambia baba yangu. "Sawa mwanangu. Nami nakutakia fanaka na wema wa mwenyezi mungu upate binti malkia na mwenye adabu na heshima kwa wazazi wako pia," akasema baba yangu.

Kwa wakati huo nilianza kuona mabadiliko ya mawazo kutoka kwa baba yangu mzazi ambaye alikuwa ameshikilia tamaduni sana. Nikajua kuwa muda tu ndio uliohitajika ili kugeuza msimamo wa wale wengine walioshikilia tamaduni kandamizi. Kwenye kijiji chetu niliona ndoto ya mwamko mpya kwa namna mambo yalivyoendeshwa. Elimu ndio iliyokuwa ngome ya mwamko huo. Wazee wengine walihitaji kuona umuhimu wa masomo ili kubadilika. Kwa sasa familia yetu ilikuwa mfano bora zaidi kwa kila mtu katika kijiji chetu kwamba elimu ina manufaa mengi sana. Dada yangu alikuwa katika mstari wa kwanza kuelimisha watu kuhusiana na athari za ukeketaji na ndoa za mapema na lazima. Yeye aliweza kushirikiana na wamama wengine katika kampeni hizo. Waliokuwa na maneno ya kusema walimsema hadharani na wengine faraghani. Hakuna yeyote angemdharau kwani mali na elimu alikuwa nazo. Alikuwa akiwasimulia hadithi yake ya ndoa ya lazima na namna tulivyomruzuku kutoka kwenye shimo la unyonge wa ndoa ya mapema na lazima. Watu wengi, hasa wamama na wanarika waliweza kupata mgeuko wa mawazo.

Nilimhimiza Tumaini kujiunga naye katika kampeni kama hizo. Ingawa sikuwa na wakati mwingi wa kufanya hivyo, muda kidogo

niliopata ulikuwa unatosha. Kaka yangu pia aliweza kuwaambia watu kila alipokuwa kijijini. Mwamko mpya wa elimu uliweza kufikia wazee na wakaanza kuona kuwa walichodhania kuwa ukweli kilikuwa hakifaidi chochote. Tulifurahia sana kushuhudia mabadiliko sambamba na matarajio yetu. Waganga waliokuwa na sifa kubwa kubwa walianza kunyamaza mmoja baada ya mwingine. Mji wa Weusisi uliokuwa kituo cha kwanza cha wateja wa uganga ulipata habari ya unyonge wa uganga. Watu wakaanza kuwa wachache kila juma. Vijana waliokuwa na mazoea ya kuvuna walikokuwa hawajapanda wakalazimika kwenda shule na kuchukulia elimu kwa uzito wa kipekee. Huo ndio mwamko mpya kwenye kijiji kilichokuwa katika giza. Katika unyonge wa kukosa mkombozi wa ndoto zao.

Siku moja wakati nilipokuwa nimepumzika kwenye chumba changu niliweza kuona simba wa kiume na wa kike kwenye runinga. Simba hawa wawili walikuwa na mtoto wao mchanga sana ambaye bado hakuweza kuwinda. Alikuwa mnyonge sana kutokana na umri wake mdogo. Kwenye msitu mkubwa huo, kama angeachwa peke yake pengine angeuawa na wanyama wengine wenye nguvu zaidi kama tembo au pengine kuwa chakula cha chui. Wakati mmoja simba wa kike ambaye ndiye aliyekuwa akimtafutia mwanawe chakula aligonjeka kiasi cha kwamba hangeweza kuwinda. Wakakaa kwa siku mbili bila chakula. Yule simba ndume alilazimika kwenda mawindoni kutafutia familia yake chakula. Akawa akifanya hivyo kila siku hadi wakati yule simba wa kike alipokuwa na afya yake kamili.

Niliona maisha yangu yalihitaji msaidizi wakati wa shida kama hiyo. Sio kila wakati ningekuwa na uzima wa mwili. Kuna wakati wa ugonjwa na wakati wa uzima, kila jambo na wakati wake. Nilihisi kuwa nilihitaji mchumba atakayenizalia watoto wangu. Sikusita kuwaza kuhusu Karembo ambaye alikuwa msichana mrembo kama

malaika. Alikuwa mweupe na aliyesoma kama mimi. Nikaona kuwa alikuwa na uwiano na mimi. Nikaanza kumwalika kwangu mara kwa mara. Hakupinga kuja kwangu hasa wakati tulipokuwa kwenye likizo. Siku zikasonga. Urafiki kati yangu naye ukawa kama wa mama kwa mwanawe. Kila wakati ungemwona Karembo nami nilikuwa karibu. Akitoka kazini tulitoka pamoja. Wakati mwingine tungetumia gari moja, lake au langu kwenda kazini au kutoka kazini. Tulifanya hivyo kwa muda wa miezi mitatu.

Nilipoona kuwa tumekuwa marafiki kwa muda tosha wa kuweza kujuana, nikaamua kumwambia wazi jambo lililokuwa moyoni. Nilitaka tufunge ndoa. Nilikuwa na uhakika kuwa Karembo hangenikataa kutokana na namna nilivyomjua. Wakati nilipomwambia kuhusiana na uchumba wangu, alitabasamu kama kwamba lilikuwa jambo alilotarajia. Akanieleza kuwa yeye tayari alinichukua kama mume wake na alisuburi tamko langu tu. Nikafurahi sana. Baada ya majuma mawili tuliweza kufunga ndoa. Tukaenda kuwaona wazazi ambao walitubariki na kufurahia pamoja nasi. Maisha yetu yakapata mwelekeo mpya na kuanza maisha ya ndoa yaliyokuwa yenye furaha na upendo wa kweli. Tukajaliwa na watoto watatu, wavulana wawili na msichana mmoja.

Kwenye maisha yetu ya uzazi hatukukoma kuwaelimisha wazee na wamama wa kale kuhusiana na umuhimu wa kuacha tamaduni mbaya. Tulikuwa katika mstari wa kwanza kuwasaidia watoto wanyonge na ambao wazazi wao hawakuwa na uwezo wa kuwaelimisha. Mola alitujalia tukaweza kufungua shule ya kuwasaidia watoto yatima na wale ambao walikuwa wametoka kwenye familia maskini. Shule hiyo ilikuwa ya bweni na ilijengwa katika kijiji chetu; Kilimoni. Watu waliweza kubadilisha mawazo yao na kuamini elimu na dini ya kigeni zilikuwa na umuhimu mkubwa

zaidi. Nikafikia ndoto yangu ya maisha. Ndoto ya kuona watu wa jamii yetu wakitenda mambo ya kuleta maendeleo lakini sio mambo ya kuangamiza maono ya vijana. Watu waliweza kutoka kwenye umaskini kwa sababu ya kuelimisha watoto wao. Hivyo ndivyo tulivyotakiwa kuishi. Katika mambo halisi ya maisha wala sio ufukara wa kujitakia. Huo ndio uhalisia wetu. Kila mja akajimezea tembe yake ila wakati huu ilikuwa tamu na ilileta tiba kamili.